# Nipashe
Jumanne Februari 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580157
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mwanajeshi JWTZ kortini tuhuma kumuua kwa risasi 19 mpenzi wake

UKURASA 2




UKURASA 15

# MAKONDA AJICHONGEA

**ADAI** kutumia fedha za Tasaf nauli kwenda kuomba uongozi UVCCM, Rais ataka achunguzwe, azirejeshe ...

*Endelea ukurasa wa 2*




Rais John Magufuli akiwa na marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete pamoja na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akikata utepe kuzindua kipindi cha awamu ya tatu ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: IKULU**

## WADAIWA SUGU NHC KUANIKWA HADHARANI

UKURASA 3

# Shida ulawiti shuleni inavyotesa wanafunzi-2

UKURASA 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** YANGA YAGEUKIA POINTI ZA SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Makonda ajichongea kwa Rais Magufuli

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kurudisha fedha alizodai alinufaika nazo japo si moja kwa moja kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) ilhali hakuwa na sifa za kupewa fedha hizo.

Agizo hilo alilitoa jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na mfuko huo, utaotekelezwa katika halmashauri zote 185 Tanzania Bara na wilaya 11 za Zanzibar kwa gharama ya Sh. trilioni 2.032.

Kabla Rais Magufuli hajatoa uamuzi huo, Makonda alieleza kuwa alipata fedha kutoka kwa Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa na akazitumia kwenda kufanya kampeni za siasa mkoani Dodoma na anaamini zilitoka Tasaf.

"Ninamshukuru Mzee Mkapa kumwona bado anaendelea kufanya kazi, mfuko huu si tu alikuwa sehemu ya mwanzilishi.

"Mheshimiwa Rais, naomba niseme mbele yako kuwa mfuko huu wa Tasaf nimenufaika nao. Haikuwa moja kwa moja lakini. Mwaka 2012 wakati naomba nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Tanzania, Mzee Mkapa ndiye aliyenipa nauli ya kwenda Dodoma kwenda kuomba kura.

"Nina imani ilikuwa ni sehemu ya huu mfuko, kwamba alikuwa na moyo, pamoja na kwamba alikuwa mwanzilishi wa mfuko huu, lakini moyo wake haukuishia kwenye mfuko wa Tasaf, aliendelea kuhakikisha na mimi ananipatia nauli.

"Mheshimiwa Mkapa, kweli nilitumia kwa makusudi uliyonipatia hatimaye leo naendelea kufanya kazi ya utumishi kama ambavyo uliniotea," alisema Makonda.

Hata hivyo, akihutubia katika hafla hiyo, Rais Magufuli alimwagiza Makonda kurudisha fedha hizo, huku akianika vikwazo vilivyojitokeza wakati wa uhakiki wa kaya maskini, uliofanyika kuanzia Novemba mwaka 2015 hadi Juni 2017.

Rais alisema uhakiki ulibaini uwapo wa kaya hewa 73,561, akifafanua: "Kaya 22,034 zilithibitika kuwa wanakaya wake siyo maskini, hapa ninafikiri miongoni mwao ni kina Makonda ambao walizitumia hizi fedha kwenda safari ya Dodoma wakati siyo maskini.

"Ninaomba kama hili ndiyo ukweli, Makonda azirudishe hizi fedha, kama ni kweli alizitumia fedha za Tasaf, akaenda nazo

INAENDELEA UK 8



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiruka maji machafu yanayotiririka kutoka kwenye takataka zilizotelekezwa katika soko la Ubungo Mawasiliano, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanajeshi kortini madai mauaji ya askari mwenzake

**Na Said Hamdani, LINDI**

ASKARI wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Praiveti Pascal Lipita (28), anayefanya kazi katika wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kikosi cha 843 Nachingwea, mkoani Lindi, amefikishwa kwa tuhuma za mauaji.

Lipita (28) anatuhumiwa kumuua askari mwenzake, Praiveti Baserisa Ulaya kwa kile kinachodaiwa kuwa wivu wa kimapenzi.

Mtuhumiwa huyo alifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa huo, Maria Batulaine, na kusomewa shtaka linalomkabili.

Mwanasheria wa Serikali, Abdulrahman Mohamed, alidai kuwa askari hao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na kwamba wivu ndio unaodaiwa kusababisha mauaji hayo.

Mwanasheria huyo wa serikali alidai kuwa mshtakiwa alifanya mauaji hayo Februari 10, mwaka huu, majira ya Saa 12;00 jioni wakiwa kambi ya Nang'ondo.

Alidai kuwa siku hiyo ya tukio, wakiwa kambini hapo, mshitakiwa akiwa na silaha, alimmiminia askari mwenzake risasi 19 kisha kuchakaza mwili wake na kumkatisha uhai.

"Baada ya kumpiga risasi moja na kuanguka chini, mshtakiwa aliendelea kummiminia zingine mwili wote na kumpotezea uhai wake," alidai Mohamed.

Mwanasheria huyo alidai kuwa kutokana na kitendo hicho, mshtakiwa alifanya kosa chini ya kifungu cha 196 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 marejeo mwaka 2002.

Hata hivyo mshtakiwa hakutakiwa kukubali wala kukataa mashtaka yanayomkabili kwa kuwa mahakama hiyo kisheria haina mamlaka ya kusikiliza kesi zinazohusu mauaji.

Mshtakiwa baada ya kusomewa mashtaka hayo, alipelekwa rumande na atafikishwa tena mahakamani Machi 2, mwaka huu, kesi itakapotajwa.

## Tembo watishia maisha wananchi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MAKUNDI ya tembo yamevamia katika vijiji vya kata sita za Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro na kusababisha uharibifu wa mazao na kutishia maisha ya wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Florent Kyombo, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kufikishiwa malalamiko na wananchi juu ya kuvamiwa na wanyama hao.

Wananchi hao wamelalamikia tembo hao kuvamia kwenye vijiji vyao na kuharibu mazao na kuhatarisha maisha yao wanapokuwa shambani na katika makazi yao.

Kyombo alisema mwishoni mwa mwaka jana zilipoanza mvua, kumekuwapo na ongezeko la tembo katika baadhi ya maeneo ya vijiji wakitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Alisema kuongezeka kwa wanyama hao maeneo ya vijijini pia kimechangiwa na mvua za mafuriko zilizotokea wiki tatu zilizopita katika baadhi ya maeneo ya hifadhi wanakoishi, hivyo kuyahama maeneo hayo kwenda maeneo yasiyotuama maji na kutafuta malisho.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na Wilaya ya Mvomero kupakana na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, kuna shoroba nyingi ambazo tembo kwa nyakati tofauti huingia kwenye maeneo ya vijiji vya wananchi kutafuta malisho.

Kyombo alisema hadi sasa vijiji vya kata sita za Doma, Lubungo, Melela, Mangae, Msongezi na Dakawa kumekuwa na tembo wanaotoka kwenye hifadhi hiyo. Alisema uvamizi huo umesababisha uharibifu wa takribani ekari 2,000 za mazao ya wananchi.

Alisema tembo hao wamekuwa wakiingia zaidi katika vijiji vya Kata ya Lubungo lakini hawasababishi madhara ya kuopoteza maisha ya watu isipokuwa uharibifu wa mazao.

Baada ya kuliona tatizo hilo, wilaya wakishirikiana na askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa) na wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wameanza kuwaswaga kwa kuwatoa tembo kwenye maeneo ya wananchi kwa kuwarudisha hifadhini.

Pamoja na hayo alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wa maeneo ya vijiji vya kata hizo wakiwamo wanaopenda kutembea nyakati za usiku kuendelea kuchukua tahadhari kwani nyakati hizo Tembo wamekua wakitoka kwenda kutafuta malisho na hivyo kuweza kuwadhuru .

Aliwashauri kufuata maelekezo ya wataalamu wa wanyamapori kuhusu namna ya kujikinga na Tembo kwa kupanda pilipili kuzunguka mashamba yao ikiwa na kufuga nyuki kwani pilipiki na nyuki si rafiki wa wanyama hao kuweza kuwakaribia ikiwa na kuacha kulima karibu na makazi mazao yanayowavutia kama maboga na matikiti maji.

## HABARI KITAIFA



Meneja wa Miradi wa Kampuni ya CRCEG, Mhandisi Jamal Mruma (kushoto), akiwaonyesha waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, jana, vifaa vya ujenzi vinavyotumika kwenye mradi wa barabara ya Feri- Kibada, inayounganisha na daraja la Nyerere wilayani Kigam-

# Wadaiwa sugu NHC kuwekwa hadharani

**Na Beatrice Moses**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limekusudia kutangaza majina ya wapangaji wenye madeni sugu zikiwamo taasisi za umma, wakala wa serikali na kampuni binafsi, ikiwamo na waliohama na bila kulipa kodi.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Huduma kwa Jamii NHC Makao Makuu kwenye vyombo vya habari jana, limebainisha kuwa baada ya kuwatangaza wadaiwa hao shirika litaanza kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Huduma kwa Jamii NHC Makao Makuu, Yahya Charahani, alithibitisha kutoa matangazo hayo, ambayo pia yameonya wapangaji ambao waliingia kwa njia zizizo sahihi kutakiwa kijisalimisha.

Taarifa zaidi katika tangazo hilo zinabainisha kuwa NHC inakusudia kuanza kufanya uhakiki wa wapangaji wake wote nchi nzima.

"Hili limeanza wiki hii na litaendelea muda wote hata siku za mwisho wa wiki na sikukuu ili liweze kukamilika mapema mwezi Machi 2020, wapangaji wote wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa maofisa wa shirika ambao muda wote watakuwa wamevaa vitambulisho vya kazi," ilieleza taarifa hiyo.

NHC pia imewashukuru wapangaji waliokamilisha kulipa kodi zao na malimbikizo, pamoja na wengi waliojisalimisha katika ofisi mbalimbali za shirika hilo na kuomba muda wa kukamilisha kulipa madeni yao.

Hatua hii ya NHC inakuja ikiwa ni siku chache baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuuagiza uongozi wa Bodi ya NHC, kuhakikisha wapangaji wanalipa madeni yao ifikapo Mei 30, mwaka huu.

Alitoa agizo hilo wakati alipozungumza na viongozi na wajumbe wa Bodi ya Shirika hilo kwenye kikao kilichofanyika ofisini kwake, jijini Dar es Salaam.

"Taasisi zote za serikali ambazo zimepanga kwenye nyumba za shirika ni lazima zilipe madeni. Chombo chochote cha serikali kinaishi na bajeti, kwa hiyo hata kama wamejenga ya kwao, walipaswa walipe kabla hajahama."

Alitaka pia apatiwe orodha ya taasisi za serikali zinazodaiwa ili awafuatilie; "Nitawaita makatibu wakuu wao mmoja mmoja. Hao wadaiwa binafsi wachukulieni hatua stahiki."

Waziri Mkuu alitaja madeni ambayo taasisi za serikali zinadaiwa yanafikia Sh. bilioni 4.3 na kama zitalipwa zote zitalisaidia shirika kuendelea na mpango wake wa ujenzi wa nyumba nafuu kwenye maeneo mbalimbali.

# Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Baada ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Denice Mrashani, kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, alisema mahakama hiyo imejiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa anayo hatia dhidi ya kosa analoshtakiwa nalo, huku akimpatia fursa ya kuiomba mahakama kumpunguzia adhabu.**

**Na Daniel Limbe, CHATO**

MKAZI wa Kata ya Buseresere wilayani Chato mkoani Geita, Medi Maliatabu, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita.

Imeelezwa mbele ya mahakama ya Wilaya ya Chato kuwa mshtakiwa alikamatwa na polisi Oktoba 7, mwaka 2019, na kwamba baada ya mahojiano ya awali alikiri kufanya mapenzi na mtoto huyo(jina tunalo), ambaye ni mwanafunzi wa shule ya msingi Maweni Kata ya Buseresere.

Mwendesha Mashtaka wa serikali, Erasto Anosisye akishirikiana na Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Mauzi Lyawatwa, waliieleza mahakama hiyo mshtakiwa alitenda kosa la kumbaka mtoto aliye chini ya miaka 18 kinyume cha sheria.

Walidai tendo la kufanya ngono na mtoto ni kosa la jinai ambalo linaangukia kwenye kifungu cha sheria namba 130(1) na 2(e) pamoja na kifungu namba 131(1) cha sheria ya makosa ya jinai.

Waliiomba mahakama iwapo itamkuta na hatia mshtakiwa apewe adhabu kali kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ubakaji kwa watoto, ambavyo vimekuwa vikidhoofisha malengo ya serikali ya kumpatia elimu mtoto wa kike, magonjwa ya ngono na hata mimba za umri mdogo.

Baada ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Denice Mrashani, kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, alisema mahakama hiyo imejiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa anayo hatia dhidi ya kosa analoshtakiwa nalo, huku akimpatia fursa ya kuiomba mahakama kumpunguzia adhabu.

Katika utetezi wake, Maliatabu ameomba kupunguziwa adhabu kwa kuwa hana ndugu karibu na kwamba amekaa gerezani akiwa mahabusu muda mrefu.

Mahakama hiyo ilimhukumu kifungo cha miaka 30 jela ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye kufanya vitendo hivyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA "BIOMETRIC VOTER REGISTRATION" (BVR) KATIKA MIKOA YA DAR ES SALAAM NA PWANI**

**TAREHE 14 - 20/02/2019**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. kuwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia Teknolojia ya Biometric Voter Registration (BVR) litafanyika kama ifuatavyo:

1. **SIKU:** Tarehe **14/02./2020. hadi tarehe 20/02/2020** Mikoa ya Dar es Salaam naPwani
2. **VITUO:** Zoezi la Uboreshaji litafanyika katika vituo vilivyoko katika Mitaa na Vijiji katika Kata zote za mikoa hiyo
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA UTAHUSISHA MAMBO YAFUATAYO:-**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wote wapya ambao ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria watakaokuwa wametimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri wa Miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2020
2. Mpiga Kura ambaya anayo Kadi ya Mpiga Kura ya zamani na imeharibika, imefutika maandishi au kukosewa taarifa zake anatakiwa kwenda kituoni kwa ajili ya kupatiwa kadi mpya
3. Kuandikisha wale wote ambao wanazo sifa lakini hawakujiandikisha mwaka 2015'
4. Mwananchi ambaye ni mara ya kwanza kuandikishwa,atakapofika Kituoni atachukuliwa alama ya vidole vyote kumi vya mikono yote miwili na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
5. Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni. Watu wenye Ulemavu, Wagonjwa, Wajawazito, Akina Mama wanaonyonyesha na Wazee watapata kipaumbele.
6. Mwananchi anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Uandikishaji wa Kituo.
7. Wapiga kura wa Kata ya Kibuta, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoani Pwani waliojiandikisha kwenye zoezi la Majaribio tarehe 29 Machi 2019 hadi tarehe 4 Aprili, 2019 wanatakiwa kwenda vituoni tena ili taarifa zao ziweze kuingizwa rasmi katika Daftari la Kudumu la awapiga kura

**KUMBUKA:**

- SIFA MUHIMU YA KUKUWEZESHA KUTUMIA HAKI YAKO YA KUCHAGUA KIONGOZI UNAYEMTAKA NI KUJIANDIKISHA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA
- NI KOSA LA JINAI KUHARIBU KWA MAKUSUDI AU KUUZA KADI YAKO YA KUPIGIA KURA
- TANZANIA YA SASA NA IJAYO IKO MIKONONI MWAKO, NENDA KAJIANDIKISHE ILI UWEZE KUPIGA KURA UCHAGUZI MKUU 2020
- KURA YAKO NI KADI YAKO, NENDA KAJIANDIKISHE.

215632302

Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar es Salaam
Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.

RIPOTI MAALUM -2

# Shida ulawiti inavyotesa wanafunzi

## ■Mwalimu aibua janga lililojificha
## ■Mzazi: Mimi namwachia Mungu



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu

**Na Elizabeth Zaya**

***SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, iliibua mambo yanayoenda kinyume cha staha ya binadamu, yanayofanywa na baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi zilizoko wilayani Mkuranga mkoani Pwani na namna taarifa ya mshtuko zilizoufikia uongozi wa shule na hatua za awali kukuchuliwa. Endelea kupata picha halisi ya kinachoendelea:***

---

Mwalimu wa nidhamu katika shule yenye wanafunzi 2,284, Adeline Kulele, alisema wanafunzi wengi shuleni kwake wamekuwa wakibainika kufanyiwa vitendo hivyo wanapopewa adhabu shuleni.

"Wengi huwa tunawabaini kwamba wanafanyiwa vitendo vya ulawiti pale unapotaka kuwachapa, siku nyingine mtoto akifanya kosa, ukitaka kumchapa, anapiga kelele akisema 'mwalimu huku nyuma kunauma'," alisema.

Mwalimu huyo aliendelea na simulizi yake namna uhalisia unavyojianika, akimtaka: "... ukimuuliza amefanya nini, ndiyo anaanza kueleza na ukiwabana wanatajana wote.

"Tunaowabaini sana huwa ni hawa wadogo wa madarasa ya mwanzo na tunahisi wakubwa wenyewe huwa wanajitahidi kujificha kwa sababu wanajielewa."

**MABADILIKO**

Mwalimu huyo alibainisha kuwa baadhi ya wanafunzi katika shule hiyo wameanza kubadilika tabia na hata namna ya kutembea.

"Vitendo hivi kwa kweli vinatishia usalama wa watoto na wengine hata ukiwaona tabia zao zimeanza kubadilika, hata namna wanavyotembea pia inaashiria kuna tatizo, inasikitisha sana kwa kweli.

"Kama kuna jambo la kufanyika haraka kuwaokoa watoto hawa, tunaomba lifanyike, tuwekewe hata uzio tu hapa shuleni," mwalimu huyo alishauri.

Kulele alisema tayari wameshaanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwaelimisha wanafunzi juu ya madhara ya vitendo hivyo, kuita wazazi na kujadiliana nao namna ya kuwasaidia watoto wao ikiwamo kuwa karibu nao na kuwapeleka vituo vya afya kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi zaidi.

Mwanafunzi wa darasa la saba katika shule hiyo (jina tunahifadhi), alidai kuna kundi la wanafunzi shuleni hapo, ambalo limekuwa likiwashawishi wanafunzi wenzao kwenda porini na kufanyiana vitendo hivyo.

"Kuna kundi la wanafunzi wakubwa wa darasa la sita na la saba ambao huwa wanawashawishi wengine hasa wale wadogo, wanaenda kwenye mapori yanaitwa 'Mambonyuma', huko ndiko wanafanyiaga hiyo michezo michafu na hata ukiwaambia hawasikii.

"Na ukiwa unawaambia sana, wanaanza kukutishia na wanakuambia 'unajifanya kimbelembele tutakuonyesha', na ndiyo maana huwa wanawaonea hao wadogo ambao wakiwatishia wanaogopa.

"Na kule kwenye hayo machimbo, kuna mabwawa ya maji ambayo huwa wanawadanganya wanawachukua kwenda kuogelea, lakini wakifika huko wanaanza kuwaingilia."

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Mohamed Mazoea, alikiri kuwapo kwa kadhia hiyo na tayari kamati yake ilishaijadili na kukubaliana hatua za kuchukua kuidhibiti.

"Ni kweli hilo tatizo lipo, lakini tuligundua kwamba mojawapo ya sababu zinazochangia watoto kufanya vitendo hivyo ni malezi mabovu kutoka kwa wazazi au walezi wao, na tulishawaita wazazi na kuzungumza nao.

"Pia, shule yetu ni ndogo sana kimiundombinu, haiendani na idadi ya wanafunzi, tulishakaa kikao na kulizungumza hili, tuliwahimiza wazazi kuhakikisha wanashirikiana na walimu katika ulinzi wa watoto," alisema.

**MSAMIATI MPYA**

Udadisi wa Nipashe ulihamia kwenye shule nyingine iliyoko kilometa 24.8 kutoka mjini Mkuranga, ambayo Mwalimu Mkuu wake, Victor Marisha, alisema haijasalimika katika kashfa hiyo.

Alisema walibaini kuwapo kwa vitendo hivyo baada ya kuwabana baadhi ya wanafunzi waliokuwa wametoroka shuleni na katika maelezo yao, waliibuka na msamiati mpya kwa walimu.

"Siku moja watoto walikuwa wametoroka, tulivyoitisha majina, tukawabana wanafunzi wataje wenzao ndipo wakaropoka na hilo, wakitaja na eneo ambalo huwa wanalitumia kufanya hivyo vitendo.

"Walitajana mmoja mmoja na watu ambao wanawafanyia wenzao, vitendo vinafanyika sana kabla ya muda wao wa kuingia darasani kufika, kwa sababu hapa tunatumia 'shifti' kutokana na uchache wa vyumba vya madarasa.

"Tuliwahoji kwa undani zaidi na tukabaini wanaofanyiwa sana ni watoto wadogo wa darasa la pili, tatu na nne. Mwanzoni tulikuwa hatuelewi vizuri maelezo yao, kwa sababu walikuwa wanazungumza maneno mageni kidogo.

"Wanatumia maneno kama vile 'kubambiana', tulipowabana zaidi ndiyo tukaelewa kwamba ndiyo ulawiti wenyewe. Ilibidi tuwaite wazazi wao na kuwaeleza na sasa hivi tunaendelea kuwapatia elimu juu ya athari ya vitendo hivyo na pia tuliripoti katika uongozi wa serikali za mitaa.

"Na shida kubwa nyingine ya hapa ni ukosefu wa uzio, watoto ni wengi na wanapotoka kwenye mapumziko, kawaida lazima wanunue vitu vidogo vidogo vya kula na huo ndiyo muda wanautumia kwenda huko," alieleza.

**"Kuna kundi la wanafunzi wakubwa wa darasa la sita na la saba ambao huwa wanawashawishi wengine hasa wale wadogo, wanaenda kwenye mapori yanaitwa 'Mambonyuma', huko ndiko wanafanyiaga hiyo michezo michafu na hata ukiwaambia hawasikii.**

Nyayo za udadisi wa Nipashe zilitinga kwenye shule nyingine iliyoko kilometa 24 kutoka mjini Mkuranga na kuzungumza na Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Tukae Bakari, ambaye alikiri kuwapo kwa vitendo hivyo kwa baadhi ya wanafunzi wao.

Alisema baada ya kupata taarifa za kuwapo kwa vitendo hivyo, walifanya uchunguzi na kubaini wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo kwenye maeneo ya mapori.

"Yaani dada huku hali ni mbaya, watoto wengi hawashikiki, wana mambo makubwa kuliko umri wao, tumeongea mpaka tumechoka, mtoto mwingine aliletwa hapa juzi na mzazi wake, anaongea bila wasiwasi kwamba hata shule yenyewe hataki tena.

"Tunajitahidi kadri tunavyoweza kuzungumza nao, kuzungumza na wazazi wao, lakini hali bado ni ngumu, hawaogopi mtu yeyote. Watoto wengi hapa wanafundishana ujinga wenyewe kwa wenyewe.

"Wakitoka kuona huko majumbani kwao kwenye televisheni, basi wanaona na wao wajaribishe, watoto wanalawitiana hapa, hata dawati la jinsia wameshakuja kutoa elimu hapa mara kadhaa na hata sisi tunaendelea kuzungumza nao," alisema.

Pili Bakari, mkazi wa Kimanzichana wilayani humo, alisema vitendo hivyo vinatishia usalama kwa watoto, akieleza kuwa vinachagizwa na wilaya hiyo kuwa na mapori.

"Mimi mwenyewe ni mzazi, kiukweli na sisi tunashtushwa na hivi vitendo vya watoto hawa kulawitiana, tumeshakata tamaa na watoto wetu kwa sababu hili wimbi limekuwa kubwa.

"Na kama unavyoona huku kwetu mapori ni mengi, tunaomba lifanyike jambo lolote la haraka la kuwaokoa watoto wetu, hali si nzuri kwa kweli," alilalamika.

Mtendaji wa Kata ya Kimanzichana, Said Abdalah Said, alisema tatizo la watoto kulawitiana lilisharipotiwa katika ofisi yake na tayari walishaitisha kikao na kuzungumza na wazazi na kupeana mikakati ya kulidhibiti.

Vilevile, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Vianzi wilayani humo, Omary Kimbache, alisema walibaini kuwapo kwa kadhia hiyo katika eneo lake la kazi mwaka jana na hatua kadhaa zimechukuliwa kupambana na vitendo hivyo.

"Hili tatizo hapa kwetu liliwahi kuripotiwa mwaka jana, kulikuwa na pori fulani hivi, watoto walikuwa wakitoroka katika vipindi vya masomo na kwenda kujificha huko na kufikia hatua hiyo ya kufanyiana huo uchafu.

"Baada ya kupata taarifa hizo tulifyeka lile pori na mpaka Januari hii (2020), halijaripotiwa tukio la aina hiyo kutokea tena," Kimbache alisema.

***ITAENDELEA KESHO**

# Serikali kupunguza bei ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema serikali iko katika utafiti kuhakikisha matumizi ya gesi kama mbadala wa kuni na mkaa yanakuwa ya bei nafuu kwa wananchi wote.

Amesema tatizo kubwa kwa sasa ni kukithiri kwa ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, hivyo kuna haja kukabiliana nalo na suluhu ya haraka na rafiki kwa mazingira ni matumizi ya gesi.

"Tunakuja na programu ya kulipia gesi kadri unavyotumia (paymetre)," Zungu alisisitiza alipokuwa anazungumza na wahariri na waandishi wa habari baada ya kutembelea baadhi ya vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana.

Waziri huyo alisema kwa siku mwananchi anatumia si chini ya Sh. 1,500 hadi 2,000 kununua mkaa, na mkakati wa serikali ni kuhakikisha gesi inagharimu kati ya Sh. 900-1,000 kwa siku kwa matumizi ya kawaida ya nyumbani.

"Tunataka bei ya gesi ishuke ili wateja wawe wengi ili kunusuru mazingira yetu," Zungu alisema.

Katika hatua nyingine, waziri huyo ametoa tahadhari kwa wananchi kuhusu ununuzi wa mifuko mbadala aina ya Non-Woven ambayo haikidhi viwango vilivyoainishwa.

Alisema mifuko hiyo ni lazima ikidhi viwango vya ubora vilivyoainishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ikiwa ni pamoja na kuwa na uzito usiounguza GSM 70, iwe irejelezwa, ionyeshe uwezo wa kubeba na iwe imethibitishwa na TBS.

"Nawasihi wananchi wetu kuwa makini na mifuko isiyokidhi viwango vya ubora kwa kuwa ina athari kwa mazingira na kiuchumi.

"Mifuko inayotengenezwa nchini, mingi inakidhi viwango vilivyoweka na hivyo inachangia ulipaji wa kodi na maendeleo ya taifa letu. Mifuko isiyokidhi viwango inatoka nchi jirani na inaua viwanda vya Tanzania," alisema.

Alisema walinzi wakubwa wa mazingira ni wananchi wenyewe, hivyo akatoa wito kwa umma kutoa taarifa za wanaokiuka Sheria ya Mazingira wachukuliwe hatua.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Justice Kijazi (kulia), akimpongeza Mtendaji wa Kata ya Makilawa, Salida Shinu, kwa kushika nafasi ya kwanza kwenye makusanyo kati ya kata 28, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani jana. Shinu alikabidhiwa zawadi ya Sh. 250,000. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya Kabendera yazidi kupigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili mwandishi wa habari, Erick Kabendera, imepigwa kalenda mpaka Februari 24, mwaka huu baada ya hakimu anayesikiliza kesi hiyo kuwa na udhuru.

Awali mahakama hiyo iliruhusu mazungumzo ya mwisho kuhusu kukiri na kuomba msamaha tuhuma za kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 100.

Kesi hiyo imeahirishwa na Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na hakimu anayesikiliza kesi hiyo amepata udhuru.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Februari 24, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Kabendera alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Agosti 5, 2019.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa siku na mahali pasipofahamika mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu.

Alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari mwaka 2015 na Julai mwaka 2019, alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi.

Katika shtaka la pili, Kabendera anadaiwa kuwa mshtakiwa anakabiliwa na shtaka la ukwepaji kodi, zaidi ya Sh. 173,247,047.02.

Kabendera anadaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 19, 2019, mshtakiwa huyo alishindwa kulipa kodi kiasi cha Sh. 73,247,047.02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa, kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, mshtakiwa alitakatisha fedha kiasi cha Sh. 173,247,047.02.

# Hekta 191 zazalisha mbegu za michikichi

**Na Valentine Oforo, KASULU**

KATIKA kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa la kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA), wamefungua shamba lenye ukubwa wa hekta 191.7 kwa ajili ya kuzalisha miche ya michikichi, wilayani Kasulu, mkoani Kigoma.

Serikali, katika mwaka wa fedha wa 2017/18 ilitoa kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuiongozea nguvu ASA kuzalisha mbegu bora, zikiwamo za michikichi.

Mpaka sasa, Tanzania inatumia Sh. bilioni 675 kwa ajili ya kuagiza kati ya tani 400,000 mpaka 570,000 za mafuta ya kula.

ASA imeshazalisha miche 24,331 katika shamba la Kasulu.

Akiongea na Nipashe, Kaimu Meneja Mzalishjaji wa ASA, Benjamin Mwamfupr, alisema wameshagawa kiasi cha miche 2,000 nchini.

"Pamoja na uzalishaji huu, pia tunatekeleza mradi wa kuchimba kisima, wenye thamani ya Sh. milioni 30 ili kuhakikisha mbegu hizo zinalimwa kwa ustawi," alisema.

Aliongeza kuwa mbegu wanazozalisha, zinazoitwa 'Tenera' zina uwezo wa kuzalisha kati ya tani 2.5 hadi 3.6 kwa hekari.

Mikoa inayozalisha michikichi ni Tanga, Morogoro, Kigoma, Lindi, Mtwara, Mbeya, Tabora, Mpanda, Geita na Rukwa.

**"Pamoja na uzalishaji huu, pia tunatekeleza mradi wa kuchimba kisima, wenye thamani ya Sh. milioni 30 ili kuhakikisha mbegu hizo zinalimwa kwa ustawi," alisema.**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dar, Pwani jitokezeni daftari la wapigakura

WAKAZI wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wamepewa fursa ya kujiandikisha pamoja na kurekebisha taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura, yakiwa maandalizi ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Uandikishaji huo kwa mikoa hiyo ni sehemu ya utaratibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwaandikisha wananchi wote wenye sifa kwenye mikoa yote nchini kutumia haki yao ya kikatiba kuwachagua viongozi wanaowataka ngazi ya udiwani, ubunge na urais.

Mikoa kadhaa imeshatumia fursa hiyo kwa wakazi wake wenye sifa kujiandikisha kwa mara ya kwanza pamoja na wale ambao wanataka kurekebisha taarifa zao kufanya hivyo, huku uandikishaji huo ukitarajiwa kuendelea kwa mikoa iliyobakia.

Kwa mujibu wa ratiba ya NEC, uandikishaji wapigakura katika mikoa hiyo miwili ulianza Februari 14 na unatarajiwa kukamilika Februari 20, mwaka huu.

Maboresho ya daftari la kudumu la wapigakura ni hitaji la kisheria ambalo linaielekeza NEC kulitekeleza angalao mara moja kwa mwaka ili kuwawezesha wananchi kupata haki ya kushiriki kwenye mchakato wa kuwachagua viongozi.

Hata hivyo, kumekuwapo na changamoto kwa wananchi wengi kutokuwa na uelewa kuhusiana na mchakato wa uboreshaji wa daftari hilo.

Kimsingi, katika uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kinachofanyika ni kuwaandikisha watu ambao hawajawahi kuandikishwa awali ili washiriki kupiga kura kuanzisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kundi la pili ni la watu waliohama maeneo yao, hivyo taarifa zao kuhamishiwa katika makazi yao mapya. Wamo pia walioopoteza vitambulisho vyao vya kupiga kura au kuharibika ili wapatiwe vipya. Aidha, mchakato huo unahusisha kuwaondoa kwenye daftari watu waliofariki dunia.

Ikumbukwe pia kwamba wanaotakiwa kujiandikisha ni wenye sifa ya kuwa raia wa Tanzania, kuwa na akili timamu na wawe wametimiza umri wa miaka 18 au mhusika awe amefikisha umri huo siku ya uchaguzi wa mwaka huu.

Kwa hiyo mwananchi yeyote mwenye kitambulisho halali cha mpigakura ambaye hajahama eneo lake hatatakiwa kwenda kujiandikisha au kuboresha taarifa zake.

Tumelitolea ufafanuzi suala la wahusika na sifa zao kwenye mchakato wa kuboresha taarifa, kutokana na wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha, hivyo kujichanganya.

Tunaamini kuwa wananchi ambao hawakupata vitambulisho vya kupigia kura ambavyo kwa mara ya kwanza vilitolewa mwaka 2015 kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu vilivyotengenezwa kwa njia ya kielektrokini ya Biometric Voter Regisration (BVR) watajitokeza kujiandikisha.


Kuwa na kitambulisho hicho kunamwezesha kila mwananchi kutumia haki yake ya kikatiba kushiriki kuwachagua viongozi anaowataka pale unapotokea uchaguzi, ukiwamo uchaguzi mdogo ambao hujitokeza mara kwa mara kwa wabunge na madiwani.

Tunatoa wito na kuwahimiza wakazi wa mikoa wa Pwani na Dar es Salaam ambao wanahusika katika maboresho ya daftari la kudumu la wapigakura kuzitumia vizuri siku tatu zilizobakia kuanzia leo hadi alhamisi kwenda kwenye vituo vilivyowekwa kisheria wa ajili ya kijiandikisha au kuboresha taarifa zao.

Bila kufanya hivyo watapaswa kujilaumu wenyewe, kwa kuwa watakosa haki yao ya kikatiba ya kuwachagua viongozi, ambao wanawaona kuwa wanafaa kuwaletea maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi wazembe wawajibishwe

Na Beatrice Moses

AMRI iliyotolewa na serikali ya kukamatwa wazazi 375 katika Wilaya ya Rombo, watakaoshindwa kuhakikisha watoto wao waliochaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari, wanaripoti shuleni hadi kufikia mwezi ujao, itawashitua wazazi kutimiza wajibu.

Imeripotiwa na vyombo vya habari wiki hii kuwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, alitoa amri hiyo wakati akitoa taarifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari wanaanza masomo.

Mkuu huyo wa wilaya alibainisha kuwa watu wanacheza na elimu ili kukomesha hali hiyo ameagiza wazazi na walezi wote ambao watoto wao hawaripoti katika shule walizopangiwa hadi sasa, wakamatwe na kushitakiwa mahakamani. Hatua hii ya serikali itasaidia kuwezesha wazazi au walezi ambao hawaoni umuhimu wa watoto kwenda shule kuwajibika ipasavyo katika kufanikisha malezi ya watoto.

Ingawa kuna baadhi ya wazazi wanakwama kupeleka watoto shule kutokana na kuelemewa na hali ya ufukara, lakini hawa wanaopuuza haki ya mtoto kupata elimu, huku wakijituma kwenye masuala ya anasa na starehe, wengine wakiwatumikisha katika kutafuta kipato.

Rombo wameamua kuchukua hatua hiyo nzito, ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Godwin Chacha, alitaja kuwa kati ya wanafunzi 5,080 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, nusu hawajaripoti kwenye shule walizopangiwa.

Idadi hiyo ya waliofaulu katika Wilaya ya Rombo inatajwa kuwa ni sawa na ongezeko la wanafunzi 1,080.

Tatizo hilo la baadhi ya wazazi na walezi kuamua kuvunja haki ya mtoto kupata elimu haipo Rombo pekee, inapaswa kuchukuliwa na viongozi wa maeneo mengine nchini, itasaidia kuongeza idadi ya wasomi nchini.

Mafanikio katika elimu yanatarajiwa kufanikiwa kupitia ushirikiano kuanzia Serikali Kuu, wizara, wadau wa elimu, walimu, wazazi, walezi na wanafunzi husika.

Kumekuwa na juhudi nyingi za wazi ambazo zimekuwa zikifanywa kupitia ushirikiano huo kila mmoja kwa nafasi yake lengo likiwa ni kuhakikisha mafanikio yanafikiwa.

Kuna mambo kadhaa yanabainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ni matokeo ya kuhuishwa na hatimaye kufutwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo (1996), Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu (1999) na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Elimu Msingi (2007).

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na tathimini iliyofanywa ya miaka 19 ya utekelezaji wa Sera ya kwanza ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 pamoja na Sera nyingine mahusus za elimu na mafunzo, Tanzania imepata mafanikio makubwa katika sekta ya elimu. Mafanikio haya ni pamoja na kupanua wigo wa elimu katika ngazi zote, kuanzia elimu ya awali hadi Mafunzo ya elimu ya juu.

"Kwa kutumia taarifa zilizopo za miaka mbalimbali, idadi wa watoto wanaojiunga na elimu ya awali imeongezeka kutoka asilimia 24.7 mwaka 2004 hadi 37.3 mwaka 2013 na kiwango cha watoto walioandikishwa katika elimu ya msingi imeongezeka kutoka asilimia 77.6 mwaka 1995 hadi asilimia 96.2 mwaka 2013," imebainishwa kwenye sera hiyo.

Kiwango cha watoto wanaojiunga na elimu ya sekondari kimeongezeka pia kutoka asilimia 14.6 mwaka 1995 hadi 59.5 mwaka 2013.Hali kadhalika, idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi imeongezeka kutoka 4,641 mwaka 2000/01 hadi 145,511 mwaka 2012/13. Aidha, elimu ya juu imepanuka ambapo vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki vimeongezeka kutoka chuo mwaka 1995 hadi 50 mwaka 2013 na kuwezesha idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya Shahada kuongezeka kutoka 16,727 mwaka 2000/01 hadi 162,510 mwaka 2012/13.

Utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo ulifanyika kupitia sheria, kanuni, miongozo pamoja na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu iliyoandaliwa mwaka 1997.

Serikali inaonyesha jinsi inavyotilia uzito suala zima la elimu katika ngazi zote, na juhudi inazofanya katika kutekeleza na kuboresha mipango yake, hivyo hata wazazi nao wanapaswa kuonyesha jinsi wanavyowajibika badala ya kuwa kikwazo.

Wanafunzi 701,038 sawa na asilimia 92.27 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2019 walichaguliwa kuendelea na kidato cha kwanza mwaka 2020.

Miongoni mwao 58,699 hawakupata nafasi kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, agizo litatolewa kutoka serikali kuu kuwa kila halmashauri ihakikisha ujenzi wa madarasa ufanyike mapema ili kuwawezesha vijana hao kuendelea na masomo.

# Mahakamani wakidaiwa kuchapisha picha za ngono

**Na Hellen Mwango**

WATU wawili akiwamo mfanyabiashara Samwel Tela na mpambaji wa video, Aisha Juma maarufu Kandi (19), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka mawili likiwamo la kuchapisha picha za ngono na kulawiti.

Kandi na Tela walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Kija Ruzingana, alidai shtaka la kwanza linamkabili Kandi akidaiwa Desemba 12, mwaka jana mahali tofauti jijini Dar es Salaam kuchapisha picha za ngono kwa picha.

Katika shtaka la pili linalomkabili Tela, anadaiwa mahali, tarehe na mwaka usiojulikana alimwingilia kinyume na maumbile Kandi mwenye umri wa miaka 19 wakati akijua ni kosa kisheria.

Washtakiwa hao walikana mashtaka na upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba hawana pingamizi la dhamana.

Wakili wa utetezi, Nyaronyo Kicheere alidai kosa linalomkabili mshtakiwa wa pili halihusiani na masuala ya uchumi, wala wizi, lakini jambo la kushangaza akaunti zake zimefungiwa.

Alidai mshtakiwa ni baba wa watoto na mke, ana wazazi wanaomtegemea hivyo aliomba akaunti zake zifunguliwe ili familia yake wapate kula kwa madai wamekuwa kama machokoraa mtaani.

Wakili Ruzingana aliuomba upande wa utetezi uwape muda wa kufuatilia akaunti hizo kwa sababu hajui kama zimefungiwa kwa mashtaka hayo au mengine kama yapo aliomba wapewe muda ili haki ya mshtakiwa ipatikane.

Hakimu Chaungu alimshauri wakili afuatilie suala hilo polisi kujua sababu za kufungiwa kwa akaunti hizo na alimtaka awape muda upande wa mashtaka ili tarehe ijayo waweze kueleza sababu za akaunti hizo kufungiwa.

Kuhusu dhamana, Hakimu Chaungu alimtaka kila mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaosaini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni 10, barua ya utambulisho na nakala ya kitambulisho chochote.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Afya katika kikao cha Utekelezaji wa Mpango Kazi kwa kipindi cha Julai-Disemba 2019/2020, Mjini Zanzibar, jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Waziri Zungu akoshwa maendeleo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, ameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa usimamizi aliouita makini katika kuwaletea maendeleo wananchi wa visiwa hivyo.

Zungu alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki alipofanya mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ, Balozi Seif Ali Iddi, alipomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha baada ya kuteuliwa hivi karibuni. Alibainisha kuwa pamoja na kuwapo kwa vikwazo hususani vya kimazingira, Zanzibar imepiga hatua kimaendeleo sambamba na kuongezeka kwa Pato la Taifa.

Kwa kutambua vikwazo hivyo vya kimazingira, Zungu aliahidi kuteua wataalamu maalum wa masuala ya mazingira kwa lengo la kuangalia athari za mazingira zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali visiwani humo.

Waziri huyo aliahidi kupanga ziara maalum ya kuangalia hali ya mazingira katika maeneo ya Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar inayoratibu na kusimamia mambo ya Muungano na mazingira kwa upande wa Zanzibar.

Katika mazungumzo yao hayo, Balozi Seif Ali Iddi alisema muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeinufaisha Zanzibar kwa kiwango kikubwa.

Alisema kuwa zipo fursa zinazowanufaisha wananchi wa Zanzibar ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akitolea mfano Wazanzibar wanaoishi Tanzania Bara na uwekezaji katika shughuli za kilimo na biashara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, alimwahidi Zungu kumpa ushirikiano na kumkaribisha wakati wote Zanzibar.

## RPC asikia kilio cha wanahabari

**Na Halima Ikunji, TABORA**

KAMANDA wa Polisi mkoani Tabora, Barnabas Mwakalukwa, ameahidi kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari kwa kutoa taarifa za matukio kwa wakati baada ya waandishi hao kumlalamikia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye ghafla fupi ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na jeshi hilo, alisema ahadi hiyo imefuatia kulalamikiwa na baadhi ya waandishi wa habari kuwa hatoi taarifa kwa muda muafaka na kubagua baadhi ya vyombo vilivyopo mkoani humo.

Mwakalukwa alisema kuanzia sasa milango iko wazi kwa ajili ya kutoa maelezo ya matukio na kesi zilizopo kwenye upelelezi ili waandishi wa habari wakamilishe taarifa zao.

Alisema hoja zilizoigusa Jeshi la Polisi ni kukimbia waandishi wa habari, kushindwa kutoa ushirikiano kwa baadhi ya vyombo na kuchelewesha kutoa taarifa kwa muda mwafaka.

Alisema Jeshi la Polisi linategemea taarifa kutoka kwa wanahabari na wananchi na kufanikisha kuwakamata wahalifu.

"Nawaonya wanahabari katika kipindi cha kuelekea uchaguzi wa udiwani, ubunge na kiti cha Rais jihadharini na kuegemea upande wowote tekelezeni majukumu yenu na kuzingatia maadili ya kazi zenu," alisema.

Aliwataka katika kipindi hicho kuwa makini na ili watambulike sehemu yoyote lazima wawe na vitambulisho vya kazi vinginevyo hawataruhusiwa kuingia katika ofisi ya jeshi hilo.

Kwa upande wake Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani hapa, Mussa Chaulo, amewaonya wanahabari wote kutojihusisha na kuomba na kupokea rushwa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi.

Chaulo alisema atasikitika kuona au kusikia mwanahabari amekiuka utaratibu huo na kutozingatia maadili ya kazi yake kwa kufuata tamaa ambayo itampeleka pabaya.

Naye Mwakilishi wa wanahabari mkoani Tabora, Robert Kakwesi, alimshukuru Kamanda wa Jeshi la Polisi kuandaa ghafla hiyo ambayo itawasaidia kutambua miiko na mipaka ya kazi zao.

Na mwandishi wa habari mkongwe, Titus Philipo alimwahidi kamanda huyo kwamba atajitahidi kuwakumbusha wanahabari kuzingatia maadili ya kazi na kila mwanahabari ahakikishe anavaa kitambulisho chake ili iwe rahisi kutambulika popote.

# Mkandarasi atii agizo la JPM barabara Dar

Na Mwandishi Wetu

MKANDARASI anayejenga barabara yenye urefu wa kilomita 1.2 kutoka Daraja la Nyerere hadi Feri-Kibada wilayani Kigamboni mkoani Dar es Salaam, ametii agizo la Rais John Magufuli la kumtaka kuanza kazi ya kukamilisha mradi huo haraka.

Kampuni ya ukandarasi ya China Railway Construction Engineering Group (CRCEG), jana ilianza kazi ya kutengeneza kipande cha barabara hiyo, zikiwa ni siku chache baada ya Rais Magufuli kutoa agizo la kumaliza mgogoro wa kikandarasi na kukamilisha mradi huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ofisi za Wilaya ya Kigamboni wiki iliyopita, Rais Magufuli alieleza kutoridhishwa kwake na ucheleweshaji wa mradi huo kutokana na suala la gharama.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari jana, CRCEG ilisema: "Tunataka kutoa shukrani zetu za dhati na kuunga mkono ari ya 'Hapa Kazi Tu' na utii wa sheria unaotiliwa mkazo na Rais Magufuli, kukamilisha mradi huu kwa kiwango cha daraja la juu na gharama nafuu bila kuchelewa."

Mkandarasi huyo ameeleza kuwa mradi ulichelewa, pamoja na mambo mengine, kutokana na kuchelewa kukabidhiwa eneo la mradi kutokana na nyumba zilizopo, makaburi na majengo mengine yaliyokuwapo ndani ya eneo la barabara, na kuwa malipo ya fidia yalikamilika mwishoni mwa Mei, 2018.

Ilieleza kuwa mwajiri (NSSF) kumteua meneja mpya wa mradi ni sababu nyingine ya kuchelewa kuanza kazi hiyo.

Kwa mujibu wa mkandarasi huyo, wakati ambapo meneja wa awali walisimamisha uangalizi wa kazi hiyo Mei 1, 2019, meneja mpya aliteuliwa wiki iliyopita.

"Ni Februari 14 tu ndipo mwajiri alimjulisha mkandarasi kuhusu kuletewa kutoka Tanroads kama meneja mpya wa mradi ambaye anaanza kazi Februari 17 (jana)," ilisema taarifa ya CRCEG.

Sababu nyingine za kuchelewa kwa mradi huo, kwa mujibu wa mkandarasi, ni kuchelewa kwa malipo kwa muda mrefu na kusababisha kukwama kwa mtiririko wa fedha kwa mkandarasi, pamoja na kuchelewa kwa idhini ya kuhamisha wananchi katika makazi mapya na utunzani wa miundombinu iliyokuwapo katika eneo la mradi, kama vile bomba la mafuta la TAZAMA, bomba la mafuta la MOIL na bomba la kusambaza maji la TIPER.

Ucheleweshaji wa gharama za kuhamisha nyaya za umeme za Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) ilitajwa kama sababu nyingine ya kuchelewa kwa mradi huo.

Wakati huo huo, CRCEG imeeleza kuwa sababu ya kuongezeka kwa gharama za mradi ni pamoja na barabara hiyo inajengwa kwa kiwango ubora wa hali ya juu, ikiwa ni kiwango cha barabara za haraka (express) ambacho ni kiwango cha juu zaidi nchini.

Mkandarasi huyo alieleza kuwa gharama pia ilikuwa juu kwa kuwa maeneo kadhaa yaliathiriwa na mabaki ya mafuta, hivyo kulazimika kufanyika kwa uchimbuaji wa kwenda chini kujazia udongo ulioathiriwa na mafuta.

CRCEG imeeleza pia kuwa barabara inapita katika maeneo yenye topetope yanayohitaji uchimbuaji kuondoa udongo na kujaza kama njia ya kuimarisha ufanisi wa kimakanika.

Kulikuwa pia na gharama za ziada za kuhamisha makazi ya watu na utunzaji wa miundombinu kwa huduma ambazo zilikuwa ndani ya eneo la mradi, ambavyo vyote vinaidhinishwa na mwajiri.

Mkandarasi pia alimlaumu mwajiri kwa kuchelewesha malipo, hivyo kusababisha kuongezeka kwa riba bila sababu.

Mradi huo ulisimamishwa Desemba 31, 2018 kufuatia maelekezo yaliyotolewa na meneja mradi, wakati ukisubirishwa utatuzi wa masuala mbalimbali, ikiwamo uidhinishaji wa vitu vya ziada na mwajiri, ambao haujafanyika.



Wananchi wakiangalia bajaji, iliyopata ajali baada ya kuacha njia na kuingia kwenye mtaro katika eneo la Ubungo Maji, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wauza pembejeo kilimo watuhumiwa hujuma

Na Nebart Msokwa, MBEYA

BAADHI ya wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo mkoani Mbeya, wanadaiwa kuwa wanafungua mbegu za mazao zilizofungashwa na kampuni ya uzalishaji wa mbegu hizo, na kuuza kidogo kidogo kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Mfawidhi wa Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu nchini (Tosci), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Nasari, wakati wa mafunzo kwa wazalishaji na wasambazaji wa mbegu wa Mkoa wa Mbeya.

Nasari alisema kitendo hicho ni kosa kwa mujibu wa sheria, na kwamba kinahesabika kuwa ni uchakachuaji wa mbegu.

Alisema tatizo hilo limebainika kuwa kubwa zaidi katika Wilaya ya Kyela ambako wakulima wengi wanahitaji kiwango kidogo cha mbegu kuliko uwezo wao, hivyo wanawalazimisha wafanyabiashara kuwauzia kiasi kidogo kidogo.

"Kampuni nyingi zinazalisha mbegu na kuzifungasha kwenye mifuko ya kilo mbilimbili, lakini wauzaji wanapunguza na kuweka kwenye viwango vidogo na kuuza kwa bei ndogo," alisema Nasari.

Alisema kutokana na hali hiyo, ndio maana waliamua kutoa mafunzo hayo kwa wazalishaji na wasambazaji wa mbegu za mazao katika mkoa huo.

Naye Mtafiti wa mahindi kutoka Taasisi ya Utafiti wa kilimo nchini (Tari), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Leonard Sabula, alisema mbali na wafanyabiashara kuchakachua mbegu hizo, pia wengine wanauza mbegu bila vibali.

Alisema wengi wa wafanyabiashara hao wanasingizia gharama kubwa za kupata kibali kutoka Tosci, na kwamba hao ndio wanaoongoza kwa kuchakachua mbegu hizo.

# Makonda ajichongea kwa JPM

INATOKA UK 2

huko alikokuwa anaeleza, inawezekana nimemsikia vibaya, na yeye hahusiki kwenye kaya maskini, mkae mziangalie hizo fedha, lazima zirudishe," aliagiza.

Rais Magufuli alisema uhakiki ulibaini kaya 18,211 zilikuwa na wanayaka ambao ama mmoja alikuwa amefariki dunia au wote.

"Uhakiki ulibaini kaya 18,700 hazikujitokeza mara mbili kupokea ruzuku, kaya 9,903 zilizohamia vijiji au mitaa au shehia ambapo mpango haujaanza na kaya 5,134 ambazo wanakaya wake walikuwa wajumbe wa kamati za usimamizi wa jamii; halmashauri za vijiji au mitaa na pia viongozi na watendaji," alisema.

Kiongozi huyo wa nchi alisema maeneo yaliyoathiriwa zaidi kwa kuwa na kaya hewa na idadi kwenye mabano ni Songea Manispaa (2,991), Chamwino (1840), Kinondoni (1,538), Ilala (1,476), Moshi Manispaa (1,071), Arusha Mjini (851), Temeke (2,012), Dodoma Mjini (1,334), Buhigwe (862) na Morogoro (954).

Rais Magufuli alizitaja halmashauri 10 zilizojitahidi kudhibiti vitendo hivyo na kuwa na idadi ndogo ya kaya hewa kuwa ni Pangani (149), Kilolo (211), Unguja (242), Igunga (76), Mtwara Manispaa (25), Rorya (207), Mkinga (140), Babati Mji (45), Geita Mjini na Chunya (104).

Aliwataka watendaji wa mfuko huo kuhakikisha wanaimarisha usimamizi wa fedha kwa kuhakikisha hakutokei tena kaya hewa.

"Serikali haitakuwa na huruma na mtu yeyote atakayejaribu kutaka kujinufaisha kupitia mradi huu. Ninawashukuru washirika wetu ambao tumeshirikiana kwenye awamu zilizopita, kushirikiana kwenu kumesaidia katika kutekeleza hizi awamu na hii tunayoizindua," alisifu.

Rais Magufuli alitambua mchango wa marais wastaafu, kila mmoja katika kipindi chake na kuwaeleza kuwa ana deni la kutimiza katika utawala wake ili kuhakikisha umaskini unapungua zaidi.

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akisoma hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema wameona mabadiliko makubwa visiwani humo kupitia Tasaf.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, aliwataka wananchi kuelewa kuwa fedha za wafadhili zilizotolewa kwenye mfuko huo, zinatakiwa kurejeshwa, hivyo siyo za kugawana.

Mwakilishi kutoka Benki ya Dunia, Preet Arora, alipongeza utekelezaji wa mpango huo na kueleza kuwa ni moja ya miradi ya mfano duniani katika kupunguza umaskini.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na marais wastaafu, Ali Hassan Mwinyi, Mkapa na Dk. Jakaya Kikwete.

# Citi, TAMF zazindua tuzo wajasiriamali

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya wakfu ya Citi kwa kushirikiana na shirikisho la asasi zinazotoa huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo (TAMFI), wamezindua shindano la kuwania tuzo ya wakfu wa Citi kwa wajasiriamali wadogo (CMA).

Tuzo hizo zimelenga kuangalia mchango kwa wajasiriamali wadogo katika kuimarisha uchumi wao binafsi, katika ngazi ya familia na kijamii nchini.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Citibank Tanzania, Geofrey Mchangila, alisema tuzo hizo zitasaidia kuchagiza mafanikio kwa baadhi ya wajasiriamali wabunifu.

"Tuzo hizo ni sehemu ya ahadi ya Citibank katika kuhakikisha kwamba taasisi ndogo za kifedha zinawasaidia wajasiriamali wabunifu ambao watakuwa wafanyabiashara wakubwa wa baadaye," alisema Mchangila.

Alisema kuanzia mwaka 2005 tuzo za CMA zimejikita zaidi katika kuamsha fursa za kukua kwa ujasiriamali mdogo katika nchi takribani 30.

"Zaidi ya Sh. milioni 70 zitatuzwa kwa washindi 16 na fedha hizo zitaenda sambamba na kuhimiza mchango wa taasisi ndogo za kifedha na wajasiriamali wadogo nchini," alisema Mchangila.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na wakfu wa Citi ni kuchangia katika kusukuma mbele lengo namba nane la malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa.

"Tuzo hizo zinaboresha ujumuishaji wa fedha na kuzalisha utambulisho kwa wajasiriamali waliofanya ya ziada katika kuhakikisha kwamba wanajiwezesha kiuchumi wao na familia zao na kuchangia uchumi wa jamii zao na uchumi wa Taifa," alisema Mchangila.

Naye Mtendaji Mkuu wa TAMFI, Winnie Terry, alisema tuzo hizo ni chachu katika kuonyesha jamii kwamba ukopaji wa fedha na ulipaji wenye nidhamu ni ufunguo katika maendeleo yao.

Alisema tuzo hizo zitashindaniwa katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia jinsia, uchumi na idadi ya raslimali watu na kwamba biashara itakayoshindanishwa ni yenye na matokeo chanya kwa mjasiriamali, familia yake na jamii kwa ujumla.

Alisema katika tuzo hizo kutakuwa na mshindi wa jumla wa tuzo ya mjasiriamali wa mwaka na pia kutakuwa na tuzo ya taasisi ya fedha bunifu.

**"Zaidi ya Sh. milioni 70 zitatuzwa kwa washindi 16 na fedha hizo zitaenda sambamba na kuhimiza mchango wa taasisi ndogo za kifedha na wajasiriamali wadogo nchini," alisema Mchangila.**

# Elimu maadili yatakiwa viongozi mabaraza ardhi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa Umma kanda ya magharibi (TABORA) kutoa mafunzo ya maadili kwa viongozi wa mabaraza ya usuluhishi ya ardhi kwa ngazi ya kata.

Ombi hilo lilitolewa jana wakati wa mafunzo ya uzingatiaji wa maadili kwa viongozi wa umma namna bora ya kujiepusha na migogoro ya kimaslahi yaliyotolewa na Ofisa ya Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa Umaa Kanda ya Magaharibi kwa madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo.

Sharifu Samuel, Diwani wa Kinamapula, alisema viongozi wa mabaraza ya usuluhishi ya ardhi ngazi ya kata hawana elimu ya maadili na kujikuta wamejiingiza katika migongano ya kimaslahi wanapotoa maamuzi ya mashauri wanayosimamia kwa wananchi.

Pia alisema elimu hiyo itawasaidia kuwawezesha kutambua wajibu wao na kujiepusha kuomba na kupokea rushwa wanapotoa huduma kwa wananchi.

"Mabaraza mengi ya ardhi yamekuwa yakilalamikiwa kwa kutoa upendeleo wanapotoa maamuzi na kusababisha wananchi kukosa imani nayo na wanyonge kukosa haki zao, nahii ni kwa sababu ya kukosa elimu ya maadili na kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa," alisema Samuel.

Estar Matone, Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Bulungwa, alisema elimu ya maadili ni muhimu kutolewa kwa ngazi zote hususan wanafunzi kuanzia ngazi ya awali hadi chuo kikuu ili kujenga Taifa la watu waaminifu wasiotanguliza maslahi yao wanapokabidhiwa mamlaka serikalini.

Kaimu Mkuu wa Kanda, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Gerald Mwaitebele, alisema wameanzisha klabu za maadili katika shule za msingi na sekondari ambazo zina jukumu la kuwafundisha wanafunzi kuhusiana na maadili.

Awali akifungua mafunzo hayo Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Kimisha, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliwataka viongozi na madiwani kuzingatia maadili ili kuepuka kujiingiza katika migongano wakati wa usimamizi wa miradi ya maendeleo.




Mafundi wakipima barabara za mitaa katika eneo la Lumumba jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa lami. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kairuki azindua mwongozo wa uwekezaji mkoani Songwe

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki amezindua kitabu cha mwongozo wa uwekezaji katika Mkoa wa Songwe na kuwahamasisha wawekezaji kuchangamkia fursa lukuki zilizopo mkoani humo.

Akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika uzinduzi wa kitabu cha mwongozo na Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Songwe jana, Kairuki alisema washiriki watapata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali zinazokwamisha maendeleo ya uwekezaji na biashara.

"Uzinduzi wa kitabu hiki unaonyesha dhamira ya kweli na utayari wa Mkoa wa Songwe kuvutia wawekezaji katika mkoa huu. Bado ninatoa rai kwa mikoa ambayo bado haijakamilisha mwongozo wa uwekezaji kufanya hivyo," alisema.

Waziri Kairuki alisema Waziri Mkuu Majaliwa mbali ya kuwapongeza Wanasongwe wote kwa hatua waliyofikia, amesema majumuisho na taarifa ya kongamano hilo ameagiza apelekewe kwa ufuatiliaji zaidi.

"Mkoa wa Songwe una fursa nyingi sana za kiuwekezaji na hasa eneo la kilimo pamoja na kuwapo fursa nyingine kama madini, ufugaji, utalii.

Mna mtaji mkubwa wa watu na hivyo hamna budi mkazitumia fursa hizo kubadilisha maisha," alisema.

Kairuki aliipongeza Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) kwa kufanya kazi bega kwa bega na uongozi wa Mkoa wa Songwe kuhakikisha kuwa fursa za kibiashara na uwekezaji zinatangazwa na pia kongamano la uwekezaji linaleta mafanikio yaliyokusudiwa.

"Nitakuwa mstari wa mbele kutangaza fursa zilizopo katika mkoa huu na pia naomba msichoke kujifunza kutoka katika mikoa mingine. Jitahidini pia kuwekeza katika miundombinu muhimu ili kuvutia wawekezaji zaidi," alisema.

Alisema tangu alipowasili mkoani Songwe hajasikia malalamiko yoyote kutoka kwa wawekezaji wala wananchi na hivyo akauomba uongozi wa mkoa kuendelea kufanya kazi karibu na wawekezaji ilikuongeza mapato na makusanyo ya serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliipongeza serikali ya Rais John Magufuli kwa kufanikiwa kubadilisha fikra miongoni mwa watumishi wa umma.

"Naomba niwe mkweli Mheshimiwa Rais Magufuli amebadilisha kabisa fikra za watendaji na watumishi wa umma dhidi za dhana ya uwekezaji na biashara. Waziri Kairuki amekuwa msaada mkubwa sana katika eneo la uwekezaji na biashara," alisema.

# Jela miaka 30 kwa kubaka mtoto

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemuhukumu mkazi wa Kijiji cha Mmangawanga, Kata ya Kiwalala, Issa Mussa Tambue (62), kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya kubaka mtoto.

Tambue mwenye umri wa miaka 10, jina limehifadhiwa.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu mkazi mfawidhi wa Mahakama hiyo, Maria Batulaine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Batulaine alimuuliza mshtakiwa iwapo anayo sababu itakayoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kosa linalomkabili mbele yake, hata hivyo hakuweza kutoa neno la kujitetea zaidi ya kung'ang'ania kumkana mtoto huyo.

Baada ya maelezo hayo, Batulaine alimuuliza mwendesha mashtaka wa serikali, Yahaya Gumbo, kama anakumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana lakini aliiomba Mahakama impatie adhabu kali ili iwe fundisho kwa mshtakiwa na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

"Sina kumbukumbu ya makosa ya zamani, lakini naomba Mahakama yako tukufu kuona adhabu itakayomfaa na fundisho kwa wengine walio na tabia hiyo," alisema Gumbo.

Hakimu mkazi Batulaine akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 85/2019, chini ya vifungu 130 kifungu kidogo (1) na cha 2 (e) na 131 kifungu kidogo cha (1) alimuhukumu kifungo cha miaka (30) gerezani na atakapomaliza adhabu amlipie mlalamikaji fidia ya jumla ya 2,000,000/-

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo, kuwa kati ya mwezi Juni na Julai 2019, mshtakiwa amekuwa na tabia ya kushiriki mapenzi na mtoto huyo hadi alipokamatwa na wazazi na kaka wa mtoto huyo akiwa chumbani mwa nyumba ya mshtakiwa.

## Wateja Exim wakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu**

Benki ya Exim Tanzania imezindua kampeni ya uhamasishaji ikilenga kuwashawishi zaidi wateja wa benki hiyo kutumia kadi za MasterCard ambapo pamoja na mambo mengine itatoa zawadi mbalimbali kwa wateja hao.

Uzinduzi wa kampeni hiyo mpya iliyopewa jina la 'Chanja Kijanja na Exim Mastercard' unalenga kutoa fursa ya kipekee kwa wateja wa benki hiyo kufurahia huduma zinazokwenda sambamba na mfumo wa maisha yao kupitia benki hiyo.

Kwa mujibu wa mkuu wa kitengo cha wateja wadogo na kati wa Benki ya Exim Tanzania, Andrew Lyimo, kampeni hiyo inalenga kuhamasisha wateja wa benki ya Exim kutumia kadi za benki hiyo katika manunuzi ya mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS) katika maduka mbalimbali na maeneo mengine nchini.

"Kwa upande wetu Benki ya Exim, wateja wanaotumia kadi zetu wamekuwa wakifurahia urahisi wanapofanya manunuzi au malipo kwenye ya mahitaji muhimu kwenye maduka, ununuzi wa bidhaa kimataifa kupitia mtandaoni, malipo wakati wa safari, malipo ya hoteli na shughuli za kitalii," alisema.

"Na kwa sasa, si tu kwamba wateja wetu wanafurahia urahisi mkubwa unaotokana na matumizi ya kadi za benki ya Exim, bali pia wanapata fursa ya kushinda zawadi nzuri kupitia kampeni hii. Kutakuwa na zawadi za kila wiki, kila mwezi na kubwa za mwisho wa kampeni. Wanachotakiwa wateja wetu ni kufanya miamala yao kupitia kadi ya Exim Bank MasterCard mara nyingi iwezekanavyo kwa kuwa kila muamala unaongeza nafasi moja ya kushinda," aliongeza.

Lyimo alisema washindi pamoja na wenza wao watatunukiwa zawadi ya kusafiri wakiwa wamegharamiwa gharama zote ikiwamo Visa, tiketi ya ndege pamoja na pesa za matumizi.

"Mshindi wa kwanza ataenda Dubai, mshindi wa pili ataenda Cape Town, Afrika Kusini na wa tatu ataenda visiwa vya Zanzibar," alisema.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), Godfrey Nyaisa (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Haki Miliki Afrika (ARIPO), Fernando Dos Santos, wakibadilishana hati baada ya kusaini makubaliano ya ubia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Madalali wa almasi waelekezwa masoko

**Na Mohab Dominick, SHINYANGA**

ZAIDI ya madalali 50 wa madini ya almasi mkoani Shinyanga, wametakiwa kutumia masoko kuendesha biashara zao za madini ya almasi kuliko kukwepa na kufanyia nje ya masoko yaliyoanzishwa na serikali.

Wameelezwa kuwa jambo hilo litawaingiza hatarini na kukumbana na mkono wa sheria.

Imebainishwa kuwa soko la almasi la Maganzo katika Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga limekamilika na madalali 20 kati ya 50 kutoka Maganzo na Shinyanga ndiyo wameitikia wito na kuchukua vyumba kwenye soko hilo.

Hayo yalielezwa na Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, aliyasema hayo hivi karibuni alipofanya kikao na wafanyabiashara na madalali wa madini ya almasi wa Maganzo na Shinyanga kilichohudhuriwa na viongozi wa Taasisi za Serikali katika Halmashauri ya Kishapu, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo wakiwamo viongozi wa chama cha wachimbaji wadogo mkoani Shinyanga (Shirema).

Akizungumza jana na Nipashe, Kumburu alisema kuwa kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili kwenye biashara ya madini ya almasi.

Alisema wafanyabiashara watakaoshindwa kutekeleza maelekezo hayo hawatapewa nafasi ya kununua asilimia tano kwa kuwa watakuwa wanafanya nje ya soko kinyume cha kifungu cha 6 cha Kanuni za masoko ya mwaka 2019.

"Kituo cha kununulia Almasi kilichoandaliwa kitakuwa na vifaa vyote vya kupima na kutambua madini ya almasi. Hata hivyo, madalali wataruhusiwa kwenda na vifaa vyao vya utambuzi kama wataona inafaa. Pia kituo hicho kitakuwa na ulinzi wa askari na kamera kwenye maeneo yote, hivyo nawatahadharisha madalali kuwa makini na aina yoyote ya wizi au kutaka kurubuni biashara hiyo wakiwa ndani ya soko," alisema Kumburu .

Alisema kuwa, utaratibu utakaotumika katika kuuza almasi ya Mwadui ya asilimia 5 utakuwa wa mnada ambapo madalali watapewa fursa ya kwenda kuyakaona na kujiridhisha aina, kiwango na ubora kwa saa moja na baadaye watatakiwa kuweka ahadi na ofa hizo zitafunguliwa baada ya wote kukamilika kwa ajili ya kutangaza washindi.

Aidha, aliwataka madalali wote kujisajili kwenye kituo cha maganzo na baadaye majina yao yatawasilishwa mgodini ili kuruhusiwa kuingia wao pamoja na watu watakaokuwa nao.

## Kijiji chafagiliwa matumizi ya fedha

**Na Allan Isack, BABATI**

WANANCHI wa Wilaya ya Babati, wametakiwa kuiga mfano kwa wakazi wa Kijiji cha Vilima Vitatu waliowekeza Sh. milioni 105, zilizotokana na mapato ya hifadhi ya misitu ya ndani ya kijiji hicho.

Ukusanyasi wa fedha hizo, umesaidia kijiji hicho kufanikiwa kujenga zahanati ya kisasa.

Licha ya ujenzi wa zahanati hiyo, pia wanakijiji wa eneo hilo wamefanikiwa kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita, ili kupunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kutafuta elimu.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea zahanati hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahati, Hamisi Malinga, alisema serikali ya kijiji hicho inahitaji pongezi kutokana na matumizi mazuri ya fedha za mapato ya hifadhi.

Alisema kijiji hicho kilitoa wazo la ujenzi wa zahanati hiyo kwa serikali na walipoona wazo hilo, walilifanyia kazi kwa kuwaunga mkono hadi kukamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo.

Malinga aliwataka wananchi kujijengea tabia ya kutunza fedha wanazopata katika miradi mbalimbali, ili kusaidia jitihada za serikali katika uwekezaji kwenye sekta za afya na elimu.

"Naomba niwapongeze kijiji hiki kwa jitihada mlizofanya kwenye maendeleo, ni vema wengine wakaiga mfano kutoka kwenu," alisema Malinga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Vilima Vitatu, Aboubakary Msuya, alisema eneo la hifadhi lina ukubwa wa hekta 12,800 na mapato ya hifadhi hiyo hupatikani kupitia watalii wanaokwenda kutalii, na kulala katika hoteli za kitalii.

Alisema awali walianza kupata mgao wa Sh. milioni 20 na baadaye ziliongezeka hadi kufikia Sh. milioni 40 na sasa mapato yameongezeka mpaka Sh. milioni 105.

Aidha, alisema baada ya kukusanya kiasi hicho cha fedha, walianza ujenzi wa zahanati hiyo, ambayo inahudumia wananchi takribani 4,000 walioishi kijijini hapo.

"Eneo la hifadhi tunalitunza vizuri linalindwa kwa kutumia askari ili watu wasivamie na kuharibu misitu iliyopo ndani ya hifadhi," alisema Msuya.

Hata hivyo, alisema Serikali ya Kijiji imetoa kipaumbele katika ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho, ili kutatua tatizo la wakazi wake, kwenda nje ya kijiji kutafuta huduma za afya.

"Serikali ya kijiji iliamua kujenga zahanati na shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita, kwa lengo la kutatua kero kwa wananchi wa eneo hili," alisema Msuya.

"Wananchi wa vijiji vingine wanapaswa kuiga mfano wa kijiji chetu ambacho tumeamua kujenga zahanati na shule kutokana na mapato tunayopata kupitia hifadhi ya misitu iliopo ndani ya kijiji hiki," alisema.

# Wananchi waunga mkono ujenzi kituo cha yatima

**Na Allan Isack, ARUMERU**

WAUMINI wa Kiislamu katika kijiji cha Karangai Kata ya Kikwe wilayani Arumeru mkoani hapa, wameunga mkono mpango mkakati wa kujenga kituo cha kulea watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Wakizungumza kwa niaba ya wananchi wa kijiji hicho, Zaituni Masanja na Fatuma Mohamed, walisema wamefarijika kusikia kuna mpango wa kujenga kituo cha kulea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Walisema ujenzi wa kituo hicho, utasaidia kuwalea kwa pamoja watoto wote ambao wamepoteza wazazi wao, sambamba na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

"Tunafuraha kubwa kusikia kituo hiki kinajengwa katika kijiji chetu kwa sababu kitalelea watoto wa dini zote na kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha," alisema Fatuma.

Hata hivyo, wamewaomba wananchi wa kijiji hicho, kujitoa kwa hali na mali kufanikisha ujenzi wa kituo hicho kukamilika kwa wakati.

"Tunaomba wananchi wa Karangai tushikamane na tusaidiane katika jambo hili ili likamilike kama tulivyopanga," alisema Fatuma.

Msemaji wa Taasisi ya Kiislamu ya (Twariqatul), Sheikh Haruna Hussein, alisema harambee ya ujenzi wa kituo hicho itafanyika Februari 22, mwaka huu na itaongozwa na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa.

Alisema hadi sasa taasisi hiyo imeanzisha matawi 5,662 hapa nchini na nje ya nchi.

Alisema taasisi hiyo pia imejenga vituo vya kulelea watoto yatima 851.

"Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowasa, atakuwa mgeni rasmi katika harambee yetu na ataweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hiki na mkewe atakuwa mlezi wa kituo chetu," alisema Haruna.

Aidha, alisema eneo la ujenzi wa kituo hicho, linaukubwa wa ekari moja na ujenzi utagharimu Sh. milioni 150. Alisema kituo hicho, kitakuwa na uwezo wa kuchukuwa watoto 50 hadi 60.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Taifa ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Dk. Edmund Mndolwa (kushoto), akishirikiana na Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Mkoa wa Arusha, Herzon Mbise (kulia), kupandisha moja ya mizinga ya nyuki ambayo imetokana na mradi wa jumuiya katika Kijiji cha Lorei, Kitongoji cha Mlimani, Kata cha Lorei, katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru jana. Jumla ya mizinga 100 imetolewa na jumuiya hiyo kwa ajili ya wilaya zote za mkoani humo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mradi wa bil. 2/- kukabili uhaba wa maji

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

MRADI wa maji wa Sh. bilioni mbili unatarajiwa kujengwa na serikali katika Kata ya Sigino Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara.

Mradi huo, umemwibua Diwani wa Kata hiyo, Manfred Sumaye, kudai kwamba mradi huo utamwagazia nuru ya kisiasa kwenye kata hiyo, kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba, mwaka huu.

Hayo aliyasema Mjini Babati, wakati akizungumza na Nipashe, kuhusu ujenzi wa mradi huo ambao timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Maji imeshafika na kuangalia chanzo kikuu cha maji.

Sumaye alisema mradi huo ukikamilika, wananchi 10,000 watanufaika kwa kupata huduma ya uhakika ya maji.

"Katika kata yetu tuna shida kubwa ya maji na maji tunayotumia kwa kunywa na kupikia tunachota kwenye korongo, lakini ukitaka kununua majisafi na salama tunauziwa ndoo kwa Sh. 500 yenye ujazo wa lita 20," alisema Sumaye.

Alisema maji hayo wanayotumia wananchi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pia yanatumiwa na wanyama wakufugwa na wale wa porini.

Awali diwani huyo alisema tangu alipojiunga na CCM ameona kuna nuru kwa kuwa kila alichokiomba serikali imetekeleza.

"Wakati mwingine natafutwa na viongozi wa wilaya au mkoa wananiambia kuwa kuna vitu wanakuja kufanya katika kata yangu, lakini nilipokuwa upinzani nilikuwa naenda hadi kwa Mkuu wa Wilaya na ilikuwa vigumu kusaidiwa," alisema.

Alitumia fursa hiyo kuwaomba wataalamu wa ujenzi wa mradi huo, kujenga kwa haraka ili ukamilike kwa wakati kulingana na mkataba unavyoelekeza wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (Bawasa).

Mkazi wa eneo hilo, Lilian Duday, alisema serikali ikikamilisha ujenzi wa mradi huo, wananchi wa eneo hilo hawatawasahau kwa kumaliza kero ya maji kwa wananchi.





# Serikali yaombwa walimu zaidi Same

Na Asraji Mvungi, SAME

SERIKALI imeombwa kutatua tatizo sugu la uhaba wa walimu na watendaji wa kata na vijiji linaloitesa Wilaya ya Same kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, huku idadi kubwa ya wananchi wakilalamikia kukosa huduma yao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Rogert Ngula, alisema wameshalifikisha suala hilo kwenye ngazi husika na taratibu za kupatiwa watumishi hao zinaendelea.

Mpaka kufikia sasa, wilaya hiyo inakabiliwa na upungufu wa watendaji 29 wa kata na vijiji.

"Ni kweli tuna hilo tatizo la uhaba wa watumishi hasa kada ya watendaji wa kata na walimu ambao ndio wanaohitajika zaidi kutokana na pengo lililopo baada ya wenzao kustaafu. Kimsingi tumeshalifikisha jambo hilo utumishi na linashughulikiwa na wizara husika," alisema Ngula.

Kabla ya serikali kutoa majibu hayo, awali wananchi wa wilaya hiyo akiwamo Zehania John alisema uhaba wa watumishi hao, licha ya kukwamisha shughuli za maendeleo, pia linaathiri utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

"Kuna mambo mengi hayaendi kutokana na tatizo hilo kuna huduma nyingi hazisimamiwi kutokana na tatizo hilo tunaiomba serikali imalize changamoto hii kwani tunaamini ndani ya uwezo," alisema John, mkazi wa Same.

Malalamiko kuhusu tatizo hilo pia yalitolewa na madiwani wa halmashauri hiyo, wakati wa kikao chao cha bajeti ambacho pamoja na mambo mengine mjadala wa uhaba wa watumishi ulitawala.

Wakizungumzia changamoto hiyo, baadhi ya madiwani akiwamo Eliudi Mashamba wa Kata ya Kisiwani, alisema kata yake ni miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na tatizo hilo na kwamba nafasi ya mtendaji wa kata inakaimiwa na Ofisa Mifugo ambaye amekaimishwa nafasi nyingine.

"Kwa kweli kuna tatizo kubwa maana mtu mmoja anakaimishwa nafasi za watu watatu, sasa hapo kweli tunategemea kuwa kuna kitu kitakachofanyika kionyeshe matokeo mazuri," alisemai Eliudi.

Alipotafutwa pia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Christopher Irira, alikiri kuwapo kwa mahitaji hayo ya watumishi, huku akieleza kuwa tatizo hilo liko nje ya uwezo wao.

"Ni sahihi kabisa kuna maeneo mengi watendaji wamekaimishwa na unakuta kazi ya watu watatu ama wanne inafanywa na mtu mmoja kwa kweli kuna tatizo la msingi na tunaendelea kulishughulikia kulingana na taratibu zilizopo na kwa ngazi zinazohusika," alisema Irira.

# Shinikizo la damu sasa tishio Siha

Na Anjela Mhando, SIHA

SHINIKIZO la damu limetajwa kuwa kwa sasa ni tishio jipya kwa wakazi wa Wilaya ya Siha, kati ya magonjwa 10 ambayo yamekuwa yakiwasumbua wananchi wa eneo hilo.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Andrew Method, alisema rekodi za afya wilayani humo zinaonyesha kuwa shinikizo la juu la damu, sukari na magonjwa ya macho ndio tatizo kuu linalowasumbua wakazi wa Siha kwa miaka mitano iliyopita.

Alikuwa akizungumza na Nipashe, baada ya kumalizika kwa kambi maalum ya uchunguzi na matibabu ya macho iliyoendeshwa katika Hospitali ya Wilaya hiyo kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali. "Rekodi zetu zinaonyesha kwamba shinikizo la damu, sukari na magonjwa ya macho ni miongoni mwa magonjwa kati ya 10 yanayosumbua Siha kwa kipindi ha miaka mitano sasa," alisema Dk. Method.

Alisema kwa hospitali hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujilinda ili kuepuka kupata magonjwa hayo, kwa kuwa magonjwa hayo yanaweza kuzuilika endapo wananchi watapata elimu.

Kutokana na hali hiyo, amewashauri wakazi wa wilaya hiyo kuzingatia mazoezi ili kuwa na miili yenye ubora na kushindwa kupata magonjwa ya mara kwa mara.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, akizungumzia umuhimu wa kambi hiyo alisema, kambi hiyo imesaidia kupunguza matatizo ya wananchi kupata huduma za afya.

Buswelu alisema kutokana na ushirikiano unaoonyeshwa na wadau wa maendeleo, serikali imeongeza bajeti ya ununuzi wa dawa kutoka Sh. milioni 52 hadi kufikia Sh. milioni 252.

Awali, mmoja wa wafadhili wa kambi hiyo ya matibabu ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Kilimo cha Parachichi ya Africado, James Person, alisema zaidi ya Sh. milioni 20 zimetumika kugharamia matibabu hayo.




Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Baraza la Madiwani la Manispaa ya Moshi wakiongozwa na Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya (kushoto) na Diwani wa Kata ya Bomambuzi, Juma Raibu (wa pili kulia), wakikagua baadhi ya miradi ya maendeleo katika manispaa hiyo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Ujerumani kujenga kiwanda cha uchakataji wa taka Moshi

Na Mary Mosha, MOSHI

SERIKALI ya Ujerumani kupitia Jiji la Tumbigen, imesema itawekeza nchini kwa asilimia 80 katika mradi mkubwa wa ubunifu wa uchakataji wa taka katika Manispaa ya Moshi, kuanzia Aprili mwaka huu.

Tumbigen ambao sasa unakuwa mji dada wa Manispaa ya Moshi kutokana na ushirikiano wa kiuchumi waliouanzisha, umepanga kutekeleza mradi huo kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.8.

Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, alisema mradi huo utaongeza uwezo wa halmashauri hiyo kuzoa taka kutoka tani 168 kwa siku hadi kufikia tani 230.

Alisema kiwanda hicho cha kuchakata takataka, pia kitakuwa na kiwanda pacha cha kutengeneza mbolea ya kukuza mazao.

"Ujerumani kupitia mji wa Tubingen una mahusiano na Manispaa ya Moshi na imekubali kujenga kiwanda cha uzalishaji wa mbolea kwa kutumia taka ngumu zinazozalishwa viwandani na majumbani. Sasa ujenzi huo umeshaanza na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili mwaka huu," alisema. Kwa mujibu wa Mboya, kiwanda hicho kinajengwa katika Kijiji cha Mtakuja, Wilaya ya Hai.

Alisema Manispaa ya Moshi imenunua shamba lenye ukubwa wa ekari 40, ambapo pia linajengwa dampo kubwa la kisasa la kutupia takataka na kiwanda cha gesi ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme.

Aidha, meya huyo alisema Manispaa ya Moshi, imechangia ujenzi wa mradi huo Sh. milioni 400 na mji wa Tubingen wamekubali kutoa msaada wa mitambo na kuisafirisha kuja nchini, kulipa mishahara ya wafanyakazi kwa kipindi cha mwaka mmoja na kutoa elimu kwa wananchi na wanafunzi wa shule za msingi manufaa ya mradi huo.

Alisema Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, inakusudia kuongeza magari ya kubebea takataka na mitambo ya kuzolea yenye thamani ya Sh. milioni 750 na serikali ya Ujerumani imekubali kusaidia mradi kwa asilimia 80, na halmashauri itachangia asilimia 20 mradi huo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 18, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Mzozo siasa mtoto asoma 'shule pori'**



Ukurasa 15

Hamahama inavyonyima haki elimu kwa watoto wa Meatu



Ukurasa 18

## Simulizi ya uchungu wa kubakwa miaka 14




UNAMKUMBUKA KAMISHNA TIBAIGANA?

# Kila alikoenda hakuacha darasa Polisi Jamii

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Brass Band Polisi, alama ya jeshi



Bendi ya Poisi maarufu Brass Band, wakishiriki katika matukio mbalimbali, kwa nyakari tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





**Soma zaidi makala kuhusu Polisi Jamii uk 16.**

JIELIMISHE

# Namna gani usalama wako unasimamiwa?

**DOUALA,** Cameroon

MVULANA mwenye umri wa miaka 11, Mackjourney huenda akasoma katika shule ya siri nchini Cameroon.

Hiyo ni wakati hivi karibuni, familia yake ilitoroka uasi wa wanaotaka kujitenga katika majimbo yanayozungumza Kiingereza, wadhani kuwa wamepata mahali anaweza kusoma kwa usalama.

Hilo limegeuka kinyume, kwani shule anayohudhuria mjini Douala iko hatarini kufungwa, kwa sababu inadaiwa maofisa elimu kuwa ya haramu.

Shule kama hizo zisizokubalika kisheria zimeanzishwa kwa haraka mjini Douala, ambako wakazi wengi wanazungumza Kifaransa.

Nchi Cameroun, sehemu nyingi katika majimbo yake yanazungumza Kiingereza, hasa Kaskazini-Magharibi ikiwemo miji yake ya Bamenda na Kusini-Magharibi shule zake zimefungwa kwa miaka mitatu kuwafanya watoto zaidi ya 600,000 masomo.

"Niliondoka Bamenda kwa sababu kulikuwa na vita. Walikuwa wanawauwa watu na kuwapiga watu risasi," anasema Mackjourney, huku akibaninisha kwamba shule ambazo zimefungwa, ziko katika hatari ya kushambuliwa na wapiganaji wanaotaka kujitenga.

Anafafanua: "Tulikua tunakaa darasani na kusikia risasi zinaanguka kwenye paa la darasa kama mvua. Ilikuwa inatisha."

Baadhi ya wafanyabiashara mjini Douala wamejitolea kuwapa elimukwa gharama kubwa na kwake mtoto Mackjourney, hutembea umbali wa kilomita mbili kila asubuhi akipitia njia nyembamba eneo la vichaka kwenda katika shule yake iliyotengenezwa kwa mbao bila ya madirisha.

Kutoka ndani ya darasa wanaweza kuona majani marefu pande zote, eneo ambalo limechaguliwa iwe vigumu kugundulika na mamlaka za kisheria. Kuna shule ya pili kibinafsi, aliyokuwa anasoma mjini Douala, lakini ilifungwa na serikali kwa kuwa haikuidhinishwa.

Kwa mujibu wa vigezo vya kisheria vilivyokoko, ili shule isajiliwe ni sharti kuwa na vigezo kama uwanja wa kuchezea, maktaba na madarasa.

Hadi sasa ni shule 260 tangu mwanzo wa Septemba iliyopita, lakini wamiliki wa shule hizo wako tayari kuvunja sheria kwani kuna pesa wanazopata kutoka kwa wazazi wanaohangaika kuwapatia watoto wao elimu.

Huku karo ya shule ikiwa ni Dola za Marekani 200 (Sh.440, 000), kiwango ambacho ni mara nne ya malipo ya mwezi ya chini kwa mwaka, wanaweza kuingizia pesa hizo kupitia ghasia zilizosababishwa na mzozo.

"Kulipia gharama ya usajili halikua jambo rahisi kwetu ," anatamka Mackjourney.

Wazazi wengine waliokimbia mzozo, wamekosa chaguo kwani hali inaendelea kuwa ngumu zaidi kupata nafasi katika shule zinazokubaliwa na serikali.

Maofisa wamefunga zaidi ya shule 260 tangu mwanzo wa mwaka wa masomo mwezi Septemba na wakosoaji wanasema haikutoa suluhu mbadala.

Ofisa wa Idara ya Elimu jijini Douala, Sylvestre Fils Moukalla, anasema serikali ilichukua hatua za kuwapokea wanafunzi wanaotoroka mzozo

**MASOMO NYUMBANI**

Matatizo ya mzozo wa kitaaluma, yalianza mwaka 2016 nchini Cameroun, kutokana na uamuzi wa serikali wa kuongeza matumizi ya Kifaransa katika shule na mahakama, hususan katika majimbo yanayozungumza Kiingereza.

Suala muhimu katika mapambano ya wanaotaka kujitenga limekuwa ni kususia shule, pia kuwateka wanafunzi na walimu wanaokiuka amri.

Mnamo mwezi Februari, watu 176 wengi wakiwa ni wanafunzi, walitekwa na kuachiliwa siku mbili baadae na baadhi yao walitoroka kwenda katika maeneo yanayozungumza Kifaransa, huko wakisomea nyumbani.

**KWANINI HIVYO?**

- Ilitawaliwa na Ujerumani mwaka 1884
- Majeshi ya Uingereza na Ufaransa yaliwalazimisha Wajerumani



Wanafunzi wakiwa katika 'shule pori' yenye watoto, walimu wamekodiwa na wazazi wao. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA HAPPY SEVERINE, MEATU

# Hamahama inavyonyima haki elimu kwa watoto wa Meatu

"HAMAHAMA ya wananchi wilayani Meatu mkoani Simiyu, imekuwa ikisababisha watoto wengi wa familia za wafugaji zinazohama kukosa haki zao za msingi ikiweamo elimu," ndivyo anavyoanza kusimulia, Ofisa Mtendaji Kata ya Mwamanimba, wilayani Meatu, Charles Manota

Manota anataja sababu kubwa zinazofanya wananchi kuhama kila mwaka ni hali ya ukame unaoikumba wilaya hiyo anasema, licha ya ukame wananchi wengine unatokana na kukosa mashamba ya kilimo, malisho na wengi wao wanaenda mikoa ya Morogoro, Katavi, Rukwa na Tabora.

Mtendaji wa Kata, anaeleza kuwa kipindi cha mwezi Julai, Agosti, Sepetmba, Oktoba hadi Novemba, ndicho makundi makubwa ya wananchi jamii ya wafugaji wa wakulima wa wilaya hiyo wanakimbia kuhamia mikoa hiyo tajwa.

Manonta anabainisha, kuwa moja ya eneo ambalo watoto wadogo wameendelea kukosa haki hizo za msingi kwenye wilaya hiyo ni Kata ya Mwamanimba, ambayo kwa mwaka 2019 kaya nyingi zimehama kuyakimbia makazi yao, wakifuata malisho ya mifugo.

Manota anasema, kwa kipindi cha mwaka 2019 idadi kubwa ya wananchi katika kata hiyo wamehama kutokana na kipindi hicho kuwa na ukame mkali zaidi kuliko miaka yote.

"Unaweza ukaona kata nzima yenye vijiji vitano na kaya 12 zimehama na watoto wao wanaosoma kwenda katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kutafuta, maeneo ya kilimo na malisho bila kujali hao watoto wanaohama nao wanahaki ya kuendelea kupata elimu.

"Ukiangalia kwa wastani kila kaya moja ina watu kuanzia sita, na kati ya hao wanafunzi ni wanne, hivyo kuna zaidi ya watu 100 wamehama kwa mwaka huo, na hao wameondoka na watoto ambao ni wanafunzi wa shule za msingi," anaeleza Manota.

Ofisa Mtendaji Kata huyo, anaeleza kuwa moja ya haki wanazokosa watoto wa kaya hizo zinazohama kila mwaka, ni elimu, kwani wengi huwafanyisha watoto hao shughuli za kilimo na ufugaji kwenye maeneo ambayo wanahamia.

Anasema Watoto wengi wanaokosa haki hiyo ni kutoka shule za msingi, kuliko wale wa shule za sekondari na familia zao zinahama wakiwa bado wadogo na huko wanakohamia hawapelekwi shule tena.

Manota anasema, katika Shule ya Msingi Mabambasi iliyoko kwenye kata Mwamanimba, ni sehemu moja ya shule zinazoathirika kila mwaka na 'hamahama' hiyo ya wananchi, ni idadi kubwa ya wanafunzi wanapotea bila ya taarifa na kuwakosesha haki ya msingi ya kupata elimu itakayowasaidia katika kutimiza ndoto zao.



Wafugaji na wakulima wilayani Meatu, wakihama kuelekea mikoa mingine kufuata malisho na maeneo ya kilimo na mifugo, uamuzi wenye madhara kwa maendeleo ya elimu Meatu. **PICHA; HAPPY SEVERINE**

> "Wao hilo huwa hawafanyi, wanawatorosha na wakienda huko hawawapeleki shule, tena kwani wengi wao wanaenda kuishi porini.

### WALIMU WALALAMIKA

Walimu wa shule hiyo wanasema kuwa, wanafunzi wanaotoweka bila ya taarifa shuleni, wengi ni kutoka darasa la kwanza hadi la nne na wale wa chekechea, pindi wanapoanza kuwafuatilia, hupewa taarifa kuwa familia zao zimehama.

Christopher Mwalyambi ni Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, anasema wazazi wengi wanapoamua kuhama, huwa hawatoi taarifa kwenye uongozi wa shule wa kijiji na huwachukua watoto wao bila ya kufuata utaratibu.

"Tunajua kuhama siyo jambo baya, lakini kwa mwanafunzi kuna taratibu za uhamisho. Wao hilo huwa hawafanyi, wanawatorosha na wakienda huko hawawapeleki shule, tena kwani wengi wao wanaenda kuishi porini," anasema Mwalimu Mwalyambi.

"Watoto wengi ni kutoka darasa la kwanza hadi la nne na mtoto akifika darasa hilo ukimchukua bila ya uhamisho uko ambako unampeleka, siyo rahisi kupokelewa lazima kuwepo na taarifa zake," anaongeza.

Aidha, anasema kuwa mwaka huu walitarajia watoto 21 ambao walikuwa wamewaandaa kuanza darasa la awali mwaka jana, lakini saba kati ya hao hawajulikani waliko.

Mwalimu Mwalyambi anasema kuwa, watoto hao wanatoka kwenye familia mbili na wamepata taarifa zao kuwa, wazazi wao wamehama na kwenda mkoani Morogoro, kutokana na hali ya ukame iliyokuwamo mwaka jana.

" Tunajua watoto hao saba hawaendi kusoma tena, huo ndiyo mwisho wao wa elimu. Wanakosa haki yao ya msingi, tunajua wataendelea kupungua maana bado familia nyingi zinahama hasa kipindi hiki cha kilimo," anasema.

Emmanuel Zakayo, ni mwalimu wa darasa la kwanza shuleni hapo, anasema kuwa hama hama hiyo ya wananchi imekuwa ikiathiri shule, kwani baadhi ya wananfunzi wanaoachishwa masomo wamekuwa na uwezo mkubwa darasani.

"Jambo hili linatuvunja moyo wa kufundisha. Wanafunzi wengine unakuta wana uwezo mkubwa na mzuri darasani, lakini wanapelekwa hizo sehemu na hawapelekwi shule tena," anasema Mwalimu Zakayo.

Aidha, baadhi ya wakazi wa mji wa Mwanhuzi, wanasema wilaya hiyo awali ilikuwa na changamoto ya ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya Taifa, hata kushika nafasi ya pili kutoka mwisho kwa mara kadhaa, lakini kwa sasa tatizo hilo limeisha, limebaki ya wazi kuhama na kuwakatisha masomo watoto.

### MKAZI WA MEATU

Ruben George, mkazi wa mjini hapo, anabainisha kuwa Wilaya hiyo wakazi wake kwa asilimia 90 ni wafugaji, lakini mazingira ya maeneo yao ni kame hivyo hulazimika kuishi maisha ya kuhamahama wao na familia zao.

"Kutokana na idadi kubwa ya wazawa wa hapo kuwa ni wafugaji hivo kipindi cha kiangazi, wengi huhama na familia zao hali inayosababisha watoto wengi kushindwa kuendelea na masomo na kukosa haki ya elimu kwani hata huko wanakoenda hawapelekwi shule, badala yake hutumikishwa kwenye mifugo na kilimo,: anasema.

George anapendekeza kuwa, serikali kupitia wadau wa elimu itafute njia ya kulitatua hilo kwa kuwajengea hosteli na mabweni ambayo yatawasaidia watoto wa wafugaji na wakulima kubaki kuendelea na masomo pindi wazazi wao wanapotaka kuhama.

"Nashauri kama inawezekana serikali na wadau wa elimu ione namna itakavyotatua hilo...nahisi kulitatua kwake ni kujenga hosteli na mabweni yatakayowahifadhi kipindi wazazi wao watakapoanza kuhama," anamalizia George.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

UNAMKUMBUKA KAMISHNA ALFRED TIBAIGANA?

# Kila alikoenda hakuacha darasa Polisi Jamii

• Somo lake 'lilivyowakosha' dereva teksi • Analijua jiji, mithili ya bodaboda kazini • Masihara yalimgeuza mvuto wa kila kona

MAGEUZI makubwa kimataifa yanayoendana na kuja utandawazi, kwa kiasi kibubwa umeeneza kuwapo polisi jamii ambayo kwa wastani wa robo karne sasa au zaidi kidogo imemea nchini, mizizi yake ikiwa na safari ndefu ikishika kasi katika karne ya 20.

Nchini, Polisi Jamii ina nafasi kubwa sasa, inafanya kazi kubwa katika muonekano wa idara ndani ya Polisi, sehemu ya jukumu hilo ni lililozoekeka kwa jina; Dawati la Jinsia.

Ni mfumo wa kipolisi ambao mwanazuoni Bertus Ferrera, anaeleza kwamba, jeshi hilo linajenga uhusiano wake na jamii, kufanya kazi kwa pamoja kukabili na kuzuia uhalifu na msuguoano kwa kijamii.

Ferrera anatoa maana yake rasmi akitamka: "Ni falsafa ambayo utendaji wa askari wa polisi anakuwepo katika eneo maalum kutumikia kwa doria na ushirkikiano na raia wa mahali hapo kutambua matatizo (yanayohatarisha usalama) na kisha kuyatatua."

Msingi mkuu hapo unawekezwa katika uhusiano wa karibu kati ya polisi na wanajamii walioko katika kudhibiti na kufuta uhalifu ndani ya makundi yao.

Jijini Dar es Salaam, bado Kamishna Alfred Tibaigana anakumbukwa sana kwa utumishi wake, akiwa na sifa zote, mkali kwa anayeenda kinyume na utii wa sheria na wakati huo huo rafiki wa umma. Hapo, wanahabari wana ushahidi katika urafiki wao.

Kuna wakati alifika hatua anakuwa mkali sana dhidi ya wanahabari anapohisi wamemuendea kinyume, kisha huyo huyo aliyevurugana naye anapokutana naye tena, anakuwa rafiki tena akimtania kwa 'kumpa vidonge' vya kinidhamu kama kaka, mjomba au baba mdogo, maana wengi walikuwa vijana wadogo kwake.

Kamishna Tibaigana, hakuuficha ukada wake wa polisi jamii, kuna wakati aliwachekesha pale alipouambia mkutano mmoja wa kikazi na wadau wake, akitaja mahali alikozoea kunyoa nywele, ni kwenye mchangayiko hasa wa jamii, ambako wengi hawakumtegemea.

Siku moja akiwa katika kikao cha kuhimiza namna gani polisi jamii inaweza kutimizwa kati ya Polisi na madereva wa teksi, Kamishna Tibaigana alishangaza kwa mambo makuu matatu:

Anaijua vyema kazi ya teksi; anaelewa vyema jiji lakwe kwa 'vipengele' na kile kinachoendelea; pia mbinu zinazowafaa madereva teksi kujihami na kufanya kazi zao kwa usalama. Anajuaje? Siri yake kikazi!

Siku hiyo akiwa amevaa kiraia katika ukumbi wa Polisi Barracks, Kilwa Road, Kamishna Tbaigana akiwa na umati wa madereva teksi aliowaalika, aliwaambia amevaa hivyo ili siku hiyo wawe 'wenzake' kila mmoja amtegenezee mwenziwe kazi kwa kuwajibikia eneo lake la usalama wa polisi jamii.



Alfred Tibaigana, katika maisha ya ustaafu, nyumbani mkoani Kagera. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Ni jambo lililowashangaza madereva teksi namna anavyofahamu mji kila hatua, baadhi ya baa, migahawa na vijiwe kila moja kwa wasifu wake...

Aliwachekesha pale alipowaambia ameamua kwenda kwenye ukumbi huo maana uko chini ya himaya yake na mkutano huo si rahisi kukatizwa kwa dharura, tofauti na Oysterbay Police Officers Mess, ambako wangeweza kumkatiza kwa dharura nyinginezo.

Kamishna Tibaigana, aliwapa dodoso namna anavyoujua udereva wa teksi kwa kina tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970, aliwachambulia mengi ya ndani kuhusu kazi yao na kisha akamaliza kuwahoji ni wangapi wanaolaza magari yakiwa na mafuta mengi? (wakihofu wanaweza kunyang'anywa ufunguo wakati wowote ).

Hapo madereva teksi waliagua kicheko cha mshangao alivyojua siri yao, nao wakamuamini kauli yake ya utangulizi kuwa anaifahamu vyema kazi hiyo hata akajitambulisha ni 'teksi dereva.'



Aliendelea kwa kuwaasa kuwa makini na abiria, pia madereva wenzao wanaokuwa nao katika vijiwe vya kazini, ambao si waadilifu, akiwamegea njia za kuijulisha Polisi ichukue hatua, naye akiahidi kuwatetea wasionewe.

Ndipo ilipofika hatua Kamishna Tibaigana 'alipowaacha hoi' waendesha teksi namna ya kumgundua abiria mhalifu, mathalan anapokodi usafiri kutoka Buza hadi Tegeta, akichambua maeneo ya mfano, kwa weledi unaofanana na mwendesha bodaboda au kondakta wa daladala.

Ni jambo lililowashangaza madereva teksi namna anavyofahamu mji kila hatua, baadhi ya baa, migahawa na vijiwe kila moja kwa wasifu wake, baadhi wakajikuta wanampigia makofi.

Ilipofika zamu yao madereva teksi hao kutoa maoni, baadhi walilalamika kwa baadhi ya mambo, KamishnaTibaigana, alirejea kuwashangaza alipoainisha anavyolijua hilo ni tatizo na ahadi ya papo kwa hapo kulitatua.

Hapo alienda mbali kuwaambia madereva namna anavyofahamu baadhi ya upungufu akiwatania katika lafudhi yake: "Tunajua, lakini tunawaachia watoto wapate 'mukate'..."

Ni kikao kilichoisha Kamishna Tibaigana na waalikwa wapo madereva Polisi, wote wakitabasamu kirafiki wakiahidi kushirikiana.

Kimsingi, katika hadhira tofauti alikuwa na simulizi nyingi za kina namna ambavyo Polisi Jamii imefanya nchini Marekani kwa mafanikio, akisimulia hata vituo vya polisi ambavyo si vingi sana.

Kamanda Tibaigana alifika jijini Dar es Salaam kurithi jukumu kutoka kwa mtangulizi wake walioitana 'wajina' Naibu Kamishna Alfred Gewe, yeye akiwa na cheo cha Kamishna Msaidizi Mwandamizi.

Ni katika zama za uongozi wake, jiji la Dar es Salaam lilipandishwa hadhi kuwa Kanda Maalum ya Mkoa Dar es Salaam, Tibaigana naye akikwea kutoka Naibu Kamishna hadi Kamishna, hapo alipolingana cheo na makamishna wakuu waliomsaidia kazi Inspekta Jenerali wa Polisi.



Kamishna Alfred Tibaigana, alipokuwa kazini.

> Tunajua, lakini tunawaachia watoto wapate 'mukate'...

Hao ni kama Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI); Kamishna wa Utawala na Fedha: Kamishna wa Operesheni na Mafunzo; pia Kamishna anayehusika na Zanzibar.

Inakumbukwa siku yake ya kwanza kuonekana mbele ya jamii tangu apanidishwe cheo hicho, Kamishna Tibaigana akionyesha masihara na Polisi Jamii iilivyomkaa kila mahali akihamasisha kujenga ubia wa jamii na jeshi hilo, alidai hatoanza mpaka wanahabari wa ITV wafike.

Hapo wanahabari wakamrejeshea maswaIi "kulikoni mpaka wafike hao (ITV)?" Naye hakusita kujibu kwa utani: "Ni televisheni inayoonekana vizuri hadi nyumbani" huku akiwahamasisha wapiga picha 'wajitahidi kumulikia begani (kwenye cheo)' aonekane kwao... huku akicheka.

Hakika, Alfred Tibaigana alivaana na Polisi Jamii, katika zama za utendaji wake Polisi.

Ni zaidi ya miaka 11 na nusu sasa tangu akabidhi ofisi kwa mrithi wake Suleiman Kova, alipotaja siri ya mfanikio yake kikazi, siku ya kukabidhiana ofisi kwamba ni ushirikiano kutoka serkalini, wabunge, mameya, viongozi wa serikali za mitaa na jamii kwa jumla.

## Kila siku unakula. Hiko chakula kina nini kwako?



Mlo kwa afya ya wanadamu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MSAMIATI chakula unaanzia katika kitenzi 'kitu kula'na watu wanatumia kudumisha na kustawisha uhai wao. Ni kwamba, mwili unahitaji virutubishi kama nishati na maji. Hayo yote hupatikana katika chakula.

Virutubishi vya mwili, vinajumuisha protini. Mafuta, wanga au kabohadrati, vitamin na madini.Kwa ujumla chakula kinaangukia makundi makuu matatu: Vya kujenga mwili kama nyama na maziwa; kulinda mwili kama vile mboga na matunda; pia cha kuupa mwili nguvu- wanga.

Vyakula hukuza mwili yaani katika mfumo wa mmeng'enyo wa chakula tumboni, vinapasuliwa kwa sehemu asilia zake na kuingizwa katika muundo wa seli za mwili.

Pia, kinaweza kutoka kwenye mimea au kwa wanayama. Sehemu ya mahitaji yanatoka pia moja kwa moja kwenye mazingira, kupitia mimea na wanyama, hasa madini kama vile chumvi

Inaelezwa chakula haishii katika kazi ya kibaioliojia na kifiziolojia pekee, bali kina upande wa utamaduni na kijamii.

Kila nchi ina chakula chake na watu wamezoea vyakula pamoja na namna ya kutayarisha vyakula vyao. Huo ni muundo wa maisha unaoangukia dhana utamaduni.

**CHAKULA & AFYA**

Chakula kinatakiwa kuwa na sehemu zote zinazohitajiwa na mwili. Uhaba wa sehemu moja utasababisha upungufu kama utapiamlo na magonjwa mbalimbali.

Kuna matatizo hasa kama watoto hukosa chakula chenye ulinganifu. Kuna baadhi ya wanajamii na hasa kinamama, wanawapa watoto chakula wakijali tu kwamba mtoto ashibe.

Mtu anaweza kushiba kutokana na wanga peke yake, lakini uhaba wa protini na vitamin, humletea utapiamlo na kusababisha magonjwa, inaishia watoto wanakuwa na upungufu wa kukua kwa sehemu za ubongo na kimwili. Vilevile kuna tatizo la kila mara: ni uhaba wa madini fulani katika mazingira ya kipekee. Chakula kinahusiana na afya, pia kinahusu wingi au uhaba wake. Inaeleweka kwamba, uhaba wa chakula yaani njaa ya muda mrefu, nayo inadhoofisha mwili na afya kwa jumla.

Kinyume chake, nako kuzidi kwa chakula kunaleta hatari. Hapo inamaanisha mwili kupoewa mlo wa ziada. Katika maisha hasa ya mijini, hali ya kunenepa kwa mtoto tangu utotoni nako kumekuwa tatizo kubwa.

Huko kunenepa mno kunafupisha maisha na kuandaa mwili kwa magonjwa mengi yasiyotarajiwa katika hali ya kawaida

Vyakula vingi hutokana na mimea. Hata wanyama nao wanatumiwa chakula kwa kanuni za kibinadamu. Huwa wanafugwa na kupewa vyakula vinavyotokana na mimea. Hivi sasa asilimia 75 ya vyakula vinavyoliwa na binadamu, vinatokana na wanyama na mimea. Baadhi ya vyakula vya nafaka kama mahindi, ngano na mchele

Ngano ndiyo nafaka yenye nishati ya juu kuliko nyinginezo zote duniani.

Vyakula binadamu, mbali nafaka, inajumuisha matunda, mboga, jamii ya maharage, mboga za majani, viungo, nyama, samaki, mayai, maziwa na asali

**Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za afya.**

JE, WAJUA?

# Simulizi ya uchungu wa kubakwa miaka 14



Ndiye mwanamke Rose, katika mwonekano wa sasa. **PICHA: BBC**

MWAKA jana, Rose aliandika kwenye blogu akieleza namna ilivyokuwa tabu kwake alipobakwa akiwa na umri wa miaka 14. Watu wengi walimtafuta wakisema kuwa wanakumbwa na tatizo hilohilo hivi leo.

Muuguzi alimzuia, alisimama mlangoni alipokuwa akitazama kwenye chumba cha hospitali alimokuwa Rose kisha aligeuka kumtazama "Pole sana kwa kilichokutokea," alisema sauti yake ikitetemeka, akitamka: "Binti yangu pia alibakwa."

Rose alimuangalia muuguzi ambaye kwa kukadiria, hakuwa na umri unaozidi miaka 40. Hapo wazo la Rose likasafiri mbali, kwamba yeye na binti wa muuguzi, wanaweza kuwa na umri sawa.

Alikumbuka asubuhi ile baada ya tukio la kubakwa, alikumbuka mazungumzo yake na polisi ambaye hakuonuesha chembe ya huruma. Kila mtu alitumia neno "madai" walipokuwa wakielezea tukio lililoelezwa na Rose.

Ukiacha baba yake na Bibi yake, walezi wake wengi nao hawakumuamini. Kwa muuguzi ilikuwa tofauti, Rose akimtafsiri 'aliniamini.' Ilikuwa jambo lililompa matumaini sana kwa watu kutambua kilichotokea. Ahueni ilikuwepo, ikiashiria mwanzo wa kupona.

Baada ya muda mfupi, maelfu ya watu wakaanza kuona tukio hilo la ubakaji wao wenyewe na kwa wale ambao hawakusikitishwa na tukio hilo. Mtu aliimuibuka akiwa amemshikia kisu, alimlazimisha aingie kwenye gari. Katika kiti cha abiria alikuwa mtu wa pili, mwenye umri wa wastani miaka 19. Alikuwa huwa anamuona mjini.

Walimpeleka nyumbani kwenye makazi kando ya mji na wakambaka kwa muda wa saa 12, wakati mtu wa tatu alikuwa akipiga picha za video wakati wa tukio hilo.

Rose alikuwa katika mshtuko - hakuweza kupumua. Alipigwa vibaya na kuchomwa kisu kwenye mguu wake wa kushoto, nguo zake ziliiloa damu. Alianguka na kupoteza fahamu.

Wakati fulani, mmoja wa wanaume hao alitoa kompyuta mpakato na kumuonyesha video Rose zilizochukuliwa wakati walipokuwa wakiwabaka wanawake wengine .

Baadaye, wanaume hao waliitishia kumuua. Kwa kujilazimisha, Rose alianza kuongea nao, ikiwa wangemwachilia, asingeweza kuwatambua, anasema. hakuna kitu kingewatokea, wala mtu ambaye angelijua hilo.

Walipomrudisha ndani ya gari, wanaume hao walimtupa barabarani karibu umbali wa nusu saa kutoka nyumbani kwake, akitembea kupitia mlango, alijiona kwenye kioo cha ukumbini . Ni mshtuko kichwani kujaa damu.

Baba yake aitwaye, Ron na wana familia kadhaa walikuwa sebuleni kula chakula cha mchana. Bado damu ikichuruzika kutoka kwenye jeraha lake alipochomwa, akawaeleza kilichomtokea.

"Baba yangu aliipigia simu Polisi. Alinifariji, lakini wengine walisema nimependa mwenyewe kutembea usiku sana," Rose anasimulia.

Huko hospitalini, Rose alionwa na daktari wa kiume na Ofisa wa Polisi wa Kiume, aliyemuuliza ikiwa tukio hilo lilianza kwa makubaliano?

Rose aliwajibu 'hapana' kwamba hayakuwepo makubaliano yoyote na hakumjua aliyemshambulia. Polisi walishindwa kupata chanzo cha kuendelea na uchunguzi.

Rose alipoachiwa siku iliyofuata, alijaribu kujiua. Kilichomsukuma, ni pale aliposhindwa kupata majibu ya namna gani angeweza kuishi maisha ya kawaida. Kaka yake alimuokoa dhidi ya jaribio hilo.

Miezi michache baadaye, Rose alikuwa akirambaza kwenye mtandao wa MySpace, aliwakuta watu kadhaa anaosoma nao wakishirikishana anuani, kisha wakamtumia.

Alipoifungua, ikamuonyesha mtandao wa ngono. Alijisikia kichefuchefu na alipoona video zilizorekodiwa alipokuwa akibakwa.

Vichwa vya video hizo vilieleza yaliyokuwa yakifanyika katika video hizo, moja ikiwa imetazamwa na kutolewa maoni 400,000, Rose anaeleza. Hapo hapo alifanya uamuzi wa kutoiambia familia yake kuhusu video hizo. Aliamini kuwaambia kusingewasaidia chochote.

Ndani ya siku kadhaa ilikuwa wazi kabisa kuwa wengi wa wanafunzi wenzake waliziona video hizo.

Rose anasema alituma barua pepe kwa mtandao wa Pornhub mara kadhaa kwa muda wa miezi sita mnamo 2009 ili kuomba video hizo ziondolewe

"Nilituma barua pepe nikiomba... tafadhali, mimi ni mtoto. Hili lilikuwa shambulio, tafadhali iondoeni. "

Hakupokea jibu na video zilibaki moja kwa moja na mwaka uliofuata alijitenga.

Alikuwa akijiuliza kila anapokutana na watu wakamuangalia, alijiuliza kama wameona video hizo.

Hakuweza kuvumilia kujiangalia. Ndio sababu alifunika vioo na blanketi, alikuwa akiosha meno yake na kunawa gizani, akifikiria wakati wote juu ya nani anaweza kutazama video hizo.

Kisha akapata wazo na kuandika barua pepe nyingine akijifanya mwanasheria na kuitishia kwa barua pepe kuwa atachukua hatua ya kisheria dhidi yao na ndani ya saa 48 video hizo zilitoweka.'

Miezi kadhaa baadaye, Rose alipata ushauri nasaha, hatimaye alieleza mwonekano wa waliombaka kwa mwanasaikolojia. Lakini hakuiambia familia yake wala Polisi kuhusu video hiyo.

Polisi walichukua maelezo muhimu kutoka kwa Rose na familia yake. Wakili wa waliombaka walisema kuwa Rose aliridhia na wanaume hao walishitakiwa si kwa ubakaji, bali kitendo chao cha kumchangia binti huyo mdogo kufanya ngono.

Rose na familia yake hawakuwa na nguvu au rasilimali za kupambana kuhakikisha wanapata adhabu kali. **BBC**

## RIPOTI

# Uhaba wa damu Kenya

**Na Mwandishi Wetu**

KENYA imetajwa kukabiliwa na uhaba mkubwa wa damu ya binadamu hospitalini, hali inayowafanya ndugu na jamaa ya wanaotaka msaada, kutumia mitandao ya kijamii kuwaomba jamaa na marafiki msaada wa mchango wa damu.

Shirika la Msalaba Mwekundu, limetaarifu kupitia mitandao, pia likichapisha ujumbe kwenye mtandao wa Twitter kuwasaidia wanaohitaji damu.

Tayari mwezi huu, wameshachapisha ujumbe kutoka kwa zaidi ya watu 10 waliohitaji damu kwa dharura katika hospitali mbalimbali nchini humo.

Shirika la Afya Duniani (WHO), imetoa ushauri kuhusu sehemu ya jumla ya idadi ya watu katika taifa husika wanaofaa kutoa damu ndipo taifa liweze kujitosheleza, Kenya inafaa kukusanya vipimo milioni moja vya damu.

WHO inapendekeza asilimia moja hadi tatu ya watu wake kutoa damu kila mwaka. Taifa la Kenya inakadiriwa kuwa na watu milioni 47, iwapo asilimia moja ya raia hao wangetoa damu, Kenya ingepata vipimo 470,000 vya damu kila mwaka.

Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vipimo 164,000 vya damu ndivyo vilikusanywa, kiasi ambacho kinatajwa kuwa cha chini ikilinganisha na kiasi kinachofaa.

Inalalamikiwa wakazi wengi wa nchi hiyo ni wazito kutoa damu yao, ikirejewa mwaka 2018, asilimia 77 ya wakazi walitoa damu ilikuwa mara yao ya kwanza, ikimaanisha kwamba watu hawana mazoea ya kutoa damu.

Kuwapo idadi kubwa ya watu wenye mazoea ya kutoa damu, kunahakikisha nchi kuwapo kiwango cha kutosha cha damu na inachotakiwa ni watu kujitolea kwenda kwenye vituo vya kuchangia damu, pasipo gharama ya kuwatafuta.

Kwanini uhaba? Sehemu kubwa ya ufadhili wa mfumo mzima wa kukusanya damu nchini Kenya, ulikuwa unategemea wafadhili wa kigeni na ripoti ya serikali ya Kenya iliyotolewa hivi karibuni, inasema wafadhili waligharimia asilimia 80 ya fedha zote za kukusanya na kuhifadhi damu.

Inaelezwa, Kenya ilichangia takriban Sh. bilioni 1.6 za nchi hiyo au sawa na Dola za Marekani milioni 16 (Sh. za Kitanzania bilioni 35.2).

Fedha hizo zilihakikisha ununuzi wa vifaa na mitambo ya kuchangia na kuhifadhi damu, kuajiri wafanyakazi na kugharamia mahitaji mengine.

Mfadhili Mkuu anatajwa kuwa serikali ya Marekani kupitia Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na Ukimwi, maarufu kama Pepfar.

Mpango huo lengo lake lilikuwa kusaidia kuokoa maisha ya walio na virusi vya Ukimwi katika mataifa mbalimbali duniani.

Inadaiwa fedha hizo zinazotolewa kupitia mpango huo zilipunguzwa sana Septemba mwaka jana na mgawo uliokuwa unatolewa kufadhili mfumo wa damu Kenya kusitishwa.

Ripoti ya serikali iliyotolewa Desemba ilitahadharisha kuhusu hatari iliyokuwa njiani, ikisema: "Huduma ya Taifa ya damu inakabiliwa na hatari ya kupungukiwa sana na damu" ikaomba ufadhili wa haraka kutoka kwa hazina kuu.

**Kwa mujibu wa BBC**




Uchangiaji damu ukiendelea nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU
NA GWAMAKA ALIPIPI

MIAKA 38 YA CHUO KAMILI

# NIT sasa kuhamia sekta ya anga

• Marubani, wahudumu hapahapa • Ndege za mafunzo njiani zinakuja • Kwenye reli, nako marafiki China



Ndege ya mafunzo ya urubani chuoni NIT. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji kina hisitoria ndefu. Kilianza mwaka 1975, kikiwa ni kitengo muhimu cha mafunzo cha lililokuwa Shirika la Taifa la Usafarishaji (NTC).

Hilo lilikuwa shirika mama chini yake kukiwapo, taassi kama Kampuni ya Mabasi ya Taifa (Kamata), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na Shirika la Usafirishaji Mikoani (RETCO), ambayo ilimiliki malori kusafirisha mizigo mikoa mbalimbali..

Kutokana na kuonekana haja ya kuwapo mageuzi katika na haja zaidi ya mafunzo ya juu na ya kina, NIT ilifanyiwa mageuzi ya kisheria kuwa chuo cha elimu ya juu mwaka 1982 na mwaka mmoja baadaye ikaanza kupokea wanafunzi.

Kwa muda mrefu imekuwa ikitoa kozi mbalimbali, ikiwamo ya usimamizi wa usafiri na ufundi mitambo wa magari, kwa ngazi ya diploma na diploma za juu (advanced diploma).

**MAGEUZI MAPYA**

NIT sasa imepiga hatua kwa kuja na kozi mpya katika historia yake, ikitarajia kuanzisha mafunzo ya urubani ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Ni nyongeza, kwani NIT katika maendeleo yake ya karibuni imekuwa ikifundisha kozi mbalimbali kama vile usafiri wa reli ilikozalisha wahandisi wa kuhudumu mabehewa na wataalamu wa teknolojia ya mawasiliano ya reli.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof, Zacharia Mganilwa, anasema hiyo nyongeza kwa mafunzo ya udereva magari, uchukuzi na ugavi, ikijitanua kuisaidia serikali kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Anasema, NIT kinatarajia kupokea ndege mbili aina ya Cessna 172 ifikapo Oktoba mwaka huu, kwa ajili ya kufundishia masomo ya urubani na Prof. Mganilwa anasema, maandalizi ya kuanza kufundishia kama vile madarasa na walimu yameshakamilika na kinachosubiriwa ni ujio wa ndege hizo.

"Hizi ndege tunatarajia kuzipokea kuanzia kipindi cha Oktoba hadi Novemba mwaka huu, tutapokea ndege mbili aina ya Cessna 172 zitakazotoka Marekani na zitakuwa na uwezo wa kuchukua abiria wanne,"anasema Prof. Mganilwa.

**UHABA MARUBANI**

Wakati wa mahafali ya 34 ya chuo hicho yaliyofanyika Desemba mwaka juzi, Prof. Mganilwa alieleza kwa sasa nchi ina upungufu mkubwa wa marubani na kwamba asilimia 60 ya marubani waliopo wana umri kuanzia miaka 55 na wengi ni raia wa kigeni.

Anasema, idadi ya marubani waliopo nchini ni 400, lakini mahitaji halisi ni wastani wa marubani 700 hadi 800 na kwamba NIT kuanza kufundisha masomo hayo, itasaidia kupunguza uhaba wa wataalamu hao.

> Hizi ndege tunatarajia kuzipokea kuanzia kipindi cha Oktoba hadi Novemba mwaka huu, tutapokea ndege mbili aina ya Cessna 172 zitakazotoka Marekani na zitakuwa na uwezo wa kuchukua abiria wanne.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa.

Prof. Mganilwa anasema NIT ilipokea mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) wa Dola za Marekani milioni 21.5 (Sh. bilioni 47.3) ambazo zitatumika kujenga kituo cha umahiri na ununuzi wa ndege tano za mafunzo.

Prof. Mganilwa anaeleza kuwa ndege moja inaporuka ndani ya nchi, inahitaji kuwa marubani watatu hadi wanne, lakini inapoenda nje ya nchi inahitaji kuwa na marubani saba hadi nane.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Hamza Johari, anasema gharama ya kumsomesha mwanafunzi mmoja masomo ya urubani nje ya nchi yanafikia Sh. Milioni 120 na anafafanua:

"Kama nchi tumekuwa tukiingia gharama kubwa ya kuwasomesha marubani nje ya nchi, kwa mwaka 2018 tumewapeleka wanafunzi saba na mwakani (2019) tunarajia kuwapeleka wengi zaidi."

Prof. Mganilwa anaeleza, pia wanafundisha masomo ya uhudumu ndani ya ndege, akiongeza: "Walimu tunao, wahudumu ndani ya ndege tumeshatoa mikupuo miwili na mkupuo wa tatu wapo darasani na wahandisi wa ndege wameshahitimu mikupuo miwili."

**WATAALAMU RELI**

Anasema NIT imeshagiza vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 50 vyote kwa ajili ya kufundisha stadi za usafiri wa ndege, reli na sekta ya majini na chuo kilitia saini makubaliano na Chuo cha Zhengzhou Railway Vocational and Technical cha China, kuwaandaa wataalamu wa kuendesha Reli ya Kisasa (SGR).

Prof. Zacharia Mganilwaa anawaeleza maudhui ya makubaliano ni kwamba, wataweza kuzalisha watunga sera za reli, maofisa usafirishaji reli na kuwajengea uwezo wataalamu wengine katika sekta ya usafirishaji nchini.

Wakati wa makubaliano hayo, Prof. Mganilwa alieleza kuwa walimu kutoka China watakuja NIT kuwafundisha wanafunzi wafanyakazi walioko katika mashirika ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhusu uendeshaji reli na kwamba watahudumia SGR kwa ufasaha zaidi.

Prof. Mganilwa anaeleza sababu ya kushirikiana na China, kwamba nchi hiyo imebobea katika masuala ya reli, hivyo ushirikiano huo utainufaisha Tanzania, ambayo kwa sasa inaenda katika uchumi wa viwanda, pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa - SGR.

"Unapojenga uchumi wa viwanda ni lazima uwe na reli madhubuti, na ndiyo maana Rais John Magufuli ameamua kujenga reli ya kisasa, sasa tutapata walimu wa kutufundisha kuhusu masuala ya reli na namna gani ya kuiendesha reli yetu tunayojenga," anasema Prof. Mganilwa.

Anaongeza kwamba Tanzania ina wataalamu wa reli waliobobea katika opereshieni za reli, hivyo kupitia makubaliano hayo kutaongeza wataalamu wa sera za reli na maofisa usafirishaji katika njia ya reli.

Katika makubaliano hayo, Rais wa Chuo cha Zhengzhou Railway Vocational and Technical cha nchini China, Kong Fanshi aliihakikishia NIT kwamba, uhusiano waliyoanzisha utakuwa na manufaa baina yao.

"Tuna matumaini makubwa katika ushirikiano huu na tunaahidi kuleta walimu wetu hapa NIT kwa lengo la kubadilishana uzoefu," anasema Fanshi.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

Moja ya tatizo linalozikabili shule za umma na kusababisha wanafunzi kukosa baadhi ya masomo, ni uhaba wa walimu. Nini kifanyike kumaliza tatizo hili? Wadau wanajadili.



**FENA MAGIRI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TATIZO ninaloliona ni kwamba ugawaji wa walimu kati ya mijini na vijijini hauna uwiano kabisa.

Walimu wengi wanalundikana katika shule za mijini wakati zile za vijijini wapo wachache wasiotosheleza kufundisha masomo yote na kusababisha wanafunzi wafundishwe masomo machache tu, hasa wa sekondari. Umefika wakati sasa kuangalia uwezekano wa kupangua mlundikanao wa walimu katika shule za mijini na kuwapeleka vijijini.

Pia kuhamasisha vijana waliosomea ualimu, kwenda kufundikisha katika shule za vijijini kwao. Vinginevyo watakuwa wanaajiriwa na kuendelea kulundikana mjini tu kana kwamba vijijini hakuna shule. Nakumbuka kuna wakati kulikuwa na mkakati wa kuhamisha walimu toka mijini kwenda vijijini, sijui mkakati huo uliishia wapi, lakini ulikuwa mzuri na ungesaidia japo kupunguza tatizo la uhaba wa walimu, wa shule za msingi na sekondari, ambao umeendelea kuwapo licha ya kuajiri wapya.

Miaka ya nyuma tatizo la uhaba wa walimu katika shule za msingi na sekondari, lilisababisha serikali kubuni mpango wa mafunzo ya miezi mitatu kwa wahitimu wa kidato cha nne na cha sita ili kukidhi mahitaji hayo. Kwa hiyo mbinu nyingine ziendelee kuibuliwa kwa lengo la kumaliza tatizo hili.

Lakini kama nilivyosema, kuna walimu wamelundikana katika shule za mijini, wapunguzwe na kupelekwa wakafundishwe katika shule za vijijini. Hatua hiyo ikichukuliwa inaweza kusaidia wanafunzi kutumiza ndoto zao katika elimu na hasa kuwa na urahisi wa kuchagua tahasusi wanayotaka.



**SABATO MGUTU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KAULI ya serikali kuhusu uhaba wa walimu nchini ni kwamba, inaendelea na mkakati wa kupunguza tatizo la uhaba huo kwa shule za msingi na sekondari ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, imeshasema kwamba ametoa ajira 4,549 kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu shuleni.

Hivyo walimu wenye sifa wakatakiwa kuchangamkia fursa ya ajira kwa kutuma maombi yao, lakini katika hilo, waombaji wawe tayari kufanya kazi sehemu yoyote, kwani serikali inapanga kulingana na maeneo yenye uhitaji wa walimu wenye sifa husika, katika maeneo hayo, na ndiyo inayojua wapi kuna upungufu wa walimu.

Kikubwa zaidi walimu kufanya kazi kwa moyo mmoja na weledi wa juu, ili kuhakikisha watoto wa Kitanzania wananufaika na elimu inayotolewa na wao.

Hayo ndiyo maelezo ambayo yamewahi kutolewa na serikali.

Sijui walimu waliajiriwa wakakataa kwenda kwenye vituo vya kazi walivyopangiwa au walimu waliotakiwa kuomba ajira bado ni ndogo!

Ninaiomba serikali iongeze kasi katika mkakati wake wa kuajiri walimu na pia kuhakikisha wanakwenda kwenye vituo walivyopangiwa, kwani hatua hiyo itasaidia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa tatizo hili la uhaba wa walimu ambalo sasa linaonekana kuwa sugu kwenye shule za umma.

Ukienda katika shule za binafsi, utakuta walimu wanakwenda kwa wingi kuomba ajira.



**ISSA NJINJO (MWALIMU MSTAAFU, MKAZI WA RUANGWA LINDI)**

SERIKALI imejitahidi kuboresha shule zake nchini, lakini suala la uhaba wa walimu wa shule za msingi na sekondari ni tatizo ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Karibu kila taarifa za walimu wakuu kuelezea maendeleo ya shule zao, utakuta suala la uhaba wa walimu lipo, kwani uhaba huo ni miongoni mwa matatizo yanayozikumba shule za umma na uhaba huo unakwamisha utoaji elimu bora kwa wanafunzi.

Unaweza kukuta shule ina walimu wachache na nyingine mmoja. Utagemea katika mazingira hayo wanafunzi wanaweza kufundishwa masomo yote? Ushauri wangu ni kwamba serikali iangalie upya suala la ajira za walimu ili kumaliza tatizo hilo.

Imeongeza shule za msingi kuwa nyingi, uongezaji wa shule ingekwenda sambamba na uongezaji wa walimu. Siku hizi unakuta ndani ya eneo ambalo lilikuwa na shule moja, zimejengwa mbili, kwa lengo ya kupunguza msongamano wa wanafunzi wengi katika madarasa.

Hatua hii ni nzuri, ila imekumbana na hilo tatizo la uhaba wa walimu, ambalo kwa kweli ni kikwazo kikubwa kwa watoto wa Kitanzania kupata elimu bora.

Kama kuna uwezekano wa kupunguza wingi wa walimu kwenye baadhi ya shule na kuwapeleka kule ambako kuna uhaba, basi hilo lifanyike, ili angalau kupunguza ukubwa wa tatizo hili ambalo lipo kwa miaka mingi.



**HASIBU MVUNGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KATIKA juhudi za kuleta mapinduzi ya kiuchumi ili kuibadili Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Serikali inasema kuwa sekta ya elimu na mafunzo, kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mpango wa muda mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/12 hadi 2024/25, inatarajiwa kuleta maendeleo ya haraka ya rasilimaliwatu kwa kutayarisha idadi ya kutosha ya

Watanzania walioelimika na kupenda kujielimisha zaidi ili kulifanya taifa lipate maendeleo na kuwa lenye uchumi wa kati na shindani ifikapo mwaka 2025.

Ili kufikia lengo hilo, mfumo wa elimu na mafunzo unaotumika nchini lazima utoe fursa za kutosha kwa watu kujielimisha.

Pia mfumo huo unawajibika kutoa elimu na mafunzo yenye ubora unaokubalika na kutambulika kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika kufanikisha hili, Serikali imekuwa ikitekeleza sera mbalimbali, hususan, Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo (1996), Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu (1999) na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Elimumsingi (2007) na kuwa na mafanikio mbalimbali.

Lakini bado kuna changamoto mbalimbali zikiwamo za uhaba wa walimu na hata wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Uhaba wa walimu utazamwe kwa jicha la ziada na kupatiwa ufumbuzi haraka ili wanafunzi wasiendelee kufundishwa nusunusu.



**SOMOE DANIEL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ELIMU bora na yenye tija kwa maendeleo ya taifa ni ya muhimu sana, hasa shule zikiwa na walimu wa kutosha, lakini siyo bora walimu bali walimu bora.

Bahati mbaya hapa nchini unakuta shule ina mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi zaidi ya 200.

Unadhani katika mazingira kama hayo kuna elimu bora kweli kama siyo bora liende tu? Dar es Salaam. Uhaba wa walimu unachangia kuzorotesha sekta ya elimu nchini.

Unakuta baadhi ya shule na hasa za sekondari zikiwa na walimu wa kujitolea ambao wanalipwa posho na wazazi ili angalau watoto wawe wafundishwe masomo yote kuliko kwenda shule na kujikuta wakisoma masomo machache tu, kwa sababu ya uhaba wa walimu.

Wakati mwingine unakuta wahitimu wa kidato cha sita wanawafundisha wanafunzi wa kidato cha sita, hali ambayo kwa kweli haiwezi kuwa matokeo mazuri.

Ukifuatilia utagundua kuwa tatizo hilo liko katika shule nyingi za serikali na pia siyo ajabu kukuta mwalimu mwenye elimu ya diploma anafundisha zaidi wanafunzi wa kidato cha nne kana kwamba ni sahihi na kumbe sivyo, kwani walimu wenye shahada ndiyo wanatakiwa kufundisha wanafanzi wa kidato hicho.



## HABARI MBEYA

# Wafanyabiashara wa pembejeo wadaiwa kuchakachua

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo mkoani Mbeya, wanadaiwa kufungua mbegu za mazao zilizofungashwa na kampuni za uzalishaji wa mbegu na kuuza kidogo kulingana na mahitaji ya wananchi.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Mfawidhi wa Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu nchini (Tosci) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Nasari, wakati wa mafunzo kwa wazalishaji na wasambazaji wa mbegu wa Mkoa wa Mbeya.

Nasari alisema kitendo hicho ni kosa kwa mujibu wa sheria na kwamba kitendo hicho kinahesabika kwa mujibu wa sheria kuwa ni uchakachuaji wa mbegu hizo.

Alisema tatizo hilo limebainika kuwa kubwa zaidi katika Wilaya ya Kyela ambako wakulima wengi huwa wanahitaji kiwango kidogo cha mbegu kuliko uwezo wao na hivyo wanawalazimisha wafanyabiashara kuwauzia kiasi kidogo.

"Kampuni nyingi zinazalisha mbegu na kuzifungasha kwenye mifuko ya kilo mbili mbili, lakini wauzaji wanapunguza na kuweka kwenye viwango vidogo na kuuza kwa bei ndogo," alisema Nassari.

Alisema kutokana na hali hiyo waliamua kutoa mafunzo hayo kwa wazalishaji na wasambazaji wa mbegu za mazao mbalimbali ndani ya mkoa huo.

Naye mtafiti wa mahindi katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Leonard Sabula, alisema mbali na kitendo hicho cha wafanyabiashara kuchakachua mbegu hizo pia wengine wanauza mbegu bila kuwa na vibali.

Alisema wengi wa wafanyabiashara hao huwa wanasingizia gharama kubwa za kupata kibali kutoka Tosci na kwamba hao ndio wanaoongoza kwa kuchakachua mbegu hizo.

# Wateja wa umeme waonywa dhidi ya 'vishoka'

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji nchini (Ewura), imewataka mafundi umeme wanaofanya kazi ya kuunganisha nishati hiyo kwenye nyumba za watu bila kuwa na vibali kuacha mara.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Ofisa Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, wakati alipokuwa anafungua mafunzo maalumu kwa mafundi wa umeme kutoka katika mikoa ya Mbeya na Songwe kuhusu kanuni za ufungaji wa umeme za mwaka 2019.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Umeme sura ya 131 ya mwaka 2008 kifungu kidogo cha 8(I) (h), ufungaji wa nyaya za umeme ni shughuli inayotakiwa kufanywa na mtu mwenye leseni inayotolewa na Ewura.

Alisema mtu ambaye hana leseni maarufu kama 'kishoka' akikutwa anafanya kazi hiyo anatakiwa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hiyo na kwamba moja kati ya adhabu anazoweza kuzipata ni faini, kwenda jela ama vyote viwili.

"Tunataka mafundi na makandarasi wa umeme kuwa na leseni kwa sababu za kiusalama, umeme ni rafiki wa binadamu, lakini ni hatari kwa anayefanya kazi kwa kutumia umeme au jengo au chombo chochote kinachotumia umeme, hivyo weledi kwa kila mdau ni muhimu," alisema Kaguo.

Alisema kwa sasa tangu ulipoanzishwa utaratibu wa kuwazuia mafundi wasiokuwa na leseni, matukio ya majengo kuungua kutokana na hitilafu za umeme yamepungua kwa kiasi kikubwa na kwamba ndio maana wanawahamasisha mafundi wote kuwa na leseni.

Alisema awali ajali za moto zinazosababishwa na hitilafu za umeme zilikuwa nyingi kwa sababu vishoka walikuwa wengi na walikuwa wanafanya kazi ambazo zinahitaji utaalamu wa hali ya juu na hivyo kuzifanya chini ya kiwango.

Akitoa ufafanuzi wa kisheria, Mwanasheria Mkuu wa Ewura, Nzila Masunga, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Umeme, mtu yeyote akikamatwa anafanya kazi ya kuunganisha umeme bila kuwa na leseni adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano gerezani ama kulipa faini isiyozidi Sh. milioni 10 ama vyote viwili.

Alisema sheria hiyo imezitaja baadhi ya kazi za umeme zinazotakiwa kufanywa na mtu mwenye leseni kuwa ni uzalishaji, usafirishaji, usambazaji, ugavi na uendeshaji wa mifumo ya umeme.

Alizitaka kazi zingine kuwa ni biashara ya umeme kuvuka mipaka ya nchi, kuuza umeme na kuunganisha mifumo ya umeme ambayo alisema mafundi wengi wanaofanya kazi hizo nchini hawana leseni.

Alisema sheria hiyo pia inaeleza kuwa leseni hizo zinatakiwa kutolewa na Ewura pekee na kwamba mamlaka hiyo ndiyo iliyopewa pia kufuta leseni hizo endapo mmiliki atakiuka masharti.

"Kanuni ya 13 inaeleza kwamba Ewura inaweza kusimamisha au kufuta leseni endapo itabainika kuwa mmiliki aliipata kwa kuwasilisha nyaraka za uongo ama za kughushi, kuvunja masharti ya leseni au kukutwa na kosa la jinai linalohusiana na umiliki wa leseni hiyo," alisema Masunga.

Meneja wa Ewura Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Karim Ally, alisema mafunzo hayo ni endelevu na yatafanyika katika mikoa yote sita ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo imebaki.

Alisema katika mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Mbeya, walihudhuria mafundi zaidi ya 130 kutoka katika mikoa yote miwili na mingine yatafanyika katika Mkoa wa Rukwa na watawaunganisha na mafundi wa Katavi na Njombe kwa kuwaunganisha na wa Ruvuma.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, akiangalia stoo ya vinywaji iliyogongwa na lori la mafuta, lililoacha njia baada ya kugongana uso kwa uso na gari dogo, katika eneo la Ilomba, jijini Mbeya usiku wa kuamkia jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanne wanusurika kifo magari yakigongana

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WATU wanne wamenusurika kifo jijini Mbeya baada ya lori la mafuta na gari ndogo kugongana uso kwa uso katika eneo la njia panda ya Ilomba barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), usiku.

Magari hayo ni lori lenye namba za usajili T. 720 DHV lililokuwa linavuta tela lenye namba za usajili T.520 CCY ambalo lilikuwa limesheheni lita 34,000 za mafuta ya petroli na dizeli na gari ndogo aina ya Toyota Carina lenye namba za Usajili T. 536 DDM.

Akizungumza na wandishi wa habari katika eneo la tukio, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwataja watu wawili waliofahamika kuwa ni dereva wa gari la mafuta, Abubakar Mohamed (32), mkazi wa Jiji la Dar es Salaam na dereva wa gari ndogo, Abel Mwaleyego (36) mkazi wa Jiji la Mbeya.

Matei alisema gari kubwa lilikuwa linatokea Jiji la Dar es Salaam kuelekea nchi jirani ya Zambia na gari dogo ilikuwa ikitokea katikati ya Jiji la Mbeya kuelekea upande wa Uyole.

Alisema baada ya magari hayo kugongana, gari la mafuta liliacha njia na kuvamia maduka matatu ya mahitaji ya nyumbani na stoo ya kuhifadhia vinywaji na kwamba hakuna mtu aliyekuwamo kwenye maduka hayo wakati ajali hiyo inatokea.

"Chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa magari yote mawili katika eneo la makazi ya watu na bahati nzuri hakuna hata mmoja aliyepoteza maisha ingawa dereva wa gari ndogo alipata majeraha madogo na amekimbizwa katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya kwa ajili ya matibabu," alisema Kamanda Matei.

Alisema watu wengine wawili waliokuwamo kwenye gari la mafuta majina yao hayakufahamika na wanaendelea kufuatilia afya zao ingawa wanajulikana kuwa wako salama.

Alisema magari yote mawili yaliharibika na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na wananchi, walisaidiana kuzuia wizi wa mali katika eneo hilo.

Akizungumzia ajali hiyo, dereva wa gari la mafuta, Mohamed alisema ana wasiwasi kuwa dereva wa gari dogo alikuwa anayumba yumba njiani na kwamba alihangaika kumkwepa lakini ikashindikana.

Alisema inawezekana dereva wa gari hiyo alikuwa amelewa na kwamba ndio maana alikuwa anayumbayumba sana njiani na alikuwa anamchanganya na mwanga mkali.

"Bahati nzuri wote tuliokuwa kwenye gari niliyokuwa naendesha tulitoka salama, lakini gari imeharibika na namshukuru Mungu kwamba mafuta hayakulipuka," alisema Mohamed.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amewataka wananchi wote wanaofanya biashara pembezoni mwa barabara kuwa makini ili kuepuka kupata madhara ya ajali kama hiyo.





# Wawekezaji waitwa kuwekeza Dodoma

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAWEKEZAJI wametakiwa kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizopo katika Jiji la Dodoma, ili kujenga makao makuu yenye ubora katika sekta zote.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, katika kikao cha tathmini ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji hilo.

Alisema wakati umefika sasa kwa wawekezaji kutambua na kuchangamkia nafasi zilizopo kwa kuwa makao makuu inahitaji kujengwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Dodoma kuna fursa nyingi, tuna miradi ya kimkakati ambayo ipo katika hatua za mwishoni kumalizika zianze kutumika lipo soko, kituo cha mabasi, bustani ya mapumziko ya Chinangali, na kituo cha malori Nala, pia kuna miradi ambayo kulingana na jiji letu kuwa makao makuu," alisema na kuendelea:

"Tumepata neema serikali itajenga uwanja wa ndege na kiwanja cha mpira vyote vyenye hadhi ya kimataifa."

Mahenge alisema lazima kuwe na mipango mikakati mizuri ya kuwawezesha wawekezaji wenye uthubutu.

"Kwa sababu tuna miradi yenye viwango vya kimataifa, hivyo ni lazima huduma zetu za afya, elimu na huduma nyinginezo nazo tuziweke katika hadhi hiyo ili wageni mbalimbali wapate nafasi ya kufurahia uwapo wao ndani ya Jiji letu," alisema.

Alishauri uongozi wa jiji hilo kuhakikisha unaweka mipango kazi itakayowezesha wananchi kufanya shughuli zao ikiwamo maegesho ya magari.

"Kwa mfano ukizunguka maeneo ya mjini kuanzia Barabara Saba na kuendelea sehemu zote zilizotengwa kwa ajili ya kuegesha magari ya wateja hivi sasa wamiliki wa maduka wamegeuza na kuweka magari yao wenyewe," alisema.

Aliomba jiji kuzungumza na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili wawapatie eneo la Jamatini na mengine waliyonayo ya wazi yatumike katika kuingiza mapato kama sehemu ya kuegesha magari.

"Hata wateja wakilipa kwa saa sio vibaya ili eneo la mjini libaki kuwa wazi bila msongamano wa magari," alisema.

Aidha, mkuu huyo alimtaka Mkurugenzi wa Jiji kuweka usimamizi mzuri wakati wa ugawaji wa maeneo katika miradi ya kimkakati kwa wafanyabiashara.

# Wanafunzi shule wasioona Buigiri waiangukia serikali

**Na Augusta Njoji, CHAMWINO**

SERIKALI imeombwa kuongeza ruzuku katika Shule ya wasioona Buigiri iliyopo Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma ili kutatua kero zinazowakabili ikiwamo kuchakaa kwa majengo na kukosekana kwa mafuta ya mashine za nukta nundu.

Ombi hilo lilitolewa jana na wanafunzi wa shule hiyo walipokuwa wakizungumza na gazeti hili.

Mmoja wa wanafunzi hao, Daniel Japhet, alisema majengo yaliyopo yamechakaa na ruzuku inayotolewa na serikali haitoshi kutatua matatizo waliyonayo.

Naye mwanafunzi Anthony Stephano, alisema karatasi za nukta nundu ni chache na hata mashine zinapoharibika hakuna fedha ya kutengeneza kutokana na ruzuku kutotosheleza mahitaji yao.

Kwa upande wake, Mandwe Dickson, alisema serikali kujenga uzio kwenye shule hiyo kutokana na kuishi kwa hofu.

Akizungumzia kuhusu kero hizo, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Samuel Jonathan, alisema ufinyu wa bajeti ndio unaosababisha washindwe kutatua kero zinazoikabili shule hiyo.

"Kuna wakati tunakosa hata fedha ya matibabu, watoto wanaokaa hapa shuleni wengi wao wanatoka kwenye familia duni," alisema.

Kadhalika, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, alisema kwa sasa serikali inahakikisha inawaweka pamoja watoto wenye mahitaji maalum na watoto wengine.

"Lengo ni kwamba watoto ambao hawana changamoto hizo watambue tu kuwa kuna wenzao wenye mahitaji maalum, lakini watoto hawaishi kwa pamoja," alisema.

Kuhusu changamoto za shule hiyo, Mweli alisema mkakati wa uboreshaji miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi wa uzio linafanyika kwa awamu kwenye shule zenye mahitaji maalum.

"Tumefanya Makalala, Pongwe Tanga na pia Bohangijwa Shinyanga, kwa hiyo huu ni mkakati endelevu tutaendeleea kuhakikisha shule zinazochukua watoto wenye mahitaji maalum tunatatua changamoto zao," alisema.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Kichina ya Stecol Corporation, wakiendelea na ujenzi wa mradi wa jengo la hoteli ya nyota tatu, mali ya Jiji la Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwalimu adakwa tuhuma za kusafirisha wahamiaji haramu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Kifaru, mkoani Kilimanjaro, Kelvin Mpoli (39), anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, kwa tuhuma za kusafirisha wahamiaji haramu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema mwalimu huyo na Mkazi wa Kilema Moshi, Cathbert Kirita (58), alikamatwa juzi wakisafirisha wahamiaji haramu watatu kutoka Kilimanjaro kwenda Songwe kupitia njia ya Dodoma.

"Hawa walikamatwa juzi katika kijiji cha Mtera wilayani Mpwapwa, wakiwa na wahamiaji haramu watatu ambao ni raia wa Kenya wenye asili ya Somalia," alisema.

Alieleza kuwa Watanzania hao walikamatwa wakisafirisha wahamiaji kwa kutumia gari namba T. 248 AWA, Nissan Patrol rangi nyekundu.

Aliwataja wahamiaji haramu hao ni Abdulrahman Mohamed (25), Luul Mohamed (30) na Hawa Gedow (18) ambao wameingia nchini bila kibali.

Katika tukio jingine, Muroto alisema Februari 3, mwaka huu, katika kijiji cha Chinene Wilaya ya Chamwino walikamatwa pia wahamiaji haramu sita raia wa Somalia waliokuwa kwenye gari la abiria namba T.858 DAP, mali ya Kampuni ya Capricorn, kutoka Arusha kwenda Mbeya.

Alisema wote walikuwa na hati za kusafiria kutoka Kenya, lakini walitiliwa shaka na kubainika waliingia nchini bila uhalali.


"Hawa walifikisha mahakamani kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji mkoani Dodoma," alisema.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muroto alisema kwa kupitia operesheni mbalimbali, wamekamata watuhumiwa watano kwa kosa la unyang'anyi wa pikipiki katika maeneo ya Dodoma.

"Mtandao huo umenaswa na watu watano wanashikiliwa na Jeshi la Polisi na tunaendelea na mahojiano zaidi kupata mali zilizoibiwa na washiriki wengine," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kutoa taarifa za uhalifu ili kusafisha tatizo la uhalifu Dodoma.

"Pia wananchi ambao wameibiwa vitu vyao waje kituo cha Polisi kutambua mali zao wakiwa na vithibitisho vya kumiliki mali hizo," alisisitiza.



# Mawaziri wa SADC kujadili maafa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKUTANO wa kwanza wa kamati ya mawaziri wenye dhamana wa masuala ya kukabiliana na maafa wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini wa Afrika (SADC) unatarajiwa kuanza leo Mjini Zanzibar ambao unarajiwa kufunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein.

Akizungumza jana na wanahabari, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili, wa Rais Muhamed Aboud Muhamed, alisema mkutano huo unafanyika kutokana na umuhimu mkubwa wa mawaziri wa nchi hizo kujadili na kuweka mikakati ya pamoja namna bora ya kukabiliana na matukio ya maafa yanayoukabili ukanda huo kikiwamo kimbunga, mafuriko, ukame na ajali za barabarani.

Alisema athari za kimbunga aina ya Kennedy katika nchi za Madagascar, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe vimepelekea vifo vya maelfu ya watu na wengine kutoonekana kabisa na kupelekea mahitaji ya kiasi cha dola bilioni 10 za Marekani kwa ajili ya kurejesha hali ya awali.

Alisema mkutano huo umekuja katika kipindi ambacho nchi nyingi wanachama wa ukanda huo zimekuwa zikiathiriwa na majanga ya asili mara kwa mara, na kusababisha madhara makubwa hali iliyoonesha umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika kukabiliana na maafa.

"Mara nyingi athari zinazotokana na majanga ya kimaumbile yakiwamo ukame, mafuriko, maradhi ya mlipuko na mengineyo hupelekea gharama kubwa katika kurejesha hali, baada ya kutokea," alisema Aboud.

Aidha, alieleza kuwa katika hatua ya kujenga mataifa yenye uhimili katika kukabiliana na maafa, SADC imefanikiwa katika kuimarisha mifumo ya tahadhari za mapema inayoendana na majanga na hali ya hewa kwa kuandaa vikao vya mwaka kwa nchi wanachama kwa ajili ya kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa. Alisema pia wanaandaa mipango ya dharura na kutoa mafunzo ya utafutaji wa uokozi kwa majanga ya bahari kwa nchi wanachama.

Alieleza kuwa SADC imetekeleza programu ya ufanyaji wa tathmini na uchambuzi wa usalama wa chakula kwa nchi wanachama 14 zilizoathiriwa na majanga yanayoendana na hali ya hewa, ukiwamo ukame.

"Pia SADC imeandaa mpango na mikakati yote hiyo ni kwa ajili ya kupunguza athari za maafa katika kanda hii... mwaka 2017/2018 watu wapatao milioni saba waliathiriwa na maafa, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na watu milioni 17 walioathirika katika miaka ya 2015/2016.

Alieleza kuwa kwa upande wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, imeshakamilisha kuandaa nyaraka zote muhimu katika masuala ya kukabiliana na maafa ikiwamo sheria ya taifa ya kukabiliana na maafa namba 7 ya mwaka 2015, sheria ya kukabiliana na maafa Zanzibar namba moja ya mwaka 2015 na sera za kukabiliana na maafa.

Alisema pia imeandaa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa na mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa, na rasimu ya mkakati wa kukabiliana na maafa pamoja na kuanzisha vituo vya mawasiliano na operesheni za dharura na vituo vya ukozi hasa kwa majanga ya baharini.



Waziri asiye na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib (wa pili kushoto), akizungumza na baadhi ya wageni waliofika katika Baraza la Wawakilishi, kwa ajili ya kusikiliza kikao cha baraza hilo, jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Zanzibar, Balozi Mohamed Hamza, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mohamed Muombwa (wa pili kulia) na mfanyakazi mstaafu wa Shirika la Ndege za Serikali, Amour Jeri. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shule mpya kumaliza msongamano darasani

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema kuwa serikali imejenga shule mpya katika eneo la Wingwi Pemba na Mwanakwerekwe Unguja kufuatia wingi wa watoto katika maeneo hayo, hivyo kusababisha msongamano wa wanafunzi darasani.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Riziki Pembe Juma, wakati akijibu swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid.

Mwakilishi huyo alihoji kutakuwa na utaratibu gani ambao utatumika kwa wanafunzi wa kila mkoa kusoma katika shule iliyomo ndani ya mkoa wake kwa lengo la kupata nafasi kwa kila mwanafunzi ndani ya eneo husika.

Waziri Pembe alisema wanafunzi watakapofaulu katika mitihani yao kutoka maeneo hayo, watapewa kipaumbele kikubwa kujiunga na shule hizo.

Alisema vituo vya ubunifu wa sayansi vitakuwa na uongozi wake na vitatumika na wanafunzi kutoka shule za karibu na kituo husika.

Aidha, alieleza kuwa serikali imefuta michango ya wazee kwa shule zote za msingi na sekondari ili kutoa fursa kwa watoto wote kupata elimu bila ya ubaguzi.

Alieleza kuwa suala la kuzisaidia shule kujiendeleza litakuwa chini ya serikali, hivyo ruzuki zitaendelea kutolewa hata baada ya mradi kumalizika.

# Wafungwa, mahabusi wafunguka kero kibao

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

VIONGOZI wa Idara ya Msaada wa Kisheria na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wamefanya ziara ya kutembelea Makao Makuu ya Vyuo vya Mafunzo Kilimani (Magera), kusikiliza matatizo yanayowakabili wafungwa na mahabusi wa chuo hicho.

Viongozi hao wakiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhan, walishtushwa na idadi kubwa ya mahabusu ambao ni nguvu kazi ya Taifa.

Viongozi hao walisema wengi wa mahabusi hao wanatoka Mahakama za Mwanzo za Manispaa kwa makosa madogo baada ya kushindwa kulipa faini na kunyimwa dhamana.

Wakizungumza na maofisa hao, baadhi ya mahabusi walisema wamepelekwa hapo kwa tuhuma za uzururaji, uzembe na kulewa wakati wa kazi na wengine wamebambikiziwa kesi za dawa za kulevya, kulawiti na kubaka.

Rashid Salum, mahabusi, alisema wanapokamatwa kwa makosa ya uzembe na kulewa hupelekwa mahakama za mwanzo na hutakiwa kulipa Sh. 50,000 hadi 70,000 bila kupewa nafasi ya kujitetea na wanaposhindwa hupelekwa mahabusu.

"Nipo mahabusu tokea mwezi uliopita kwa kushindwa kulipa faini ya Sh. 70,000 kwa kosa la kulewa mchana... ni afadhali hakimu angenifunga nikamaliza muda nikatoka kuliko hali hii," alisema Rashid Salum kutoka Magogoni.

Alieleza kuwa idadi ya mahabusi ni kubwa na kipindi cha joto kinachoendelea hivi sasa hali sio nzuri katika vyumba vya kulala.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhani Said, alishauri kufanywa juhudi za makusudi kupunguza idadi ya mahabusi kwa kuwapa dhamana wale wenye haki ya kupewa dhamana.

Wakili wa Serikali Mkuu, Ali Ali, alisikitishwa na tabia ya kuwakamata na kuwafungulia tena mashtaka watuhumiwa wanaoachiliwa huru na mahakama baada ya kushinda kesi zao.

Alisema utaratibu huo sio mzuri, kwani watuhumiwa hao huachiwa baada ya hakimu kujiridhisha kuwa kesi zao hazina ushahidi na nyingine ni za kubuni.

Mwanasheria Mkuu wa Vyuo vya Mafunzo, Seif Makungu, alisema Idara yake imekuwa ikifanya kila juhudi kuhakikisha haki za binadamu hazivunjwi wanapowahudumia wafungwa na mahabusi pamoja na wenye matatizo ya afya hupatiwa matibabu na wengine hupelekwa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

Mkuu wa mapokezi ya mahabusi na wafungwa wa Chuo cha Mafunzo Kilimani, Mzee Nassor, alishauri kuwekwa kifungu mbadala cha sheria kumwezesha Jaji Mkuu kutoa dhamana kwa makosa yasiyokuwa na dhamana baada ya kufutwa kifungu 151 cha mwenendo wa makosa ya jinai.

# Wauguzaji wagonjwa walalamikia hospitali

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

WAUGUZAJI wagonjwa wanaolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wamelalamikia kitendo cha kushinda juani na kunyeshewa na mvua kutokana na kufukuzwa wodini inapotokea wagonjwa wao wamezidiwa.

Wamedai kutokana na hali hiyo, wagonjwa wengi ambao hulazwa wakiwa wamezidiwa wamekuwa wakikosa usaidizi kutoka kwa wauguzi wa hospitali hiyo, jambo ambalo limekuwa likihatarisha usalama wao.

Kufutia uwapo wa zuwio hilo, wauguzaji wamekuwa wakishinda juani na hata kunyeshewa na mvua nje ya uzio wa hospitali hiyo na wengine kulala katika eneo hilo kwa ajili ya kusubiri kuitwa na wauguzi, inapotokea mabadiliko ya hali ya mgonjwa na muda wa kuingia wodini ili kuwaona wagonjwa wao.

Hadija Hasan, alisema aliwahi kupeleka majamzito hospitanili hapo kwa ajili ya kujifungua, lakini baada ya kufukuzwa, aliporudi alikuta mgonjwa wake amefariki dunia pamoja na mtoto wake.

Alisema katika ufuatiliaji wa tukio hilo, alielezwa kuwa mgonjwa huyo aliita muda mrefu wauguzi wamsaidie kupokea mtoto wake baada ya kujitahidi kusukuma.

Alisema katika hali hiyo ya kukosa usaidizi mtoto mchanga aliyezaliwa alidondoka chini kutoka kitandani, hali ambayo ilisababisha mama huyo kutokwa na damu nyingi kutokana na mtoto kuvuta mfuko wa uzazi bila utaratibu.

Alipotakiwa kuzungumzia malalamiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, alidai kutokuwa na taarifa hizo na kuomba apewe muda wa kufuatilia na kutoa taarifa baada ya kukamilisha.

"Hilo naomba nilichukue, nitatuma timu yangu kwa ajili ya kulifanyia kazi na kulipatia ufumbuzi wa kudumu," alisisitiza Balyomi.

Hata hivyo, alisema ofisi yake inaandaa utaratibu wa kuwajengea eneo la kuegesha magari, pikipiki na baiskeli wagonjwa na wauguzaji kuwapunguzia adha hizo.

# TPSF yaguswa kasi utendaji wa JPM

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), imepongeza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Rais John Magufuli, ikiwamo kubadilisha fikra za kiutendaji miongoni mwa watumishi wa umma kuelekea uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza baada ya kuzinduliwa kwa Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Songwe sambamba na Kitabu cha Muungozo wa Uwekezaji wa mkoa huo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Godfrey Simbeye, alisema katika kipindi cha miaka minne tu utendaji kazi wa watumishi umebadilika na kurudisha imani kubwa kwa sekta binafsi.

"Siyo kitu rahisi kubadilisha fikra ya mtu kwa kipindi kifupi, lakini utendaji kazi wa Rais Magufuli na dhamira yake ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 imeweza kubadilisha fikra na mitazamo ya watumishi wa umma," alisema Simbeye.

Alisema katika vikao vingi ambavyo vinawashirikisha watendaji kutoka sekta za umma na binafsi vimekuwa na mafanikio mengi, kwani kumekuwa na kuelewana katika majadiliano na pia kutatua changamoto mbalimbali bila vikwazo.

"Leo tunakaa meza moja na kukubaliana namna ya kufanikisha utekelezaji wa mambo mbalimbali kwa faida ya Taifa. Hakuna urasimu wala ukiritimba katika ofisi za serikali kama ilivyokuwa hapo awali," alisema Simbeye.

Simbeye alisema Rais Magufuli kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, anafanya kazi nzuri kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyorudisha nyuma ukuaji wa uwekezaji na biashara vinaondolewa.

"TPSF itaendelea kuwa imara na kutoa mchango stahili katika ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda kama ilivyokusudiwa kwa ustawi wa maendeleo ya Tanzania na watu wake wote," alisema na kuongeza kuwa Songwe ni eneo lenye fursa nyingi za uwekezaji mbali kuwa lango kuu katika nchi za ukanda wa SADC.

Waziri Kairuki alisema sekta binafsi imetoa mchango mkubwa katika kufanikisha Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Songwe, na kwamba wakati umefika kuchangamkia fursa za uwekezaji na biashara mkoani humo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Godfrey Simbeye (kushoto), alipotembelea banda la taasisi hiyo wakati wa kongamano la uwekezaji linalofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usajili wa haki bunifu wahimizwa

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), umesema bado Watanzania wengi hawajajua maana ya haki bunifu hivyo kushindwa kusajili kazi zao za kiubunifu ili waweze kunufaika nazo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyaisa, wakati wa uzinduzi wa Shahada ya Uzamili ya Haki Bunifu ambayo imeanza kufundishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Uzinduzi wa Shahada hiyo ulifanyika jana chuoni hapo na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali wa mashrikia ya kimataifa ya haki miliki kama Shirika la Haki Miliki Afrika (ARIPO) na Shirika la Haki Miliki Duniani (WIPO).

Nyaisa alitoa mfano wa Watanzania wanaotengeneza asali nzuri lakini wanaziweka kwenye vifungashio vya chupa za kampuni nyingine hivyo kupoteza haki zao.

Alisema uzinduzi wa shahada hiyo unafungua ukurasa mwingine wa kulinda na kuhifadhi haki za wagunduzi hasa kwenye Chuo cha Sayansi na Teknolojia.

Alisema kuna umuhimu kwa wadau kuhamasisha watu kusajili kazi zao na kuongeza idadi kutoka 30 kwa mwaka hali ambayo inaonyesha kuwa kumekuwa na idadi ndogo ya wagunduzi na wavumbuzi wa vitu.

Hata hivyo, Nyaisa alisema kwa upande wa usajili wa biashara na huduma, Tanzania iko kwenye nafasi nzuri zaidi ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika ingawa alisema hali hiyo haiwezi kuwafanya wabweteke.

"Kama tunavyofahamu kwamba serikali ya awamu ya tano inatekeleza sera ya ujenzi wa viwanda hivyo haki miliki itakuwa na umuhimu mkubwa sana kwenye kulinda bidhaa na huduma zetu zinapovuka mipaka yetu kwenye masoko ya kimataifa," alisema.

Nyaisa aliahidi kuwa katika mwaka ujao wa fedha, miongoni mwa vipaumbele vya Brela itakuwa ni kutoa elimu kupitia semina mbalimbali na makongamano maeneo ya mijini na vijijini ili wananchi wengi wajue kuhusu haki miliki na waweze kusajili kazi zao.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema kuanzishwa kwa masomo hayo kunaendana na masomo ya chuo hicho kufikia mwaka 2061.

Alisema UDSM imejizatiti kifedha na kirasilimali watu kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa masomo hayo kama kukarabati madarasa yatakayotumika na majengo watakayotumia kwenye kampasi ya maeneo ya Mikocheni.

Profesa Anangisye alisema kwa miaka mingi, UDSM imekuwa ikisaidia jitihada za kulinda haki miliki kwa hapa nchini na kimataifa na kwa hapa nchini UDSM ilikuwa ya kwanza kuweka sera ya haki miliki mwaka 2008.

**HABARI KIMATAIFA**

# Simulizi ya Mwafrika aliyepona virusi corona

**YAOUNDE,** Cameroon

KEM Senou (21) Mwanafunzi raia wa Cameroon anayeishi katika mji wa Jingzhou, China ambaye aliambukizwa virusi vya ugonjwa wa Corona sasa amepona.

Anakuwa ni mgonjwa wa kwanza mwenye asili ya kiafrika kupona ugonjwa huo baada ya kuambukizwa.

Anasema wakati anapatiwa matibabu mjini humo aliwaeleza madaktari kuwa hata asipopona ugonjwa huo hatarudi nchini Comeroon kwani asingependa kuona wananchi wengi wakipata ugonjwa huo.

"Chochote kitakachofanyika sitaki kupeleka ugonjwa Afrika," alisema akiwa katika chumba chake cha malazi katika Chuko Kikuu, ambako ametengwa kwa siku 14.

**Sitaki kurudi nyumbani hadi nikamilishe masomo yangu. Nadhani hakuna haja ya kurudi nyumbani kwasababu gharama zote za hospitali zimesimamiwa na serikali ya China.**

Alikuwa anaugua homa kali, kukohoa na kuonyesha dalili za mafua. Alipokuwa mgonjwa alikumbuka namna alivyopata malaria akiwa mtoto Cameroon. Alihofia sana maisha yake.

Alitibiwa kwa antibiotiki na dawa za kutibu wagonjwa walio na virusi vya Ukimwi, HIV. Baada ya wiki mbili ya uangalizi alianza kuonesha dalili ya kupona. Uchunguzi wa kimatibabu wa CT scan haukuonesha dalili zozote za ugonjwa.

Misri ni nchi ya kwanza ya Afrika kuthibitisha kupata mtu aliyeambukizwa virusi vya corona.

Wataalamu wa Afya wameonya kuwa nchi zilizo na mifumo hafifu za matibabu huenda zikakabiliwa na changamoto ya kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo, ambavyo vimesababisha vifo vya watu zaidi ya 1,600 na wengine zaidi ya 68,000 kupata maambukizi.

"Sitaki kurudi nyumbani hadi nikamilishe masomo yangu. Nadhani hakuna haja ya kurudi nyumbani kwasababu gharama zote za hospitali zimesimamiwa na serikali ya China," alisema Senoua.

Tangu Januari, serikali za mataifa tofauti duniani, zikiongozwa na Marekani, zilianza mpango wa kuwaondoa raia wao kutoka mji wa Wuhan na miji mingine jirani. **BBC**



Kem Senou (21) Mwanafunzi raia wa Cameroon ambaye aliambukizwa virusi vya Corona wakati akipatiwa matibabu. **PICHA: REUTERS**

# Pompeo ziarani Afrika, atoa ujumbe

**ACCRA,** Ghana

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, amefanya ziara Afrika katika nchi za Senegal, Angola na Ethiopia, na kueleza kuwa nchi yake itashirikiana na Afrika kupambana na ugaidi.

Alisema serikali ya Rais Donald Trump inajaribu kutathmini idadi ya wanajeshi wa Marekani inayohitajika Afrika Magharibi kupambana na vurugu za makundi yenye misimamo mikali ya kidini katika eneo hilo.

Pompeo alisema Marekani itashirikiana na Senegal na mataifa mengine ya Afrika Magharibi pamoja na Ufaransa kupambana na kitisho kinachotokana na vurugu za makundi ya kigaidi.

Waziri huyo wa Marekani alihitimisha ziara yake nchini humo juzi kwa mkutano wa pamoja na waandishi wa habari akiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Senegal, Amadou Ba.

Pompeo alisema Marekani inaitegemea Senegal kushirikiana nayo kupambana na ugaidi wa misimamo mikali ya Kiislam, na kwamba itaendelea kutoa mafunzo kwa askari wa kulinda amani nchini Senegal.

"Nimezungumza na viongozi wa Senegal kuhusu ugaidi wa makundi yenye misimamo mikali ya Kiislam, ambao unahatarisha maisha ya watu milioni 350 hapa Afrika Magharibi. Unahatarisha pia maisha ya Wamarekani. Tunaitegemea Senegal," alisema Pompeo.

Kwa upande wake Ba alithibitisha wasiwasi ulioko kuhusu ugaidi, na jinsi unavyosambaa kwa kasi Afrika Magharibi.

Alisisitiza kwamba serikali ya Senegal na ya Marekani zitashirikiana kumaliza vitisho kwa amani ya kikanda na ya ulimwengu kama vile ugaidi na uhalifu wa kuvuka mipaka.

"Afrika kwa sasa inatikiswa na mizozo mingi na utulivu hauwezi kupatikana bila Waafrika. Hali inavyoendelea nchini Libya ni mfano mzuri," alisema Ba.

Baada ya kukamilisha ziara yake Senegal, Pompeo aliondoka na kuelekea Angola na anatarajia kwenda Ethiopia, ikiwa ni mojawapo ya juhudi za kutaka kuzuia ushawishi wa China na Urusi pamoja na mataifa mengine yenye nguvu duniani barani Afrika.

Akiwa Angola, Pompeo atakutana na Rais wa nchi hiyo, Joao Lourenco, anayepambana na sakata la rushwa linalomhusisha mtoto wa kiongozi wa zamani wa nchi hiyo, Isabel dos Santos.

Baada ya hapo, Pompeo ataelekea Ethiopia, taifa la pili barani Afrika lenye idadi kubwa ya watu wapatao milioni 100 na pia ndiko yaliko makao makuu ya Umoja wa Afrika. **DW**

## Walioambukizwa Corona wafikia 70,000, vifo 1,770

**BEIJING,** China

IDADI ya walioambukizwa virusi vya Corona nchini China imefikia watu elfu sabini.

Taarifa iliyotolewa na maofisa afya nchini humo inaeleza kuwa idadi ya vifo kutokana na virusi hivyo imeongezeka na kufikia watu 1,770.

Kulingana na Tume ya Afya nchini China kulikuwa na zaidi ya maambukizi 2,000 na vifo vya watu 105 katika kipindi cha saa 24.

Idadi hiyo ya waliofariki hadi kufikia jumapili imezidi kushuka kidogo ikilinganishwa na Jumamosi ambapo watu 142 walifariki, huku idadi ya walioambukizwa ikidaiwa kuongezeka kidogo.

Hapo jana mji wa Hubei ambao ndiyo kitovu cha virusi hivyo ulianzisha hatua nyingine kali zaidi zinazolenga kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Hatua hizo mpya zinajumuisha kuendelea kuwadhibiti watu wasitoke nje kwa saa 24 na pia kuweka marufuku ya magari yote barabarani isipokuwa yale yanayotoa huduma za dharura. **DW**

## Mwanamuziki wa injili ajinyonga

**KIGALI,** Rwanda

JESHI la Polisi nchini Rwanda, limesema kwamba msanii maarufu wa nyimbo za injili, Kizito Mihigo amejinyonga akiwa mahabusi.

Kwa mujibu wa tangazo la polisi, maiti ya msanii huyo imepatikana katika chumba alimokuwa anazuiliwa kwenye kituo cha polisi mtaa wa Remera, mjini Kigali.

Polisi imesema kwamba Mihigo alijinyonga siku tatu baada ya kukamatwa karibu na mpaka baina ya Rwanda na Burundi katika kile ambacho polisi ilisema alikuwa na nia ya kutoroka nchi na kujiunga na makundi ya waasi dhidi ya Rwanda.

Alikuwa ameanza kufanyiwa uchunguzi kuhusu madai hayo pamoja na kutaka kuwahonga wananchi waliomkataa.

Mwaka jana Mihigo aliachiwa huru kwa msamaha wa Rais Pul Kagame baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 10 jela kwa hatia ya kutaka kumuua rais na kuhamasisha raia kupinga serikali.

Kumekuwa na hisia tofauti katika mitandao ya kijamii kuhusiana na kifo cha ghafla cha msanii huyo wa muziki wa injili huku baadhi ya watu wakitaka majibu kutoka kwa serikali.

Mihigo aliyekuwa na miaka 38 alipata umaarufu kutokana na nyimbo zake kama vile 'Inuma' ambao unaelezea kifo ni nini. **BBC**

# Mashine zanunuliwa kudhibiti Corona

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

WATEDAJI wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamesema wamenunua mitambo maalumu za kuchunguza virusi vya magonjwa hatari yanayoambukizwa kwa njia ya virusi yakiwamo Ebola na Corona.

Mashine hizo zitapelekwa katika nchi wanachama kwa ajili ya kusaidia kudhibiti magonjwa hayo.

Naibu Katibu Mkuu wa EAC, anayeshughulikia miundombinu, Mhandisi Steven Mlote, alisema juzi kuwa mitambo hiyo imeshafika katika makao makuu ya Jumuiya hiyo na utaratibu wa kupelekwa kwa nchi wanachama unafanyika.

Alisema watazikabidhi mashine hizo Februari 29, mwaka huu kwenye mkutano wa wakuu wa nchi hizo unaotarajiwa kufanyika Jijini Arusha

Licha ya jitihada za kupambana na magonjwa hayo kufanyika, Mlote alisema hadi sasa hakuna taarifa zozote za kuwapo kwa Ebola wala Corona katika nchi wanachama.

Katika hatua nyingine, serikali mkoani Arusha imesema taarifa zinazoenea kwenye mitandao ya kijamii za kuwapo kwa mtu mmoja mkazi wa Ngaramtoni, Moses Mollel anayejiita Nabii Namba Saba anayedai kugundua dawa ya kutibu ugonjwa wa Corona si za kweli.

Akizungumzia taarifa hizo ofisini kwake jijini hapa, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema ngazi zinazohusika zimefuatilia na kubaini kuwa mtu huyo hana uwezo huo na kwamba kwa sasa anaendelea kuhojiwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Wedson Sichalwe, alisema maelezo ya awali ya mtu huyo kudai kuwa ameoteshwa na Mungu, alipotakiwa aonyeshe dawa anayodai kuwa inatibu ugonjwa huo, alishindwa kufanya hivyo.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, akizungumza wakati kushiriki kifungua kinywa cha pamoja na wafanyakazi wa Manispaa ya Kinondoni kilichoandaliwa na NMB kwa ajili ya kujenga uhusiano. Kushoto ni Mkuu Kitengo cha Wateja Binafsi, Omari Mtiga na Kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji wakaribishwa Songwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA) imewahimiza wawekezaji kutumia fursa kubwa za uwekezaji zilizopo Mkoa wa Songwe kuanzisha viwanda ambavyo ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa uchumi wa nchi.

Ofisa Mwandamizi Uhamasishaji na Uwekezaji wa EPZA, Nakadongo Fares, amesema katika Jukwaa la Fursa za Uwekezaji Mkoa wa Songwe mwisho wa wiki kuwa Mamlaka ya EPZA ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wawekezaji katika viwanda kuweza kufikia lengo lao.

"Mamlaka ya EPZA imekuwa ikifanya kazi na uongozi wa Mkoa wa Songwe ili kuweka mazingira wezeshi na kuvutia uwekezaji katika viwanda kwenye mkoa ambao umejaliwa kuwa na vivutio vingi. Mwekezaji anapata uhakika wa soko pana la ndani, ukanda wa Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla," alisema.

Kadhalika alisema, Mamlaka ya EPZA hutoa huduma zote ambazo mwekezaji kwenye viwanda anastahili kupata hivyo kuwahakikishia mazingira bora zaidi watakapoenda kuwekeza katika mkoa huo.

Alisema kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji ni muhimu kwa sababu wawekezaji wote duniani ni sawa na ndege ambaye huruka kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kutafuta sehemu ambayo atafanya biashara katika gharama ndogo na kupata faida kubwa.

Fares alisema Mamlaka ya EPZA ambayo ipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, itaendelea kufanya kazi na mikoa yote nchini ili kuvutia uwekezaji hasa katika maeneo maalum ya SEZ na EPZ ambayo ni muhimu katika kujenga uchumi imara wa viwanda.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila, alisema wawekezaji watakaowekeza mkoani humo watafaidika na soko kubwa nchini la zaidi ya watu milioni 60 na zaidi, pia soko kuwa la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), lenye watu zaidi ya milioni 400.

"Tunawakaribisha sana wawekezaji katika Mkoa wa Songwe kuwekeza katika viwanda ili kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli ambaye ni mwenyekiti wa SADC ya kujenga uchumi imara wa viwanda na kuwaondoa wananchi katika lindi la umaskini," alisema.

Alisema Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), inazitaka nchi za Afrika kuwekeza katika miundombinu kama ifanyavyo Tanzania ili kuongeza kiwango cha biashara kwenye nchi hizo na zilizoendelea.

# Wapigwa 'stop' kuuza vyakula karibu na shule

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wadogo wa chakula karibu na shule za msingi na sekondari katika Tarafa ya Moshi Magharibi mkoani Kilimanjaro, wako katika wakati mgumu baada ya serikali kuweka zuio.

Ofisa Tarafa ya Moshi Magharibi, Senzia Lushino, alisema juzi kuwa kutokana zuio hilo, kuanzia sasa ni marufuku kuuzwa kwa vyakula hivyo katika tarafa anayoiongoza.

Alisema atawakamata wafanyabiashara wote wanaouza vyakula katika shule hizo kwa kuwa wao ndio chanzo kikuu cha tamaa kwa watoto wa kike kujiingiza katika uhusiano wa kingono.

"Nitawakamata na kumweka ndani mfanyabiashara yeyote wa chakula atakayekaidi amri hii kuanzia sasa. Watoto wengi wa kike wanaopata mimba ni kwa sababu hawana pesa ya kununua vitu vya kula kula wakiwa shuleni. Kwa hiyo wakiviona pale hurubuniwa na wanaume kwamba kula hiki, kunywa hiki ni rahisi ndiyo maana tumeweka zuio," alisema Lushino.

Alipotafutwa kutoa mtazamo wake kuhusu zuio hilo, Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Nguvu ya pamoja ya Kutetea Wanawake na Watoto katika Mkoa wa Kilimanjaro kupitia Shirika la kiraia la Kwieco, Veronica Ullomi, alisema zuio hilo la serikali ni mtazamo mpya kuhusu mimba za utotoni, ukiangazia si tu tabia za watoto hao kama sababu hizo za mimba, bali pia vitendo vya familia zao, jamii na serikali.

Mwanaharakati huyo alisisitiza zaidi kuwa: "Zuio hilo limekuja wakati mwafaka kwa sababu mimba za utotoni huathiri afya, elimu na haki za watoto wa kike.

"Mtoto wa kike asiye na elimu atakuwa na ugumu kupata ajira na kujijengea maisha bora na familia yake na msichana anayeshika mimba akiwa na umri chini ya miaka 18, haki zake zitakuwa zimekiukwa.

"Familia zisizojiweza ndizo zinazoingia makubaliano na familia ya mwanamume na wengine wanaogopa kutoa taarifa polisi kwa sababu ya kulinda undugu na ujirani mwema," alisema Ullomi.

**Zuio hilo limekuja wakati mwafaka kwa sababu mimba za utotoni huathiri afya, elimu na haki za watoto wa kike.**

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. MWENYE NYUMBA **0757 804 970**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**FATUMA MWIDINI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.4023/0017 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RUVU STATION SEKONDARI mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/URA/403942/2019.

115633402

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo - KINGOLWIRA-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;07/2020**

Ombi la MARRY EFATA META Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MBONEA SADIKIEL MSANGI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/02/2020.

15634002

## KUPOTEA KWA CHETI



**YOHANA S. MBISE** AMEPOTELEWA NA CHETI CHA ELIMU YA KIDATO CHA NNE, ALICHOSEMEA KTK SHULE YA PRESBYTERIAN SEMINARY. ALICHOMALIZA MWAKA 2012 NA CHENYE INDEX NO, S.1330-0095.
KWA YEYOTE ATAKAEKIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KTK KITUO CHOCHOTE CHA POLISI,
TAARIFA YA POLISI: KGD/PS/B.1/1/21/VOLXX111/228.

156335

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo - CHAMWINO-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;10/2020

Ombi la AHMED.N.MKOBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANZAE HUSSENI GUNGUTI, Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/02/2020.

Sahihi ya Hakimu

115633602

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo - MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;48/2020

Ombi la **PASKAZIA JOHN KATO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LINUS GEORGE MDEDE,Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 12/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/02/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115633702

## KUPOTEA KWA KADI

**Irene Cecil Mtoi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya DAIHATSU-TERIOS yenye namba ya usajili wa namba T771 ASU iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/STA/RB/24714/2020

125633102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DAVID JOHNSON CHANGAE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 488 ACF SUZUKI SAMURAI. Chassis namba SJ80120280. Engine namba G13BA664504.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/144197/2020.

115632802

## PRO SHARE CAPITAL LIMITED

**GARI LINAUZWA**

1. RACHEL JUMA JUMBE (TOYOTA PROGRESS T766 DES)

115633202

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MAOMBI NA.330 YA 2019
BAINA YA
JUMA ABDALAH MUSA ………………MUOMBAJI
DHIDI YA
DIONDI MADEJE alias BEYOND MADEJE……MDAIWA

KWA:- DIONDI MADEJE alias BEYOND MADEJE
POPOTE ULIPO
YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anruhusiwa kisheria tarehe 09.03.2020 saa3.00 asubuhi.Kwa kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO:-kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 5 ya mwezi wa Februari, 2020.

115633302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo - KINGOLWIRA-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;02/2020

Ombi la SHABANI SAIDI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMADI IDD GOHEZA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/02/2020.

115633802

## KUPOTEA KWA KADI

Caroline Alfred Mkemwa anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA BELTA yenye namba ya usajili wa namba T 800 DSL iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/URA/RB/144804/2020

115632902


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SOLSKJAER: UTD ITAPETA USAJILI HATA ISIPOFUZU UEFA

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inaweza kuwavutia wachezaji bora duniani ikishiriki au kutoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa mujibu wa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

United imepanga kutumia fedha nyingi kwenye usajili mwishoni mwa msimu huu wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakiendelea kusuasua kwenye Ligi Kuu ya England wakiwa nafasi ya tisa wakipitwa pointi 41 na vinara Liverpool.

Nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, mkali wa Leicester City, James Maddison na nahodha wa Aston Villa, Jack Grealish ni miongoni mwa wachezaji wanaohusishwa na kutakiwa United, ambao wamepitwa pointi sita kwenye nne bora.

Huku akijua kwamba kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kutaifanya klabu hiyo kuwasajili kwa urahisi nyota wakubwa, kocha huyo aliyekalia kuti kavu, Solskjaer amesisitiza United bado ina nguvu ya kuvutia wachezaji wakubwa.

"Ligi ya Mabingwa inaipa klabu vyanzo vingi, fedha nyingi, hicho ni kitu kimoja," alisema Solskjaer kabla ya mchezo wa jana Jumatatu dhidi ya Chelsea.

"Ni michuano mikubwa kuwapo bila shaka yoyote, lakini bado Man United inaweza kuvutia wachezaji wakubwa.

"Lakini tukiendelea kucheza vizuri kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki, naamini wachezaji ambao tunawahitaji tutawapata tu bila tatizo lolote."




# Sterling haendi Madrid-Wakala

**MANCHESTER,** England

RAHEEM Sterling kwa sasa akili yake ni kuichezea Manchester City, kwa mujibu wa wakala wake baada ya ripoti kudai anahusishwa na mpango wa kwenda Real Madrid.

Uvumi kuhusu majaliwa ya wachezaji kadhaa pale City umesambaa kwa kasi baada ya klabu hiyo kufungiwa kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu miwili kwa kuvunja sheria ya usawa wa matumizi ya fedha.

Sterling, ambaye mkataba wake na City unamalizika mwaka 2023, ameripotiwa kuwaniwa na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Madrid.

Lakini wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, Aidy Ward, amesema Sterling kwa sasa akili yake ipo kwa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya England.

"Raheem kwa sasa bado ana mkataba na Manchester City na ataendelea kuwa hapa kwani mkataba wake bado unamruhusu kuendelea kucheza hapa," alisema akiliambia gazeti la Daily Mail.

Sterling, aliwasili hapo City akitokea Liverpool mwaka 2015, na amefunga mabao 20 katika mechi 35 kwenye mashindano yote msimu huu.

# Arteta hawaombei mabaya City

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesisitiza "haiombei mabaya" Manchester City kwa kufungiwa kucheza michuano inayoandaliwa na UEFA baada ya Arsenal kuifumua Newcastle United na kujivuta kwenye nafasi zenye uwezekano wa kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya.

Kocha huyo msaidizi wa zamani wa City, alishuhudia kikosi chake kikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Newcastle Jumapili, lakini taarifa kwamba kikosi cha Pep Guardiola wanakabiliwa na adhabu ya kufungiwa miaka miwili kushiriki mashindano ya Ulaya zilitawala wikendi yote.

Wakati City imetangaza mpango wa kukata rufani, kuna uwezekano wa timu itakayoshika nafasi ya tano kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku zile zitakazocheza Ligi ya Europa kupata nafasi hiyo hata ile itakayoshika nafasi ya nane.

Arsenal wapo nafasi ya 10 kwenye msimamo baada ya mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Pierre-Emerick Aubameyang, Nicolas Pepe, Mesut Ozil na Alexandre Lacazette, lakini Arteta hafikiri kwamba hiyo ni nafasi ya kuwaombea mabaya waajiri wake hao wa zamani.

"Hatujui chochote kuhusu hilo," alisema akiiambia Sky Sports. "Tutatakiwa kusubiri na kuona.

"Ni jambo gumu. Siwaombei mabaya. Napenda waepuke hali hiyo, nawatakia heri Manchester City, heri kwa Pep na heri kwa wachezaji.

"Nawapenda sana watu wa pale na nina kumbukumbu nzuri wakati nilipokuwa pale. Kitu pekee kinachotaka kutoka kwao ni kuwa kwenye wakati mzuri."



# Klopp abainisha kuihofia Atletico

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amezungumzia heshima yake kwa Diego Simeone wakati wakielekea kwenye mchezo wao pale katika dimba la Wanda Metropolitano, akisema alikuwa na wakati unaofanana na kocha huyo wa Atletico Madrid.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya England watacheza na Atletico mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora leo, Jumanne.

Liverpool wanarudi kwenye hatua hiyo baada ya kushinda taji hilo kwenye fainali ya mwaka jana, na wanajiandaa kupambana na Atletico kikosi ambacho kinasuasua kwenye Ligi Kuu ya Hispania.

Lakini Klopp bado anamheshimu Simeone na Atletico, ambao wameshinda mchezo mmoja tu kati ya michezo saba iliyopita kwenye mashindano yote.

"Tofauti yao ya mabao kwenye LaLiga ni kwamba wamefunga 25 tu ambapo ni mengi, lakini wameruhusu 17, ambapo ni machache," alisema akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Wana tatizo kubwa la majeruhi katika wiki za hivi karibuni, wanawakosa washambuliaji wengi. Lakini (Alvaro) Morata alikuwa benchi (dhidi ya Valencia Ijumaa), nimesikia (Diego) Costa amerudi kwenye mazoezi na Joao Felix yupo.

"Kama kuna mtu ambaye anacheza kwa ajili ya matokeo tu ni Atletico na Simeone, na nawaheshimu.

"Tulikuwa na wakati kama huo. Tulijaribu sana na bado tunajaribu. Napenda hivyo.





# COURTOIS AFURAHIA KURUDI KWA HAZARD

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard alirudi dimbani baada ya kuwa nje kwa miezi mitatu na alitoa mchango wakati Real Madrid ikitoka sare ya kufungana 2-2 na Celta Vigo, huku Thibaut Courtois akiamini kwamba fowadi huyo atakuwa nguzo ya kikosi hicho cha Zinedine Zidane.

Majeruhi ya enka yalimuweka benchi Hazard tangu Novemba, lakini alirudi uwanjani Jumapili na kupata penalti iliyofungwa na Sergio Ramos na kuiweka Madrid mbele kwa mabao 2-1 kipindi cha pili.

Ushindi wa Madrid katika mechi tano mfululizo kwenye Ligi Kuu ulihitimishwa na bao la Santi Mina la dakika 85 na matokeo kuwa sare, ingawa wanaongoza kwenye msimamo kwa pointi moja dhidi ya wapinzani wao wa Clasico, Barcelona.

Hata hivyo, kurudi kwa Hazard, ambaye amefunga bao moja tu katika mechi tisa za Ligi tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea Chelsea kabla ya kuanza kwa msimu huu kulionekana kuwa na manufaa kwa mchezaji mwenzake Courtois.

"Kidogo ataweza kurudi kwenye kiwango chake baada ya miezi mitatu," alisema Courtois, ambaye alicheza na Hazard pale kwenye dimba la Stamford Bridge, akiiambia Movistar.

# *Gerrard asubiria adhabu ya Man City kuporwa taji EPL*

**LONDON,** England

STEVEN Gerrard amebainisha "ana hamu kubwa" kuona kama hatua itachukuliwa dhidi ya Manchester City na kupokonywa ubingwa wao wa Ligi Kuu ya England wa mwaka 2014.

City imefungiwa miaka miwili kushiriki michuano inayosimamiwa na Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), baada ya kuvunja sheria ya usawa wa matumizi ya fedha, huku klabu hiyo ikiwa imekata rufani kwa Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo, CAS.

Kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kinaweza kupoteza ubingwa wao wa mwaka 2014 kama uchunguzi wa Ligi Kuu England utabaini kwamba walivunja sheria hiyo ya fedha - ambapo watatakiwa kupokwa pointi.

"Nimesoma asubuhi hii," alisema kocha huyo wa klabu ya Rangers, Gerrard, ambaye alikuwa nahodha wa Liverpool wakati walipomaliza nafasi ya pili wakipitwa pointi mbili nyuma ya City mwaka 2014, wakati timu yake iliposhinda dhidi ya Livingston.

"Tutasubiri na kuona. Adhabu ya UEFA kwa uhakika ni kubwa. Nina uhakika watakata rufani na tutaona nini kitatokea.

"Halafu tutaona kama Ligi Kuu ya England nao watachukua hatua. Lakini kama ukiangalia adhabu ya UEFA, kuna kitu fulani hakipo sawa.

"Hivyo, nina hamu kubwa ya kuona matokeo yake. Hadi nitakapoona adhabu kutoka Ligi Kuu ya England."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# 'RONALDO HAWEZI KUCHEZA MECHI 75'

●●● Asema kocha Sarri akitoa sababu ya kumsugulisha benchi wakati Juve ikishinda dhidi...

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri ameelezea uamuzi wake wa kumpumzisha Cristiano Ronaldo wakati Juventus ikishinda 2-0 dhidi ya Brescia, akisema mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, "hawezi kucheza mechi 75" kwa mwaka.

**Ronaldo aliachwa nje ya kikosi baada ya kufunga mabao 10 katika mechi sita za hivi karibuni za Serie A alizocheza na hivyo kufikisha mabao 20 msimu huu, lakini Paulo Dybala na Juan Cuadrado waliziona nyavu juzi, Jumapili wakati alipopumzishwa.**

Sarri pia aliwakosa majeruhi Douglas Costa, Federico Bernardeschi, Sami Khedira, na Merih Demiral, lakini Giorgio Chiellini alicheza mechi yake ya kwanza tangu Agosti, mwaka huu akitokea benchi katika kipindi cha pili.

Kocha wa Juve, Sarri alimwacha nje nyota huyo wa Ureno, Ronaldo akiamini anahitaji muda wa kupumzisha miguu yake kutokana na kazi kubwa aliyoifanya akiwa na timu yake ya taifa na klabu.

Sarri alisema: "Ni vigumu; tunao wachezaji wengi imara na wengine wapo nje.

"Wote ni wachezaji wazuri, bila jukumu maalum. Tunayo hali nyingi za kurekebisha.

"Ronaldo ni mshambuliaji wa kati ambaye anatokea pembeni. Leo [juzi] Cristiano anapaswa kupumzika; hawezi kucheza mechi 75 kuna mwaka kati ya timu ya taifa na klabu, hivyo tumeamua kumuacha apumzike."

Kuhusu Chiellini, aliongeza: "Alijiweka kwenye timu. Alikuwa ameyasema hayo tangu jana [juzi]. Alitoa miezi sita ya dhabihu kubwa."

Sarri alikiri kiwango cha kikosi chake dhidi ya Brescia kimetoa nafasi kubwa ya kujizatiti baada ya kushuhudia mabingwa hao wa Serie A wakipata ushindi wa pili pekee kati ya mechi tano.

Kipigo dhidi ya Napoli na Hellas Verona huku ikishinda dhidi ya Fiorentina kabla ya sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya Coppa Italia dhidi ya Milan na kisha ushindi dhidi ya Brescia Jumapili, sasa Juve inajiandaa kuivaa SPAL Jumamosi na Ronaldo akijiandaa kucheza mechi yake ya 1,000 kwenye wasifu wake kisoka.

"Tunaweza kujizatiti kwa kila kitu," alisema Sarri. "Kuhusu kiwango cha safu ya ulinzi tunayo nafasi ya kujizatiti. Pia tunao nafasi ya kujizatiti kwa upande wa ushambuliaji.

"Tuligongesha mlingoti mara tano katika mechi mbili zilizopita, bahati kidogo zaidi ingeweza kutusaidia. Lazima tuzingatie wenyewe, badala ya kuwatazama wengine."

## ZISIKUPITE

### HAITAMKIMBIZA GUARDIOLA

PEP Guardiola ataendelea kubaki kuwa kocha wa Manchester City hata kama ikishindwa kupindua adhabu yao ya kufungiwa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha miaka miwili. ***(Mirror)***

### LIVER BADO KWA WERNER

RB Leipzig imesisitiza Liverpool haijafanya mawasiliano yoyote na kuhusu kumpata mshambuliaji wao, Mjerumani Timo Werner, 23, ambaye amefunga mabao 20 Bundesliga msimu huu. ***(Transfermarkt via Mirror)***

### MAGALHAES AIANIKA ARSENAL

BEKI wa Lille, Gabriel Magalhaes, 22 anayewindwa na Arsenal na Everton, amesema kuwa atapenda "kucheza" klabu yoyote ya Ligi Kuu England. ***(Sun)***

### STERLING ATULIZWA CITY

WAKALA wa winga wa Manchester City, Raheem Sterling, 25, amesema nyota huyo wa kimataifa wa England hawezi "kusumbuliwa na mazungumzo yoyote ya kuhamia klabu yoyote kwa sasa". ***(Mirror)***

### CHAMBO YA MARTINEZ

BARCELONA inaweza kumjumuisha Antoine Griezmann katika dili lolote la kuijaribu Inter Milan kuwauzia Lautaro Martinez. Nyota huyo wa Argentina, 22, ameripotiwa kuwa na kipengele kinachomruhusu kuuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 92. ***(Sun)***

### SOLSKJAER AITOA HOFU UTD

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer hafikirii kukosa kukosa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kutaiathiri klabu hiyo katika mipango yao ya usajili wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### UEFA KUKIMBIZA NYOTA CITY

MANCHESTER City imekiri kwamba baadhi ya wachezaji wake watahitaji kuondoka mwishoni mwa msimu kama kifungo cha klabu hiyo kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya hakitaondolewa. ***(Telegraph)***

### IGHALO ANUKIA JUMLA UTD

OLE Gunnar Solskjaer amesema mshambuliaji raia wa Nigeria, Odion Ighalo, 30, aliyetua Man United kwa mkopo akitokea Shanghai Shenhua anaweza kununuliwa jumla na klabu hiyo. ***(Manchester Evening News)***

### DEL PIERO AVUTA GUARDIOLA

NGULI wa Juventus, Alessandro del Piero anaamini Pep Guardiola atakuwa "vizuri tayari" kwa klabu ya Serie A. Kocha huyo Man City amekuwa akihusishwa na kuchukua nafasi ya Maurizio Sarri pale Turin. ***(Sky Sports)***

### INTER YAMFUATA CHONG

INTER Milan ipo katika mazungumzo ya kumsajili winga wa Manchester United na Uholanzi U-21, Tahith Chong, ambaye atamaliza mkataba hapo Old Trafford majira haya ya joto. ***(Tuttosport, via Sun)***

### MORRISON AITWA JAMAICA

KIUNGO wa Sheffield United, Ravel Morrison, 27, ambaye anacheza kwa mkopo Middlesbrough, anajiandaa kucheza mechi ya kimataifa baada ya kuitwa timu ya Taifa ya Jamaica kwa mechi ya kirafiki dhidi ya Catalonia itakayopigwa Barcelona Machi 30, mwaka huu. ***(Sheffield Star)***

HABARI MICHEZO

## Mngazija amrithi Seif ukocha KVZ

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ inayopo katika mchakamcha wa kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, imemtangaza Ali Bakari Mngazija kurithi mikoba ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Mohamed Seif, ambaye ameomba kupumzika kukinoa kikosi hicho.

Akizungumza na gazeti hili jana, mratibu wa timu hiyo, Hassan Haji alisema Kocha Mngazija kwa sasa atakuwa kocha mkuu wa timu hiyo katika kipindi hiki cha kuelekea mwishoni mwa msimu wa 2019-2020.

Alisema anaamini kocha huyo ataweza kuyaendeleza mafanikio ya timu hiyo ili iweze kufanya vizuri zaidi katika mzunguko huu wa lala salama ambao kila timu inapigana vikali iweze kubaki Ligi Kuu.

"Tumepata kocha mwingine, hii haimaanishi kocha wa awali hakufaa, hapana alikuwa na mchango mkubwa katika timu ya kvz, ila mwenyewe aliandika barua ya kuomba kupumzika na ndio tukamtafuta kocha mpya," alisema.

Aidha, alisema KVZ kwa sasa inafanya vizuri ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza uliomalizika ambao walikuwa wakipata matokea mabaya ya kufungwa na kutoka sare jambo lililokuwa likiwapa wasiwasi mkubwa mashabiki wa timu hiyo.

Hata hivyo amewataka mashabiki na wachezaji wa KVZ kumpa hamasa kocha huyo ili timu iweze kufanya vizuri zaidi katika mzunguko huu wa lala salama.

Kibarua cha kwanza kwa Mngazija kitakuwa leo dhidi ya KMKM katika Uwanja wa Amaan, wakati huu timu hiyo ikiwa nafasi ya sita na alama zake 21 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

## ZFF yatangaza timu za vijana

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAIMU Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Mohed Seif Kingi, ametangaza timu endelevu za vijana zenye umri tofauti ambazo zinatarajiwa kuanza kufanya mazoezi kwa wiki mara mbili katika Uwanja wa Amaan.

Timu hizo za umri chini ya miaka 15, 17 na 20, wachezaji wake wengi wanachezea madaraja ya chini.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema katika mipango ya kuziendeleza timu hizo ili ziwe na mafanikio, zitacheza mechi mbalimbali za ndani ya Zanzibar na nje kwa timu za vijana zenye umri kama huo ambazo zipo katika ligi za vijana.

Alisema licha ya kuanza kupata wachezaji waliopo Unguja, lakini wanatarajia kufanya ziara mbalimbali katika mikoa yote ya Zanzibar ili kupata wachezaji wenye uwezo wa kucheza soka la vijana.

"Ili kuipa uhai wa timu hizi ziwe endelevu lazima ziwe zinacheza mechi mbalimbali kwa pamoja na si kutegemea mechi za timu zao kupitia madaraja wanayocheza," alisema.

# TWIGA STARS KUHAMISHIA MOTO KWA MOROCCO LEO

**Na Somoe Ng'itu,** TUNISIA

HAKUNA kulala! Hayo ndio maneno ya Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, kuelekea mchezo wa Kombe la UNAF dhidi ya Morocco utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kram jijini Tunis kuanzia majira ya saa 9:15 mchana kwa saa za Tanzania.

**Twiga Stars itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mechi zake mbili zilizotangulia dhidi ya Mauritania (7-0) na Algeria (3-2) matokeo ambayo ya meiweka kileleni wakiwa na pointi sita wakati Morocco wao wana pointi tatu mkononi baada ya kushinda mechi ya kwanza dhidi ya wenyeji, Tunisia.**

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Shime alisema mechi ya leo ndio fainali yake na amejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri na kupata pointi tatu muhimu.

Shime alisema amewaangalia na kuwasoma vizuri Morocco katika mechi yao ya kwanza ambayo pia walishinda, hivyo anafahamu ubora na udhaifu wa kikosi chao.

Kocha huyo alisema wanawaheshimu wapinzani wao wote, lakini amewataka wachezaji wake kucheza katika kiwango cha juu ili watimize malengo waliyojiwekea ya kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano haya.

"Sio kama tumeshinda mechi mbili hatuna makosa, la hasha, kuna vitu tuliviona na tumevirekebisha, naamini wachezaji wangu watapambana kuhakikisha tunapata ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri," alisema Shime.

Aliongeza kuwa kazi bado wanayo na ushindi pekee katika mechi ya leo ndio utawaweka jirani na ubingwa wa michuano hii.

"Si tu kwamba tutaipeperusha na kuipa sifa Tanzania, pia tutakuwa tumeiwakilisha vema kanda yetu ya Cecafa kama wageni waalikwa, tunaamini hatutawaangusha, kila mchezaji yuko tayari kwa mapambano," Shime alisema.

Nahodha wa Twiga Stars, Asha Rashid, alisema malengo yao ni kuweka rekodi nzuri ya kutwaa kombe la mashindano hayo wakiwa wanashiriki kwa mara ya kwanza.

"Mechi itakuwa ngumu, kila timu inaimarika tofauti na tulivyowaona katika mechi ya kwanza, tunaahidi kujituma zaidi na kuhakikisha tunawapa furaha Watanzania, kwetu ni heshima kupata nafasi ya kushiriki mashindano haya, malengo makubwa tuliyonayo ni kuweka rekodi nzuri," Asha alisema.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa mapema leo mchana itakuwa ni kati ya Mauritania dhidi ya Algeria wakati Twiga Stars itashuka kucheza mchezo wake wa mwisho Jumamosi jioni dhidi ya Tunisia.

UPEPO...




Baadhi ya wanariadha wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mashindano ya wazi kutafuta nafasi ya kushiriki mashindano ya madola yatakayofanyika nchini Japan baadaye mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal itavuna 3 popote - Mgunda

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, ametamba kuwa anahitaji pointi tatu popote pale anapokwenda kucheza mechi za Ligi Kuu na si nyumbani tu bali pia ugenini.

Mgunda ametoa kauli hiyo wakati huu akiikaribisha Ruvu Shooting katika Uwanja wa Mkwakwani leo, akitoka kuiangamiza Azam FC ugenini kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kwa mabao 2-1 katika mechi iliyopita.

Ushindi huo umempa jeuri kocha huyo na kutamba kuwa wataendelea kupambana popote pale na kupanda juu ya msimamo wa Ligi Kuu msimu huu wakati huu wakishika nafasi ya nne kwenye msimamo wakiwa na alama 38 baada ya mechi 22.

Alisema kwa hatua ya ligi ilipofika ni ngumu, hivyo hawapaswi kuangalia ni mechi gani wanatakiwa kushinda zaidi ya kujiwekea malengo ya kupambana kushinda michezo yote.

"Watu wengi wanasema Coastal inashinda katika Uwanja wa Mkwakwani tu, kwangu si kweli msimu huu tumejiwekea mikakati ya kokote tutakapokwenda tunahitaji alama muhimu ili kufikia malengo yetu," alisema.

Mgunda alisema kwa sasa wapo Tanga kujiandaa na michezo yao miwili ambapo wakianza na Ruvu Shooting leo kabla ya Jumapili kuikaribisha Yanga katika Uwanja wa Mkwakwani.

Alisema anahitaji kupata pointi sita katika michezo hiyo miwili ya nyumbani ili kujihakikishia anamaliza msimu timu yake ikiwa katika nafasi nne bora katika msimamo wa ligi hiyo.

Michezo
Jumanne Februari 18, 2020
Nipashe



'Ronaldo hawezi kucheza mechi 75'
UKURASA 30

HAINA KUFELI...



Mshambuliaji wa Aston Villa na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akiucheza mpira kwa kichwa dhidi ya beki wa Tottenham Hotspur, Toby Alderweireld, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Villa Park juzi na wageni hao kushinda 3-2. Kulia ni Jack Grealish. **PICHA NA MTANDAO**

# YANGA YAGEUKIA POINTI ZA SIMBA

●●● Eymael akiri ni mlima mkubwa akiitangazia vita Polisi Tanzania, Sven yeye moto kwa Kagera...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga leo kikiwa na kibarua kigumu ugenini dhidi ya Polisi Tanzania, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Luc Eymael amekiri wana mlima mrefu wa kupanda ili kuzifikia pointi za vinara wa Ligi Kuu Bara, Simba walioopo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakiwa na alama 56.

**Yanga iliyoshuka dimbani mara 20, mechi mbili nyuma ya Simba, ina pointi 39 ikiwa katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo na alama tano nyuma ya Azam FC iliyopo nafasi ya pili baada ya kucheza michezo 22.**

Na wakati leo ikishuka katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi dhidi ya wenyeji wao hao, Eymael amesema atalazimika kutumia vema mechi hiyo na tatu zijazo ili kupunguza wigo wa pointi hizo kabla ya kuvaana na Simba.

Yanga kabla ya kukutana na Simba Machi 8, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa, itakuwa na kibarua cha mechi nne dhidi ya Polisi Tanzania leo, Coastal Union (ugenini), Alliance na Mbao, zote jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo uliopita dhidi ya Polisi Tanzania, timu hizo zilitoka sare ya mabao 3-3, mechi ambayo ilishuhudiwa 'Hat-trick' ya kwanza msimu huu ikipatikana baada ya Ditram Nchimbi kucheka na nyavu mara tatu kabla ya kujiunga na Yanga kwenye usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza na Nipashe kabla ya kikosi kuelekea Moshi, Eymael aliliambia Nipashe kuwa ana mlima mkubwa wa pointi anazodaiwa na Simba jambo ambalo linamfanya apasue kichwa kufikiria namna ya kumalizana nao.

Alisema mipango yake ni kushinda mechi nne zijazo ikiwamo ya leo, Coastal Union, Alliance na Mbao ambazo watazitumia kupunguza wigo huo wa pointi, lakini kurekebisha mapungufu kabla ya kukutana na watani zao hao.

"Kushinda mechi zote zilizobaki inawezekana endapo wachezaji watafuata maelekezo ninayowapatia, tuna mechi nyingi kabla ya kukutana na Simba na zote hizo ni ngumu, hivyo lazima tupambane kwa mpangilio mzuri, mechi hizo zitatupa hali ya kujiamini na kutengeneza kikosi maalumu kitakachotupa nguvu ya kuiangamiza Simba.

"Nimewaambia kwamba silali kwa ajili ya kuwaza mbinu mpya za kushinda mechi zetu, ili kufikia malengo ya kila mdau wa Yanga anayoyatamani kuona timu yake hiyo inafanya vizuri na mwisho wa siku tunashiriki michuano ya kimataifa," alisema.

Naye mchezaji wa Polisi Tanzania, Pato Ngonyani, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na kila timu kuhitaji matokeo mazuri na kwa upande wao watapambana kupata alama tatu.

"Mchezo utakuwa mgumu kutokana na Yanga wataingia kwa presha ya kuvuna pointi tatu kwetu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yao, lakini sisi tunajitoa kupambana kutafuta alama hizo kwa kujiweka katika mazingira mazuri ya kutoshuka daraja," alisema Ngonyani.

Na wakati Eymael akiumiza kichwa kuishika Simba kileleni, Mbelgiji mwenzake wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu, Sven Vandenbroeck amesema mkakati wao mkubwa ni kuvuna alama tatu kwa wapinzani wanaokutana nao, na imani hiyo ikiongezeka kutokana na ari ya wachezaji wake kujituma uwanjani.

"Mpango wetu ni kuona tunaendelea kupata matokeo mazuri kwenye mechi zetu zote tutakazocheza bila kuwa na visingizio," alisema Sven ambaye atakiongoza kikosi chake dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Taifa leo saa 1:00 usiku huku akiwa na kumbukumbu ya kuichapa 3-0 kwenye mzunguko wa kwanza.

## Kagere amwahidi Mo, mashabiki

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuusoma ujumbe wa mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohammed 'Mo' Dewji, na kuutafakari, mshambuliaji kinara wa mabao, Meddie Kagere amesema wao kama wachezaji wana deni kubwa la kumpa furaha yeye, uongozi mzima sambamba na mashabiki wote.

Kegere ametoa kauli hiyo baada ya Mo kutumia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii kuweka video ya mchezo wa Simba ilivyocheza na Al Alhy kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika Uwanja wa Taifa msimu uliopita.

Katika ujumbe huo Mo aliandika: "Tukumbushane, Al Ahly ndio timu iliyoshinda mataji mengi zaidi katika Klabu Bingwa Afrika. Hii ndio Simba ikicheza kwa kujituma na kupambana mwanzo mwisho, goli lilifungwa na MK14 [Meddie Kagere] kwenye CAFCL."

Akizungumza na Nipashe baada ya kauli hiyo, Kagere alisema wanapambana kila mechi kutafuta pointi tatu si tu kwa lengo la kumfurahisha bosi wao huyo, bali pia uongozi mzima na hasa mashabiki ambao mara zote wanakuwa nao pamoja.

Alisema malengo makubwa kwao ni kutetea taji la ubingwa, hivyo inawalazimu kupambana kila mechi kupata pointi muhimu kufikia kila kinachotarajiwa na mashabiki.

"Ni kweli tuliondolewa Ligi ya Mabingwa katika hatua ya mapema, tunaahidi furaha pia tuna deni kubwa la kulipa, Inshallah tutafikia malengo," alisema Kagere ambaye hadi sasa yupo kileleni mwa wafungaji wa ligi hiyo akiwa na mabao 12.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >